Mtu ambaye ni wa dini lakini hauzuii ulimi wake - Yakobo 1:26.  
Ajionaye kuwa mweny hekima - 1 Kor. 3:18.  
Asemaye kuwa hana dhambi - 1 Yoh. 1:8.  
Adhaniaye kwamba wasio haki wataupokea ufalme wa Mungu - 1 Kor. 6:9.  
Mtu anayeshirikiana na waovu - 1 Kor. 15:33.  
Yule atafutaye kupanda kwa mwili na kuvana uzima wa milele - Gal. 6:7, 7.

### **Hofu (Uchaji, Woga)**

#### Hofu Takatifu -- Heshima Na Uchaji Kwa Mungu Kwa Sababu Ya Tabia Yake:

### Kwa Nini Watu Wamche Mungu?

Kwa kuwa yeye ni Mtakatifu na wa haki - Ufu. 15:4.  
Kwa sababu ya ukuu wake - Dum. 10:12, 17, 1 Pet. 1:17.  
Kwa kuwa hana upendeleo - Kum. 10:17, 20; Mdo. 10:34, 35; Rum. 2:11.  
Kwa sababu ya wema wake - 1 Sam. 12:24.  
Kwa sababu ya msamaha wake - Zab. 130:4.  
Kwa sababu ya matendo yake makuu - Yohua 4:23, 24.  
Kwa sababu ya hukumu yake - Ufu. 14:7.  
Kwa kuwa ana uwezo wa kuwatupa waovu Jehanum - Luka 12:5.

### Jukumu la watu kwa kumcha Mungu:

Chanzo cha maarifa nikumcha Bwana - Mit. 9:10.  
Mcheni Bwana Mungu na kumtukiza - Ufu. 14:7.  
Kicho cha Bwana ni kitakatifu - Zab. 19:9.  
Kumcha Bwana ni kuchukua uovu - Mit. 8:13.  
Tunapaswa kumtumikia pamoja na unyenyekevu na kicho - Ebr. 12:28.  
Twautimiza utakatifu katika kumcha Bwana - 2 Kor. 7:1.  
Waovu hawana hofu ya Bwana - Zab. 36:1; Mit. 1:29; Rum. 3:18.  
Wakristo wanapaswa kutenda kazi ya Bwana kwa kuogopa na kutetemeka - Flp. 2:12.  
Wanapaswa kuenenda kwa hofu katika safari waliyo nayo - 1 Pet. 1:17.  
Wanapaswa kutoa majibu yao kwa upole na kwa hofu - 1 Pet. 3:15.  
Kunyenyekeana katika kicho cha Kristo - Efe. 5:21.  
Kumcha na kuzishika amri zake ndiyo impasayo mtu - Mhubiri 12:13.

### Mifano ya baadhi ya waliyomcha Bwana:

Ibrahimi - Mwa. 22:12.  
Yusufu - Mwa. 39:9.  
Nuhu - Ebr. 11:7.  
Kanisa la kwanza - Mdo. 9:31.  
Mataifa waliyomwabudu Mungu waliitwa “wale waliyomcha Mungu” - Mdo. 10:2; 13:16, 26.

### Baraka za wale wanaomcha Mungu:

Rehema zake ni kuu kwa wamchao - Zab. 103:11, 13.  
Yule amchaye Mungu an kutenda haki hukubaliwa na yeye - Mdo. 10:35.  
Kumcha Mungu ni kuacha kufanya dhambi - Kutoka 20:20.  
Kumcha Bwana ni chemchemi ya uzima - Mit. 14:27.  
Bwana huwaridhia wao wamchao - Zab. 147:11.  
Kwa kumcha Bwana watu hujiepusha na maovu - Mit. 16:6.  
Heri mtu yule amchaye Bwana - Zab. 112:1.

Hofu ya wanawake hulipamba Neno la Mungu - 1 Pet. 3:2.

### Kuwaogopa Wanadamu:

Pilato alimtoa Yesu kwa kuwa aliwaogopa wanadamu - Yn. 19:8.  
Kwa sababu ya kuwaogopa Mafarisayo, wengine waliacha kumfuata Yesu - Yn. 7:13; 9:22; 12:42, 43.  
Kristo anatuambia kwamba hatupaswi kuogopa - Yn. 14:27.  
Hatupaswi kuogopa wala kufadhaika kwa kuwa Mungu ya pamoja nasi - Isa. 41:10; 43:1.  
Mwenye mwili atatutenda nini ikiwa Mungu ni msaidizi wetu? - Zab. 56:4; Ebr. 13:5, 6.  
Wale walio pamoja nasi ni wengi kuliko maadui zetu - 2 Fal. 6:16.  
Waoga watatupwa katika ziwa la moto - Mt. 10:33; Ufu. 21:8.

### Hofu Ya Wenye Dhambi Kwa Sababu Ya Hukumu Na Adhabu:

Watenda dhambi huogopa hukumu ya Mungu:

Adamu alijificha kwa sababu ya woga - Mwa. 3:8-10.  
Belshaza aliogopa sana - Dan. 5:5, 6.  
Feliki alishikwa na hofu - Mdo. 24:25.  
Wengine watajaribu kuukimbia utisho wa Mungu - 1 Sam. 2:19; Ufu. 6:15-17.  
Dhamiri mbovu huleta hofu - Mit. 28:1; Law. 26:17, 36.

Wakristo dhafu huonywa na mifano ya wengine:

Watendao dhambi kanisani wanapaswa kukemewa mbele ya watu wote ili wengine waogope - 1 Tim. 5:20.  
Wakristo wanapaswa kuogopa wawaonapo wenzao wa - kianguka - Rum. 11:20.  
Wanapaswa kuogopa wasije wakaikosa raha ya Bwana - Ebr. 4:1.  
Wale watendao dhambi kusudi wanaitazamia hukumu yenye kutisha (Kuogofya) - Ebr. 10:26-31.

Walakini, wale wampendao Mungu kwa moyo wote hawana hofu au woga kama huo:

Kristo huwaacha huru wale walio utumwani kwa hofu ya mauti - Ebr. 2:14, 15.  
Wakristo hawapokei Roho ya utumwa iletayo hofu - Rum. 8:15.  
Mungu hakutupa roho ya woga - 2 Tim. 1:7.  
Pendo lililo kamili huitupa nje hofu - 1 Yoh. 4:18.

## **Hukumu**

### Hukumu Ya Mungu:

Hukumu za Mungu ni za kweli na haki - Ufu. 16:7; 19:2; 1 Pet. 2:23.  
Mungu ataleta hukumuni kila tendo la mtu - Mhu. 12:14; Rum. 3:5, 6; 2:6.  
Mungu atauhukumu ulimwengu kwa mtu yule aliyemchagua ambaye ni Kristo - Mdo. 17:42.  
Bwana Mhukumu wa haki - 2 Tim. 4:8.  
Ataketi katika kiti cha utukufu wake na kuyahukumu mataifa yote - Mt. 25:31-33.  
Maneno yake ndiyo yatakayowahukumu wanadamu katika siku ile ya mwisho - Yn. 12:48.  
Alipokuja hakuja kuhukumu, bali alikuja kuwaokoa wanadamu - Yn. 3:17; 12:47.

Lakini kuja kwake katika siku ile ya mwisho, nikuwatenganisha walio haki na wasio haki - Mt. 10:34.  
Hivyo, Yesu alisema, “Mimi nimekuja ulimwenguni humu kwa hukumu” - Yn. 9:39.

#### Kuna Hukumu Ya Wakati Huu:

Shetani alihukumiwa wakati Yesu alipokufa msalabani - Yn. 12:31; 16:8-11.  
Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu - Rum. 1:18; Yn. 3:36.  
Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao hao watendao dhambi kwa kusudi - Rum. 1:24, 26, 28.  
Yule ambaye hamwamini Kristo, amekwisha kuhukumiwa - Yn. 3:17; 3:18.  
Wale waliopenda giza kuliko nuru, walihukumiwa - Yn. 3:19.  
Watu wa Mungu huhukumiwa na kuadhibiwa, ili kwamba wasije wakahukumiwa pamoja na ulimwengu - 1 Kor. 11:31, 32; Ebr. 12:6-11.

#### Lakini Hukumu Ijayo Itakuwa Katika Siku Ile Kuu Ya Mwisho:

Bwana atakuja pamoja na watakatifu wake, hesabu yao yapata 10,000, ili afanye hukumu juu ya watu wote - Yuda 14-15.  
Atakuja pamoja na malaika wa uweza wake ili awaadhibu waovu - 2 The. 1:7-9.  
Mbingu zitatoweka, na dunia itateketezwa kwa moto - 2 Pet. 3:10.  
Nchi na mbingu zitaukimbia uso wa Mungu - Ufu. 20:11.  
Wote waliokufa watafufuliwa na kuhukumiwa - Ufu. 20:12-15.  
Watu wote wa kila taifa watakusanyika mbele zake - Mt. 25:31.  
Kila mut atatoa habari zake mwenyewe mbele za Bwana - Rum. 14:12.

#### Siku Ya Hukumu Imeitwa:

Siku ya Mungu - 2 Pet. 3:12.  
Siku ya Bwana - 2 Pet. 3:10.  
Siku ya Bwana Yesu - 1 Kor. 5:5  
Siku ya Kristo - Flp. 2:16.  
Siku ile - 2 The. 1:10.  
Siku ya mwisho - Yn. 12:28.  
Siku ile kuu - Yuda 6.  
Siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu - Rum. 2:5.  
Siku iliyo kuu ya hasira yao - Ufu. 6:17.  
Siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi - Ufu. 16:14.  
Siku ya hukumu - 1 Yoh. 4:17.

#### Watu Wote Watahukumiwa:

Wafu na waliohai - 2 Tim. 4:1; 1 Pet. 4:5.  
Hata malaika nao pia watahukumiwa - 2 Pet. 2:4; Yuda 6.  
Mungu Mhukumu wa wote - Ebr. 12:23.



Waasherati na uzinzi - Ebr. 13:4.  
Wale ambao hawakuiamini kweli - 2 The. 2:12.  
Atawahukumu watu wake - Ebr. 10:30.  
Hukumu itanzia katika nyumba ya Mungu - 1 Pet. 4:17.  
Waalimu watapata hukumu iliyo kubwa - Mk. 12:40; Yak. 3:1.  
Watu wamewekewa kufa mara moja, na baada ya kufu hukumu - Ebr. 9:27.

#### Mambo Yote Yatahukumiwa:

Matendo ya kila mtu - Rum. 2:6; Mt. 16:27; 25:31-46.  
Siri za watu - Rum. 2:6; 1 Kor. 4:5.  
Yote yaliyositirida na yaliyofichwa pamoja na makusudi ya moyo - Mhu. 12:14; Mk. 4:22.  
Kila neno lisilo la maana - Mt. 12:36.  
Kila kazi ndogo iliyo nzuri - Mt. 10:42.  
Mambo yatendwayo katika mwili, yawe mema au mabaya - 2 Kor. 5:10.

#### Wakristo Wanapaswa Kuwa Na Matumaini Katika Siku Ya Hukumu:

Mungu ndiye ahesabiaye haki. Ni nani atakayewashtaki? - Rum. 8:33, 34.  
Munfu hasahau kazi zao na pendo lao - Ebr. 6:10.  
Anaweza kuwalinda wasijikwae na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katiak furah kuu - Yuda 24.  
Hawapaswi kuaibika mbele zake katika kuja kwake - 1 Yoh. 2:28.  
Wanapaswa kuwa na ujasiri katika siku ya hukumu - 1 Yoh. 4:17.  
Wale wanaopenda kufunuliwa kwake wataipokea taji ya haki - 2 Tim. 4:8.

### **Husuda (Wivu)**

#### Mungu Hutafuta Kuzuia Husuda Kati Ya Watu:

Wamkataao Mungu wamejawa na husuda - Rum. 1:29.  
Wengine hupenda kubaki katika maisha ya uovu ha husuda - Tito 3:3.  
Kulikuwako husuda na fitina katiak kanisa la kule Korintho - 1 Kor. 3:3.  
Mahali penye wivu na ugomvi ndipo palipo na machafuko ya kia tendo baya - Yak. 3:14-16.  
Hatupaswi kuenenda kitika wivu - Rum. 13:13.  
Wekeni mbali uovu wote na husuda - 1 Pet. 2:1; 2 Kor. 12:20.  
Hatupaswi kuhusudiana - Gal. 5:26.  
Upendo hauhusudu - 1 Kor. 13:4.

#### Mifano Ya Husuda Au Wivu:

Kaini - Mwa. 4:4, 5; 1 Yoh. 3:12.  
Saulo - 1 Sam. 18:1-9.

Makuhani wakuu - Marko 15:10.

Masadukayo - Mdo. 5:17.

Wayahudi - Mdo. 13:45; 17:5.

Wengine wanahubiri habari za Yesu Kristo kwa ababu ya husuda na fitina - Flp. 1:15.

## **Ibada Ya Agano Jipya**

### Je! Ibada Inahitaji Nini?

Kuwapo kwa Mungu ni sehemu ya ibada ya Kikristo - Mt. 18:20; 28:20.

Ibada ya Kikristo ni pamoja na kicho na unyenyekevu mbele za Mungu (kumheshimu Mungu) - Ebr. 12:28.

Ibada ya Kikristo inapaswa kufanywa kwa utaratibu - 1 Kor. 14:40.

Ibada ya Kikristo ifanyike katika roho na kweli - Yn. 4:24.

### Jinsi Kanisa Limwabudvyo Mungu:

Maisha ya Wakristo yanapaswa kuwa ibada kwa Mungu (kitu fulani hutolewa kwa Mungu) - Rum. 21:1-2; 2 Tim. 2:15.

Wakristo hiumba nyimbo za sifa na shukrani kwa Mungu - Kol 3:16; Efe. 5:19.

Wakristo humwomba Mungu - Mt. 21:22. (angalika sehemu ya Maombi).

Kila Jumapili (siku ya kwanza ya juma) Wakristo hutoa changizo (kulingana na kufanikiwa kwa kila mmoja) ili kuwasaidia wenzao - 1 Kor. 16:1, 2; Rum. 12:8; Mdo. 20:35; 2 Kor. 9:6-8.

Kila Jumapili Wakristo wote hushiriki Meza ya Bwana (angalia sehemu ya Chakula cha Bwana) - Mdo. 20:7; 1 Kor. 11:23-29; Yn. 6:50-58; Mt. 26:26-29.

Wakristo humwabudu Mungu kwa kujifunza neno lake - Mdo. 17:10, 11, 2 Tim. 2:15.

### Ibada ya Jumapili:

Tusiache kukusanyika kwa ibada - Ebr. 10:25.

Katika ibada yetu ya Jumapili tunapaswa kumwabudu Mungu ifuatavyo:

Tushiriki chakula cha Bwana - Mdo. 20:7; 1 Kor. 11:23-29.

Tujifunze neno la Mungu - Mdo. 20:7.

Tuime - Efe. 5:19, 20.

Tuombe - Mdo. 2:42.

Tutoe - 1 Kor. 16:2; 2 Kor. 9:6, 7.

Wanawake hawapaswi kuhubiri au kuchukua mamlake juu ya wanaume ibadani - 1 Kor. 14:34; Efe. 5:22, 23; 1 Tim. 2:12-25.

Tukikosa hiki “chakula cha kiroho” tutakuwa dhaifu - Ebr. 3:12, 13.

## **Imani**

### Tunapaswa Kuamini Nini?

Mungu - Marko 11:22; Ebr. 11:6.  
Kristo - Yn. 14:1; 8:24.  
Maandiko ya Musa - Yn. 5:46, 47; Mdo. 24:14.  
Maandiko ya manabii - Mdo. 26:22, 23, 27; 2 Pet. 1:20, 21.  
Injili - Mk. 1:15; 16:15, 16.  
Ahadi za Mungu - Rum. 4:20, 21; Ebr. 11:13.

#### Tabia za Imani:

Ni yenye thamani - 2 Pet. 1:1.  
Ni takatifu sana - Yuda 20.  
Inatenda kazi - 1 The. 1:3; Gal. 5:6.  
Huambatana na toba - Marko 1:15.  
Huja kutokana na neno la Mungu - Rum. 10:17; Yn. 20:30, 31.  
Kristo ndiye mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani - Ebr. 12:2.  
Huwa imekufa isipokuwa na matendo - Yak. 2:19-26.  
Huleta wokovu kwa watu - Mdo. 16:31; Efe. 2:8.  
Huzaa amani, furaha na tumaini - Rum. 5:1; 15:13; 1 Pet. 1:8.  
Huzuia majivuno (kiburi) - Rum. 3:27; 4:2; Efe. 2:9.  
Hujaribiwa daima - Ebr. 11:17; Yak. 1:3; 1 Pet. 1:7.  
Hutumika kama ngao ya kuzimishia mishale yenye maoto ya Shetani - Efe. 6:16.  
Huushinda ulimwengu - 1 Yoh. 5:4.

#### Imani Hutuletea Baraka Za Mungu:

Kuhesabiwa haki - Rum. 3:28; Gal. 2:16; Rum. 5:1.  
Wokovu - Efe. 2:8; Mdo. 16:31.  
Utakatifu - Mdo. 15:9; 26:18.  
Ondoleo la dhambi - Mdo. 10:43.  
Kumkaribia Mungu - Rum. 5:1, 2; Efe. 3:12.  
Roho Mtakatifu kama kipawa - Gal. 3:14; Efe. 1:13.  
Amani - Rum. 5:1  
Furaha - Rum. 15:13.  
Tumaini - 1 Pet. 1:8.  
Kulindwa na nguvu za Mungu - 1 Pet. 1:5.  
Ushindi - 1 Yoh. 5:4.  
Uzima wa milele - Yn 3:16; 1 Yoh. 5:13.  
Ahadi za Mungu - Ebr. 6:12; Gal. 3:22.

#### Kwa Imani Watu Wa Mungu:

Huishi - Gal. 2:20.  
Huendelea kusimama imara - Rum. 11:20; 2 Kor. 1:24.

Huenenda - Rum. 4:12; 2 Kor. 5:7.  
Hushuhudiwa - Ebr. 11:2.  
Hutiwa nguvu - Mdo. 16:5.  
Humpinga Shetani - 1 Pet. 5:9.  
Huizima mishale ya Shetani - Efe. 6:16.  
Huushinda ulimwengu - 1 Yoh. 5:4.  
Hufa - Ebr. 11:13.

#### Kwa Hivyo Wakristo Wanapaswa:

Kujawa na imani - Mdo. 6:5; 11:24.  
Kuwa na imani isiyo na unafiki - 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 1:5.  
Kuwa na wingi wa imani - 2 Kor. 8:7.  
Kukaa katika imani - Mdo. 14:22; Kol 1:23.  
Kuwa na nguvi katika imani - Rum. 4:20.  
Kusimama imaria katika imani - 1 Kor. 16:13; Kol. 1:23.  
Kiwa na imani na dhamiri njema - 1 Tim. 1:19.  
Kuomba waongezewe imani - Luka 17:5.  
Kumkaribia Mungu Kwa utimilifu wa imani - Ebr. 10:22.  
Kuithibitisha imani yao kwa matendo - Yak. 2:19-26.  
Kujijaribu wenyewe kwamba wamekuwa katika imani - 2 Kor. 13:5.  
Kumkaribisha yeye aliye na imani dhaifu - Rum. 14:1.  
Kuichukuwa ngao ya imani - Efe. 6:16.  
Kupiga vita vizuri vya imani - 1 Tim. 6:12.  
Kuilinda imani - 2 Tim. 4:7.  
Kuomba kwa imani - Yak. 1:6.  
Kutia wema katika imani yao - 2 Pet. 1:5.  
Kuishindania imani - Yuda 3.

#### Mifano Ya Imani:

Abeli - Ebr. 11:4.  
Henoko - Ebr. 11:5.  
Nuhu - Ebr. 11:7.  
Ibrahimi - Rum. 4; Ebr. 11:8-10; 17-19.  
Musa - Ebr. 11:24-28.  
Kalebu - hesabu 13:30  
Rahabu - Ebr. 11:31; Yak. 2:25.  
Shadrak, Meshaka na Abedinego - Dan. 3:13-30.  
Danieli - Dan. 6.  
Petro - Mt. 16:16; Yn. 6:68, 69.  
Martha - Yn. 11:27.  
Stefano - Mdo. 6-5.

Barnaba - Mdo. 11:24.  
Paulo - 2 Tim. 1:12, 4:7.

### **Je, Tunaokolewa na Imani Tu?**

#### Wengi Wanafundisha Tukiamini Tu Tutaokoka, Biblia Yasemaje?

Imani bila matendo imekufa - Yak. 2:17.  
Tunahesabiwa haki kupitia matendo - Yak. 2:24.

#### Kama Imani Peke Yake Inaokoa Kwa Nini.....:

Mashetani wanatetemeka - Yak. 2:19?  
Tuwe na upendo - 1 Kor. 13:2?  
Biblia inasema, "Siyo kwa imani tu?" - Yak. 2:24.  
Tunatakiwa kubatizwa - Mdo. 2:38?  
Tuongeze kwa imani zetu - 2 Pet. 1:5?

### **Injili Ya Kristo**

#### Injili Imeelezwa Katika Biblia Kama:

Uwakili wa neema ya Mungu - Efe. 3:2  
Injili ya amani - Efe. 6:15.  
Injili ya Mungu - Rum. 1:1; 1 The. 2:8.  
Injili ya Mwana wake - Rum. 1:9.  
Injili ya Kristo - 2 Kor 2:12; 1 The. 3:2.  
Injili ya neema ya Mungu - Mdo. 20:24.  
Injili ya ufalme - Mt. 24:14.  
Injili ya wokovu wenu - Efe. 1:13.  
Injili ya utukufu wa Kristo - 2 Kor. 4:4  
Siri ya Kristo - Efe. 3:4.  
Neno la Mungu - 1 The. 2:13.  
Neno la neema yake - Mdo. 14:3; 20:32.  
Neno la wokovu - Mdo. 13:26.  
Neno la upatanisho - 2 Kor. 5:19.  
Neno la kweli - Efe. 1:13.  
Neno la imani - Rum. 10:8.  
Neno la uzima - Flp. 2:16.  
Huduma ya Roho - 2 Kor. 3:8  
Mafundisho yapatanaya na utauwa - 1 Tim. 6:3.  
Injili ya milele - Ufu. 14:6.

### Injili Ni Habari Njema Zihusuzo Yesu Kristo Na Wokovu Uliyo Katika Yeye:

Mwokozi alizaliwa kwa ajili ya watu wote - Luka 2:10, 11.  
Alikufu kwa ajili ya wenye dhambi na akafufuka kutoka kwa wafu - Rum. 4:25; 1 Kor. 15:1-4.  
Mungu aliahidi kuleta Injili Hapo zamani katika maandiko matakatifu ya manabii - Rum. 1:1, 2.  
Uzima na kutokuharibika hudhihirishwa katika Injili - 2 Tim. 1:10.  
Haikutokana na mwanadamu bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo - Gal. 1:11, 12.  
Ni uwez wa Mungu uuletao wokovu - Rum. 1:16; Marko 16:15, 16.

### Injili Ya Kristo Iliwaokoa:

Wale waliomsulubisha - Mdo. 2:22-41.  
Wachawi - Mdo. 8:5-13; 19:18, 19.  
Watu was dini - Mdo. 8:26-40; 10:1-11, 18.  
Wale walioliudhi kanisa - Mdo. 9:1-19; 22:1-16.  
Watu ambao hawakuwa na dini (wakafiri) - Mdo. 16:30-34.  
Waabudu sanamu - 1 The. 1:8-10.  
Wenye dhambi wa kila aina - 1 Kor. 6:9-11.

### Wengine Hawaitii Injili:

Ilikataliwa na Wayahudi wengi - Mdo. 13:46; 1 The. 2:15, 16.  
Wengine huigeuza Injili na kuiharibu - Gal. 1: 6, 7.  
Injili imesitirika kwa hao wanaopotea, ambao wamepofushwa fikira zao na Shetani - 2 Kor. 4:3, 4.  
Wale wanaohubiri Injili Kwa Kuigeuza wanapaswa kulaaniwa - Gal. 1:8, 9.  
Wale wasioitii Injili wataadhibiwa - Marko 16:16; 2 The. 1:8, 9.  
Kwa tabia zetu mbovu, tunaweza tukaizuia Injili - 1 Kor. 9:12.

### Jukumu Letu Katika Injili:

Hatupaswi kuionea haya - Rum. 1:16.  
Mwenendo wetu na uwe kama inavyoipasa Injili - Flp. 1:27.  
Mwenendo wetu na uwe sawasawa na ile kweli ya Injili - Gal. 2:14.  
Hatupaswi kugeuzwa na kulizcha tumaini la Injili - Kol. 1:23.  
Tunapaswa kuvumilia mabay akwa ajili ya Injili - 2 Tim. 1:8, 3:12.  
Tumewiwa nafsini mwetu kwa kuihubiri Injili - 1 Kor. 9:16; Rum. 1:14.  
Tunapaswa kuwa wahudumu wa Injili - Rum. 1:1, 15:16; Flp. 2:22; 4:3.  
Yeyote atakayeyapoteza maisha yake kwa sababu ya Injili atayaokoa - Marko 8:35; 10:29.

### **Ishara (Miujiza) Ya Yesu**

### Ishara (Miujiza) Ya Kuwaponya Wale Waliokuwa Wagonjwa:

Alimponya mtoto wa diwani - Yn. 4:46-54.  
Aliweza kuwatoa pepo - Mk. 1:23-27; Mt. 8:28-32; 9:32-33.  
Alimponya mama mkwe wa Petro - Mt. 8:14, 15.  
Aliwaponya wenye ukoma - Mt. 8:1-4; Lk. 17:12-14.  
Aliwaponya wenye kupooze - Mk. 2:3-12.  
Aliwaponya wenye viungo vya mwili vilivyopooza - Mt. 12:9-13; Yn. 5:2-9.  
Aliwaponya wenye macho yaliopofuka wakapata kuona - Mt. 9:27-30; Mk. 8:22-25; Yn. 9:1-7.

#### Ishara (Miujiiza) Nyingine Za Namna Mbalimbali:

Alibadilisha maji yakawa divai - Yn. 2:1-11.  
Aliwasaidia wavuvi wa samaki kuvua samaki wengi - Lk. 5:4-7; Yn. 21:5, 6.  
Aliwalisha chakula makutano mengi - Mt. 14:15-21; 15:32-38.  
Alitembea juu ya bahari - Mk. 6:45-52; Yn. 6:16-21.  
Alizikemea pepo za bahari kukawa shwari - Mt. 8:23-27; Lk. 8:22-25.  
Aliulaani mtini - Mk. 11:12-14; Mt. 21:18-22.  
Aliwafufua wafu - Lk. 7:11-15; Mt. 9:18-26; Yn. 11:11-44.  
Aliudhihirisha utukufu wake alipogeuka sura yake - Lk. 9:28-32; Mt. 17:1-8; 2 Pet. 1:16.  
Alifufuka kutoka kwa wafu - Lk. 24:6; Yn. 10:18.  
Aliwatokea wanafunzi wake, wakati milango ilikuwa imefungwa - Yn. 20:19.  
Alipaa mbinguni - Mdo. 1:9-11.

### **Kanisa La Yesu Kristo**

#### Matumizi Ya Neno “Kanisa” Katika Agano Jipya:

Neno “kanisa” maana yake ni “kuitwa” watu wakusanyike. Si kampuni au ushirika wa watu wakutanao kwa kupeana mawazo yao tu, bali ni watu wakusanyikao kwa kuisikiliza sauti ya Mungu.

Limetumiwa katika maana tatu katika Agano Jipya:

Kanisa zima - Mt. 16:18; Efe. 1:22, 23; Kol. 1:18.

Kundi la mahali fulani - Rum. 16:1; Gal. 1:2; 1 Kor. 1:2, 16:19.

Mkusanyiko wa Wakristo - 1 Kor. 11:18; 14:19, 23.

Halijatumiwa katika Agano Jipya kama dhehebu; kundi kubwa kuliko la mahali fulani lakini dogo kuliko kanisa zima.

Neno “kanisa” maana yake si “jengo” katika Agano Jipya.

Kuna “mwili mmoja” - lile kanisa kitaka Agano Jipya - Efe. 1:22-23; 2:16; 4:4; Rum. 12:4-5.

Wale ambao wamekwisha kuokolewa huzidishwa kanisani - Mdo. 2:47.

#### Utukufu Na Ukuu Wa Kanisa:

Lilikuwa katika kusudi la milele la Mungu - Efe. 3:8-11.

Ni ukamilifu wa Kristo - Efe. 1:22-23.

Ni mwili uliopatanishwa na Mungu - Efe. 2:11-18.

Ni maskani ya Mungu Katika Roho - Efe. 2:18-22.  
Ni hekalu takatifu la Mungu - 1 Kor. 3:9, 16, 17; 2 Kor. 6:14-16.  
Ni Nyumba ya Mungu - Efe. 2:19; 5:1-2; 1 Tim. 3:15.  
Ni bibi-arusi wa Kristo - Efe. 5:22-23.  
Ni jeshi la vita la Mungu - Efe. 6:10-17.  
Litakabidhiwa kwa Kristo katika utukufu - Efe. 5:27; 2 Kor. 11:2.  
Litaokolewa na Kristo - Efe. 5:23.

#### Kanisa Ni Mali Ya Kristo.

Yeye ndiye aliyelijenga - Mt. 16:18.  
Yeye ni msingi wa kanisa - 1 Kor. 3:11; Efe. 2:20.  
Ni mwili wake - Efe. 1:23; Kol. 1:24.  
Yeye ni kichwa cha kanisa - Efe. 1:22; 5:23.  
Alilinunua kwa damu yake - Mdo. 20:28.  
Kanisa humtii Kristo - Efe. 5:24; Rum 7:4.  
Kristo hulitakasa na kulisafisha - Efe. 5:26, 27.  
Huwazidisha wanaokolewa katika kanisa - Mdo. 2:41, 47; 5:14; 11:24.  
Kanisa ni ukamilifu wa Kristo - Efe. 1:23.  
Yeye ndiye Mwokozi wa kanisa - Efe. 5:23.

#### Majina ya Kanisa:

Hekalu la Mungu (Roho wa Mungu huishi ndani ya Wakristo) - 1 Pet. 2:5; Efe. 2:20-22.  
Nyumba ya Mungu - 1 Tim. 3:15.  
Mwili wa Kristo - Kol. 1:18; Efe. 5:23, 24; 1 Kor. 12:12, 13.  
Bibi arusi wa Kristo - 2 Kor. 11:2; Efe. 5:25-27; Ufu 21:1, 2.  
Ufalme wa Mwana (Yesu ni mfalme wa Wakristo) - Kol. 1:13.  
Kanisa la Mungu (Yesu na Mungu wana Umoja) - 1 Kor. 1:2; 3:23; Yn. 17:21; Mdo. 20:28.  
Kanisa la wazaliwa wa Kwanza - Ebr. 12:23.  
Makanisa ya Kristo - Rum. 16:16; Ufu. 1:4.

#### Majina ya Washiriki wa Kanisa:

Wanafunzi - Mdo. 6:1.  
Wakristo - Mdo. 11:26; 26:28, 29; 1 Pet. 4:16.  
Wanaoamini - Mod. 5:14.  
Wana wa Mungu - 1 Yoh. 3:1, 2.  
Viungo vya mwili wa Kristo - 1 Kor. 12:12, 13, 27.  
Watakatifu - Flp. 1:1; Rum. 1:8; 1 Kor. 6:11.  
Makuhani au ukuhani mtakatifu - 1 Pet. 2:9; Ufu. 1:6.

**Je! Kanisa la Yesu ni Sawa na Madhehebu?**



### Kanisa La Yesu Linafuata Mamlaka Yake:

Ampewa mamlaka yote hapa ulimwenguni na mbinguni - Mat. 28:18-19.  
Tunadumu katika mafundisho yake - 2 Yoh. 9.  
Malaika na enzi na nguvu ziko chini yake - 1 Pet. 3:22.

### Yesu Hataki Magawanyiko Katika Kanisa:

Tusiwe na faraka - 1 Kor. 1:10.  
Madhehebu sio matawi ya Kristo - Yn. 15:6. **Yesu aliwaita mwanadamu mtawi, hakuyaita madhehebu matawi.**  
Yesu aliomba tuwe na umoja - Yoh. 17:11.  
Kuna imani moja - Efe. 4:5.  
Kuna mwili moja - Efe. 4:4.

### Kanisa Lilianzishwa Na Yesu Madhehebu Yameanzishwa Na Wanadamu:

Tukifuata mafundisho ya wanadamu tunaabudu ibada zetu bure - Mat. 15:9.  
Kila pando asilolipanda Baba litang'olewa - Mat. 15:13.  
Kipofu akimwongoza kipofu mwenzake shimoni - Mat. 15:14.

## **Kanisa ni Mali ya Nani?**

### Mali Ya Yesu Kristo:

Yesu alisema atalijenga kanisa lake - Mt. 16:18.  
Kanisa lilikwisha jengwa - Efe. 2:10.  
Msingi ni Yesu Kristo - 1 Kor. 3:11.  
Jiwe la Pembeni ni Yesu - Efe. 2:10.  
Jiwe lililojaribiwa - Isa. 28:16.  
Jiwe lililokataliwa na watu - Mat. 21:42.  
Alikuwa kichwa baada ya ufufuo yake - Mdo. 4:10-11.  
Alilinunua na damu yake - Mdo. 20:28.  
Kanisa la Kristo - Rum. 16:16.

## **Kanisa si Jengo.**

### Neno "Kanisa" Katika Agano Jipya Haina Maana "Jengo":

### Hali Ya Kawaida:

Yesu alisema juu ya mwamba huu nitalinjenga kanisa - Mat. 16:18.

Yesu ni kichwa cha mwili yaani kanisa - Kol. 1:18.  
Alijitoa mwenyewe ili awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa - Efe. 1:22.  
Yesu alilipenda kanisa - Efe. 5:25.

#### Kanisa Mahali Pamoja:

Kanisa kule Korinto - 1 Kor. 1:2.  
Kanisa katika nyumba yao - 1 Kor. 16:19. (Nyumba sio kanisa.)  
Katika kanisa ndani ya nyumba - Filimon 2.

#### Kanisa:

Paulo aliliandikia kanisa kule Korinto - 1 Kor. 1:1-2.  
Kanisa linahitaji chakula la kiroho - Mdo. 20:28.  
Kwa mkusanyiko na kanisa - Ebr. 12:23.  
Hofu iliingia katika kanisa juu ya Kanisa - Mdo. 5:11.  
Kanisa lilikubali na lilichagua - Mdo. 15:22.  
Sauli alikuwa na haribu kanisa - Mdo. 8:3-4.

Kanisa ni mali ya Yesu Kristo na kama unataka kuwa ndani ya kanisa unahitaji kubatizwa kwa ajili ya dhambi zako na Bwana atakuzidisha katika kanisa lake - Mdo. 2:37-47.

### **Kazi (Matendo)**

#### Kazi Za Mungu Na Kristo:

Mungu anastahili heshima kwa sababu ya kazi zake - Zab. 19:1-3; 147; 148; Ufu. 4:8-11.  
Yesu alikuja ili aweze kuzitimiza kazi za Mungu - Yn. 4:34; 5:36; 10:36, 37.  
Ishara zake au miujiza zimeitwa kazi - Yn. 4:34; 5:36.  
Alimaliza kazi yake duniani, lakini bado anaendelea kufanya kazi kama ifuatayo:  
    Huendelea kulizidisha kanisa lake kwa wale wanaokolewa - Mdo. 2:47; 5:14.  
    Anaendelea kukaa pamoja na watumishi wake - Mt. 28:20; Ebr. 13:5, 6.  
    Wakati wa kuja kwake atauhukumu ulimwengu - Mdo. 17:31; Mt. 16:27; 25:31-46.  
    Huwaombea watakatifu - Rum. 8:34; Ebr. 7:25; 1 Yoh. 2:1, 2.  
    Mungu hufanya kazi kwa njia ya Wakristo - Efe. 3:20; Flp. 1:6; 2:13; Kol. 1:29; Ebr. 13:21.

#### Kazi Za Kimwili Ziisaidiazo Jamaa Na Wengine:

Mungu alimpa mwanadamu kazi katika Bustani ya Edeni - Mwa. 2:15.  
Kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu kazi yake iliongezeka - Mwa. 3:17-19.  
Yesu aliwesa kufanya kazi ya useremala - Mk. 6:3.  
Paulo alitoa mfano kwa kufanya kazi kawa mikono yake - Mdo. 18:3; 20:34, 35.

Wakristo wanapaswa kufanya kazi kawa mikono yao ili kwamba waweze kujisaidia wenyewe na kuwasaidia wenye kuhitaji - Lk. 10:7; Efe. 4:28; 1 The. 4:11; 1 Tim. 5:8, 13; 2 The. 3:10.

#### Tabia Za Matendo Mema:

Hufanywa kwa njia ya Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu - Flp. 1:11.

Hufanywa katika jina la Bwana Yesu - Kol. 3:17.

Maandiko hutukamilisha kwa kila tendo jema - 2 Tim. 3:16, 17.

Mungu hutukuzwa kwa matendo mema ya Wakristo - mt. 5:16; Yn. 15:8; 1 Pet. 2:12.

Imani isipokuwa na matendo imekufa - Yak. 2:17-26.

Matendo yatokanayo na imani humhesabia mtu haki - Yak. 2:19-26.

Watu hawahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, au kwa haki yao wenyewe - Gal. 2:16, 20; Efe. 2:8, 9; 2 Tim. 1:9.

Matendo mema hufuatana nao wafao katika Bwana - Ufu. 14:13.

Waovu ni machukizo kwa maana hawafai kwa kila tendo jema - Tito 1:16.

#### Matendo Maovu:

Matendo ya ulimwengu huu wa sasa - Yn. 3:19; 7:7.

Matendo mabaya ya watu wasio na Kristo - Kol. 1:21; Efe. 2:1, 2; 4:17-19.

Matendo maovu - Efe. 9:14.

Matendo yasiyo na sheria - 2 Pet. 2:8.

Kazi zote za upotevu zitendowazo bila kumcha Mungu - Yuda 15.

Matendo yasiyozaa ya giza - Efe. 5:11; Rum. 13:12.

Matendo ya Ibilisi - 1 Yoh. 3:8; Yn. 8:41-44.

#### Watoto Wa Mungu:

Wameumbwa katika Kristo ili watende matendo mema - Efe. 2:10.

Mungu aliyatengeneza ili waenende nayo - Efe. 2:10.

Huvaa matendo mema - Kol. 3:12-14.

Wamejawa na matendo mema - Mdo. 9:36.

Wana juhudi katika kutenda mema - Tito 2:14; 3:8, 14.

Wako tayaari kwa kila kazi njema - 2 Tim. 2:21; 3:17; Tito 3:1.

Huzidi katika kutenda mema - 1 Tim. 6:18; 1 Kor. 15:58; 2 Kor. 9:8.

Wameimarishwa katika kutenda mema - 2 The. 2:17.

Huhimiza na katika kazi nzuri - Ebr. 10:24.

Ni vielelezo vya matendo mema - Tito 2:7.

Hawatendi mema ili waonekane na watu - Mt. 6:1-4.

Watahukumiwa kulingana na matendo yao - 2 Kor. 5:10; Mt. 25:31-46; Ufu. 2:23; 22:12.

#### Kwa Matendo Mema, Wakristo Huyapamba Mafundisha Ya Mungu:

Wanapaswa kutenda mema mbele za watu wote - Rum. 12:17; 2 Kor. 8:21.  
Maaskofu (waangalizi) wa kanisa wanapaswa kushuhudiwa mema na watu walio nje - 1 Tim. 3:7.  
Wajane wanapaswa kuwa na sifa njema kwa matendo mema - 1 Tim. 5:10.  
Wafanya kazi wanapaswa kuyapamba mafundisho ya Mungu mbele za bwana zao - Tito 2:10.  
Mwenendo wa Wakristo unapaswa kuwa mzuri kati ya Mataifa - 1 Pet. 2:12.  
Watu wengine humtukuza Mungu kwa sababu ya matendo mema ya Wakristo - Mt. 5:16.

### **Kiasi**

#### Watu Wa Mungu Wanapaswa Kuwa Na Kiasi:

Kulinda moyo kwa juhudi yote - Mit. 4:23.  
Mtu aitawalaye roho yake ni bora kuliko yeye atekaye mji - Mit. 16:32.  
Paulo alihubiri habari za kuwa na kiasi kwa Feliki - Mdo. 24:25.  
Wakristo wanapaswa kutia kiasi katika maarifa yao - 2 Pet. 1:16.  
Mtu atafutaye kushinda anapaswa kuwa na kiasi - 1 Kor. 9:25.

#### Jinsi Ya Kuwa Na Kiasi:

Kumbuka mifano ya watu watakatifu:

Yusufu - Mw. 39:7-10.

Vashti - Esta 1:9-12.

Danieli - Dan. 1:8; 6:1-28.

Yesu - Mt. 4:1-11.

Paulo - 1 Kor. 9:27; Flp. 3:14, 15.

Kuacha kushirikiana na waovu - Mit. 4:14-16; 1 Kor. 5:6; 15:22; 1 Tim. 5:22; 2 Tim. 2:22.

Kuenenda kulingana na kusudi la moyo - Dan. 1:8; Mdo. 11:23.

Kujifunza manyumbani mwetu - 2 Tim. 1:5; 3:15-17.

Kuomba bila kukoma - 1 Th. 5:17; Kol. 4:2; Mt. 26:41.

Kuzitumainia ahadi za Mungu - Ebr. 13:5, 6; 4:14-16; 1 Yoh. 2:1; Rum. 8:26-39; 2 Tim. 1:12; Yn. 10:27-29; Ufu. 17:14.

Kuikumbuka bei kubwa ya dhambi - Ebr. 12:16, 17; 3:13; 11:24-26; Mt. 27:3-5; Rum. 6:23; Yak. 1:14-16.

### **Kiburi (Kujisifu, Kujivuna)**

#### Tabia Za Kiburi:

Ni nuru ya waovu - Mit. 21:4.

Ni kama mkufu shingoni mwa waovu - Zab. 73:6.

Hutoka moyoni - Mk. 7:22, 23.

Hudanganya watu - Obadia 2.

Kiburi huja na aibu - Mit. 11:2.

Huufanya moyo kuwa mgumu - Dan. 5:20.

Humtia mtu unajisi - Mk. 7:22, 23.

Kinachukiwa na Mungu - Mit. 6:16-17.  
Ni chukizo kwa Mungu - Mit. 16:5.  
Hutangulia uharibifu (uangamivu) - Mit. 16:18; 18:12.

Kiburi Hutokana Na:

Kujaribu kujihesabia haki - Lk. 18:11, 12.  
Ujuzi usio na upendo - 1 Kor. 8:1.  
Kupata mamlaka bila kuwa na ujuzi wa muda mrefu - 1 Tim. 3:6.  
Mahali penye uwezo - Law. 26:19.  
Utajiri - 2 Fal. 20:13.

Mifano Ya Kiburi (Majivuno):

Shetani - 1 Tim. 3:6.  
Nebukadreza - Dan. 4:30; 5:20.  
Belshaza - Dan. 5:22, 23.  
Baadhi ya waandishi - Mk. 12:38, 39.  
Herode - Mdo. 12:21-23.  
Walaodikia - Ufu. 3:17.  
Diotrefe - 2 Yoh. 9.

Adhabu Ya Wenye Kiburi:

Wao hukumbana na msiba (Ole) - Isa. 28:1.  
Watadhiliwa - Zab. 18:27.  
Watahushwa - Mit. 29:23; Mt. 23:12; Lk. 14:11.  
Wataangushwa chini - Isa. 13:11.  
Mungu huwapinga - Yak. 4:6.  
Wataangamizwa - Mit. 16:18; 18:12.

Wale Walio Wana Wa Mungu:

Hawapaswi kuwa wenye kiburi na majivuno - Isa. 2:12; Gal. 5:26.  
Hawapaswi kutenda neno lolote kwa majivuno - Flp. 2:3.  
Hawapaswi kuwaelekea wenye kiburi - Zab. 40:4.  
Wanapaswa kukubali kushughulishwa na mambo manyonge - Rum. 12:16.  
Wanapaswakukumbuka kwamba wameokolewa kwa neema, wala si kwa wema wao - Efe. 2: 8, 9.  
Hawana sababu ya kujisifu - 1 Kor. 1:29, 31; Rum. 3:27.  
Wana upendo usio na majivuno - 1 Kor. 13:4.

**Kipawa Cha Roho Mtakatifu**

Roho Mtakatifu Hutolewa Kwa Waliokombolewa:

Roho Mtakatifu hutumwa na kuingia mioyoni mwetu wakati tumesamehewa dhambi na Mungu - Mdo. 2:38; 5:32; Gal. 4:6; Rum. 5:5.

Roho Mtakatifu huishi ndani ya Wakristo ambao ndiyo hekalu la Mungu - 1 Kor. 3:16; 6:19; Efe. 2:22. Tafadhali Kumbuka - Yn. 4:13-14; 7:37-39; 2 Kor. 13:14.

Roho Mtakatifu Ni Ushuhuda Na Mdhamini Wa Ukombozi Wetu:

Dhamana ya kuitwa wana na ushuhuda wa msamaha:

Gal. 4:6; Rum. 8:15, 16; Tazama Yn. 14:18.

2 Kor. 1:22; 5:5; 1 Yoh. 3:24; 4:13.

Efe. 1:14, 4:30.

Huduma ya Roho ndani yetu:

Roho hutusaidia udhaifu wetu na kutuombea - Rum. 8:26; Tafadhali kumbuka Efe. 6:18; Yuda 20.

Twaishi kwa Roho ambaye hutuongoza katika mwenendo wetu - Gal. 5:25.

Huzaa ndani yetu “tunda la Roho” - Gal. 5:22, 23.

Hutusaidia kuyafisha matendo ya mwili - Rum. 8:12, 13.

Huzibadilisha tabia zetu. Hututakasa wakati tumeokolewa - 2 The. 2:13; 1 Pet. 1:2.

Huendelea kututenga na maovu na kutubadilisha kidogo kidogo katika maisha yetu yote - 2 Kor. 3:18; Rum. 12:2; Mt. 17:2; Kol. 3:10.

Hutupa furaha na amani - Mdo. 13:52; Rum. 14:17.

Twazidi kuwa na tumaini katika nguvu za Roho Mtakatifu - Rum. 15:13.

Hutusaidia kuilinda ile kweli tuliyopewa - 2 Tim. 1:14.

Roho Mtakatifu ataihuisha miili yetu iliyo katika hali ya kufa - Rum. 8:11.

Roho Mtakatifu katika Waraka kwa Waefeso:

Hututia muhuri sisi tuliookoka - Efe. 1:13.

Tumepata kumkaribia Mungu Baba Kwa njiaya Roho Mtakatifu - Efe. 2:18.

Hutujenga pamoja tuwe maskani ya Mungu - Efe. 2:22.

Aliyafunua mapenzi ya Mungu kupitia kwa mitume na manabii - Efe. 3:5.

Huufanya imara kwa nguvu utu wetu wa ndani - Efe. 3:16.

Yeye ndiye kifungo cha umoja wa Ukristo - Efe. 4:3.

Hujaa ndani yetu ili tusifanye dhambi na hutupa furaha - Efe. 5:18, 19.

Hutoa upanga wake ambao ni neno la Mungu - Efe. 6:17.

Huyasaidia maombi yetu - Efe. 6:18.

Lakini Roho Mtakatifu Hawezi Kuwasaidia Wale Wanaozikata Huduma Zake:

Wakristo wanaagizwa kwamba:

Wanapaswa kujazwa Roho - Efe. 5:18; Kol. 3:16; Luka 11:13.

Wanapaswa kuenenda kwa Roho - Gal. 5:16-18.

Wanapaswa kupanda kwa Roho - Gal. 6:7-9.

Wanapaswa kuishi kwa Roho - Rum. 8:1-13.

Wanapaswa kuongozwa na Roho - Rum. 8:14; Angalia Kum. 8:14, 15.

Wanapaswa kuzaa tunda la Roho - Gal. 5:22, 23.

Wakristo wameonywa kwamba:

Wasimhuzunisha Roho Mtakatifu wa Mungu - Efe. 4:20; Tafadhali angalia aya za 25-32, mahali tunapoweza kuona jinsi tunavyoweza kumhuzunisha Roho.

Hawapaswi kumhuzimisha Roho - 1 The. 5:19; soma pia 1 The. 4:4-8; 5:6-8; 5:14-22.

Hawapaswi kumfanyia jeuri Roho wa neema - Ebr. 10:26-29; Tafadhali kumbuka Ebr. 4:4-6; Luka 11:24-26; 2 Pet. 2:20-22.

Kwa sababu ya “udanganyifu wa dhambi” tunaoweza kuufanya kidogo kidogo bila kujua, hatuwezi kujua kwamba Mungu ametuacha - Ebr. 3:12, 13; Waamuzi 16:20.

### **Kitabu Cha Uzima**

Majina huandikwa mbinguni - Luka 10:20.

Majina yao yamo katika kitabu cha uzima - Flp. 4:3.

Wale walioandikwa katika kutabu cha Mwana -Kondoo ni wale watakaoingia mbinguni - Ufu. 21:27.

Wale ambao hawakuandikwa ndani ya hicho kitabu watatupwa katika ziwa la moto - Ufu. 20:12, 15.

### **Kristo Amegawanyika?**

#### Mwili Moja:

Watu ni wengi ndani ya mwili moja - Rum. 12:4-5.

Tunatakiwa kuwa mwili moja kama Kristo - 1 Kor. 12:12.

Alitupatanisha katika mwili moja - Efe. 2:16.

Tuliitwa katika mwili moja - Kol. 3:15.

Kuna mwili moja - Efe. 4:4.

#### Mwili Moja Ni Nini?

Mwili moja ni Kanisa - Kol. 1:18; 1:24.

Kichwa kimoja juu ya Kanisa ambalo ni mwili - Efe. 1:22-23.

#### Yesu Ni Kichwa Cha Mwili Yaani Kanisa:

Kichwa cha mwili - Kol. 1:18.

Kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa - Efe. 1:22.

Yesu ni kichwa cha kanisa kama vile mume ni kichwa cha mke - Efe. 5:23.

#### Ni Lazima Tuwe Katika Mwili Moja?

Yesu ni mwokozi wa mwili - Efe. 5:23.

Yesu alikufa kwa ajili ya kanisa (mwili) - Efe. 5:25.  
Alinunua kanisa na damu yake - Mdo. 20:28.  
Alitupatanisha sisi na Baba katika mwili moja - Efe. 2:16.  
Bwana akatuzidisha katika kanisa - Mdo. 2:47.  
Tusiwe na faraka 1 Kor. 1:10-13.

## **Kuabudu Sanamu**

### Kuabudu Sanamu Ni:

Kuchonga sanamu au kufananisha - Kut. 20:4; Kum. 5:8.  
Kuisujudia miungu ya kigeni - Kum. 30:17; Zab. 81:9.  
Kuitafuta miungu mingine na kuitumikia - Kum. 8:19; Kut. 23:13.  
Kunena kwa majina ya miungu mingine - Kum. 8:20.  
Kuicha miungu mingine na kuitolea sadaka - 2 Fa. 17:35.  
Kumwabudu Mungu pamoja na sanamu za kuyeyushwa - Kut. 32:4-6; Zab. 106:19, 20.  
Kuabudu malaika - Kol. 2:18.  
Kuabudu jua, mwezi na nyota - Kum. 4:190; 17:3.  
Kuabudu pepo wabaya - Ufu. 9:20.  
Kuzila dhabihu za wafu - Zab. 106:28.  
Kuvitia vinyago (sanamu) moyoni - Eze. 14:3, 4.  
Tamaa mbaya ni ibada ya sanamu - Efe. 5:5; Kol. 3:5.  
Mungu wao ni tumbo - Flp. 3:19.  
Kuibadili kweli ya Mungu kuwa uongo - Rum. 1:25.  
Ukaidi ni kama ukafiri na vinyago - 1 Sam. 15:23.  
Kutoa dhabihu kwa wafu (mababu) - 1 Pet. 4:3; Isa. 8:19.

### Waisraeli Walikatazwa Wasiabudu Sanamu:

1. Kut. 20:4; 34:17                      2. Law. 19:4; 26:1  
3. 2 Fal. 15:8; 21:11                    4. Eze. 14:6.

### Kuabudu Sanamu Ni Jambo La Upumbavu Na La Uovu Pia:

Kukiabudu kiumbe badala ya Muumba - Rum. 1:19-25.  
Mataifa wamechukuliwa kwa kufuata sanamu zisizonena - 1 Kor. 12:2.  
Sanamu haziwezi kuwa na uwezo wa kuwasaidia wale wanaoziabudu - Isa. 44:9-20; Zab. 115:4-7.  
Wazifanyao sanamu watafanana nazo - Zab. 115:8; Yer. 2:5; Hos. 9:10.  
Kutoa sadaka kwa sanamu ni kushirikiana na mashetani - 1 Kor. 10:19-20.  
Kuabudu sanamu ni kufanya ukahaba (uasherati) wa kiroho - Kum. 31:16; Waamuzi 2:17; Hos. 1:2.  
Mataifa hufanya ibada ya sanamu isiyo halali - 1 Pet. 4:3.  
Sanamu ni vitu vyaubatili visivyo na maana - Mdo. 14:15.



### Wakristo Wameonywa Wasiabudu Sanamu:

Wanapaswa kujiepusha na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu - Mdo. 15:20.

Ni tendo la mwili - Gal. 5:19.

Wathesalonike waliziacha sanamu wakamgeukia Mungu - 1 Thes. 5:21.

Msichangamane na waabudu sanamu - 1 Kor. 5:10-11.

Wengine walikuwa dhaifu kwa sababu walikuwa wameizoelea sanamu - 1 Kor. 8:4-7.

Hakuna mapatano kati ya hekalu la Mungu na sanamu - Yoshua 24:14-15, 23; 1 Fal. 18:21; 2 Kor. 6:16.

### Adhabu Ya Waabudu Sanamu:

Hawataugia Ufalme wa Mungu - Gal. 5:19-21; 1 Kor. 6:9-10; Ufu. 21:27; 22:15.

Sehemu yao ni katika ziwa la moto - Ufu. 21:8.

## **Kuanguka Kutoka Kwenye Neema**

### Watu Wa Mungu Wamehifadhiwa Na Mungu Kwa Imani Yao:

Wamehifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo - Yuda 1.

Wanalindwa na nguva za Mungu kwa njia ya imani - 1 Pet 1:5.

Wale wanaolisikia neno la Kristo na kumfuata wamehifadhiwa mkononi mwake - Yn. 10:27, 28

Mungu ana uwezo wa kuwafanya watumishi wake wasimame - Rum. 14:4.

Mungu huwapa Wakristo njia ya kutokea wakati wa majaribu - 1 Kor. 10:13

Mungu huwapa neema wale wajinyenyekeshao - 1 Pet. 5:5-7; Yak. 4:6.

Hurudiwa na Mungu isije ikawapasa adhabu pamoja na dunia - 1 Kor. 11:32; Ebr. 12:5-12

### Lakini Inawezekana Watu Wa Mungu Kuipoteza Imani yao Na Kuangamizwa:

Wengine wamejitenga na imani - 1. Tim. 4:1.

Wale watafutao kuhesabiwa haki kwa sheria huanguka na kutoka katika hali ya neema - Gal. 5:4.

Wale waiachoa imani yao hujitenga na Mungu - Ebr. 3:12.

Wanapaswa kufanya bidii ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi - Ebr. 4:11.

Anayejidhanika kuwa amesimama na aangelie asianguke - 1. Kor. 10:12.

Kama wataishi kwa kufuata mambo ya mwili watakufa - Rum. 8:12,13.

Wameonywa wasianguke na kuuacha uthibitifu (uaminifu) wao - 2 Pet. 3:17.

Wanapaswa kuwa waangalifu ili kwamba mtu ye yote asiipungukie neema ya Mungu - Ebr. 12:15.

Wale wapandao kwa mwili, watawuna uharibifu - Gal. 6:7-9.

Wale waliotakaswa kwa damu ya Kristo wanaweza kumkanyaga Kristo hatimaye wakaangamizwa - Ebr. 10:29.

Wale wasiodumu ndani ya Kristo watatupwa motoni - Yn. 15:1-6.

Wale wamkatao yeye anenaye hawataokoka - Ebr. 12:25.

**KUMBUKA:** Maonyo yote haya yaliandikwa kwa Wakristo, sio watu wa nje.

## **Kuiba**

### Tukiiba Tunavunja Sheria Ya Mungu:

Mungu aliwaambia wana Waisraeli wasiibe - Kut. 20:15.  
Tusiibe - Law. 19:11.  
Yesu alifundisha tusiibe - Mat. 19:18.  
Wizi hawatarithi ufalme wa mbinguni - 1 Kor. 6:10.

## **Kuimba**

Mt. 26:30; Mk. 14:26 - Tuimbe kama Yesu alivyoimba  
Mdo. 16:25 - Kila mmoja aimbe.  
I Kor. 14:15 - Ufahamu katika kuimba.  
Efe. 5:19 - Kushangilia mioyoni mwetu.  
Kol. 3:16 - Fundisha na kuonya kwa nyimbo.  
Yak. 5:13 - Imba na moyo wenye furaha  
Ebr. 2:12 - Imba kamba kusanyiko.  
Rum. 15:9 - Mtukuze Mungu katika kuimba.

## **Kuja Kwa Mara Ya Pili Kwa Kristo**

### Kwa Hakika Yesu Atakuja:

Atakuja jinsi ile ile alivyokwenda mbinguni - Mdo. 1:11.  
“Nitakuja Tena” - Yn. 14:3  
Atakuja tena kuwachukuwa watu wake - 1 Thes. 4:13-18.  
“Kila jicho litamwona” - Ufu. 1:7.

### Je! Atakujaje Tena?

Katika mawingu kwa nguvu nyingi na utukufu - Mdo. 1:11; Mk. 13:26.  
Katika siku isiyojulikana - Mt. 26:36.  
Katika hali ya kutisha - 1 Thes. 5:2-3.  
Atakuja kwa ghafula - Lk. 17:26-30.

### Kristo Atakuja Kufanya Nini?

Atawafufua wafu - Yn. 5:28, 29.  
Atauhukumu ulimwengu - Mt. 25:31-46; Mdo. 17:31.  
Atawaadhibu wasiotii - Mt. 13:41, 42, 49, 50; 2 Thes. 1:7-9.  
Atawachukua watu wake na kuwapeleka mbinguni - Mt. 25:34; Mt. 13:43; Yn. 14:1-3; Flp. 3:20-21; I  
thes. 4:17-18.

### Pamoja Na Tuamini Katika Kuja Kwake Tunapaswa Kufanya Nini?

Tusilale au tusilewe bali tukeshe - 1 Thes. 5:6.

Tunapaswa kukesha na kuomba tusije tukalemewa na masumbufu ya maisha - Lk. 21:34-36.

Tunapaswa kujitakasa - 1Yoh. 3:3; 2 Pet. 3:14.

Tunapaswa kuenenda katika utakatifu tukiwa na matumaini ya kuja kwake - 2 Pet. 3:11-12.

Tunapaswa kuwahubiria watu wote njia ya wokovu ili nao waweze kuwa tayari kwa kuja kwake - Rum. 1:14-16; 2 Thes. 1:7-9; Kol. 1:28-29.

### **Kukiri**

#### Kukiri dhambi:

Zab 32:5, Daudi alikuwa tayari kukiri dhambi zake.

Tukiwa tayari kukiri dhambi zetu, “Yeye ni mwamimifu kutusamehe,” 1 Yoh. 1:9.

Kama wataishi kwa kufuata mambo ya mwili watakufa - Rum. 8:12, 13.

Wameonywa wasianguke na kuuacha utiifu (uaminifu) wao - 2 Pet. 3:17.

#### Kukiri na kuokolewa:

Mdo. 8:37 - Towashi alikiri kabla ya ubatizo kwamba Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu.

Rum. 10:9,10 - Kukiri kuna ongoza wokovuni.

1 Yoh. 4:2 - Kila anayemkiri Yesu kwamba alikuja katika mwili ni wa Mungu.

1 Yoh. 4:15 - Kiri kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, kisha Mungu atakaa ndani yako.

Mt. 10:32 - Tukiwa tayari kumkiri Yesu basi atakuwa tayari kukiri kwamba tu wafuasi wake.

Yn. 12:42 - Wale ambao hawakukiri walitengwa, tazama Yn. 9:22.

Rum. 14:11 - Katika hukumu kila goti na kukiri kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, tazama pia Flp. 2:11.

### **Kulewa**

#### Matokeo Ya Kulewa.

Kunashusha heshima - Mwa. 9:21-22.

Kunaleta ugomvi - Mith. 20:1.

Kunaleta umaskini - Mith. 23:21.

Kunachafua haki - Isa. 5:22-23.

Kunachanganya akili - Isa. 28:7.

Ni uovu - Rum. 13:13.

Hakuna talatibu - Mat. 24:48-51.

Tutashindwa kuwa waangalifu - 1 Thes. 5:6-7.

#### Kulewa Ni Mfano Wa:

Uangamizo - Isa. 49:26.  
Mawimbi makali - Zab. 107:25-27.  
Upumbavu - Isa. 19:14.  
Makosa - Isa. 28:7.  
Kipofu cha kiroho - Isa. 29:9-11.  
Mateso - Ufu. 17:6.

#### Adhabu Ya Kulewa:

Kifo - Kumb. 21:20-21.  
Utatengwa na uhusiano - 1 Kor. 5:11.  
Utatengwa na mbinguni - 1 Kor. 6:9, 10; Gal. 5:19-21.

### **Kulitaja Bure Jina la Mungu (Bwana)**

#### Tusitumie Vibaya Jina La Bwana:

Tusitaja jina la Mungu bure - Kut. 20:7.  
Tusiape kwa jina la Mungu - Mat. 5:33.  
Tusichafu jina la Bwana - Law. 22:2.  
Tuogope jina la Bwana - Kumb. 28:58.

#### Tutumie Jina La Bwana Kwa Halali:

Tulitakase jina lake - Isa. 29:23.  
Jina lake ni takatifu - Isa. 57:15.  
Tulibariki jina la Bwana milele na milele - Dan. 2:20.

### **Kumkaribia Mungu**

#### Wenye Dhambi Hawawezi Kumfikia Mungu Mtakatifu Wakiwa Katika Dhambi Zao:

Dhambi zao huwatenganisha na Mungu - Isa. 59:1-2.  
Wao wamefarikishwa na ni adui kwa sababu ya dhambi zao - Kol. 1:21.  
Wamekufa dhambini mwao na hawana Mungu - Efe. 2:1, 12.

#### Wenye Dhambi Hupata Kumkaribia Mungu Kupitia Kwa Yesu Kristo:

Mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, naye ni Yesu Kristo - 1 Tim. 2:5.  
Yeye ndiye Njia ya pekee ya kumwenda Mungu - Yoh. 14:6; Mdo. 4:12.  
Kristo hutuleta kwa Mungu kwa njia ya mateso yake - 1 Pet. 3:18; Ebr. 10:19-20.

Twaletwa karibu na Mungu kwa njia ya damu yake Yesu - Efe. 2:13.  
Wayahudi na Mataifa wamepata kumkaribia Mungu katika Roho Mtakatifu - Efe. 2:18.  
Tumepata kumkaribia Mungu kwa njia ya Imani - Rum. 5:2.  
Tuna ujasiri na uwezo wa kumkaribia kwa njia ya kumwamini Kristo - Efe. 3:12.

#### Wakristo Wanapaswa Kumkaribia Mungu Kwa Maombi Yao Kwa Njia Ya Yesu:

Twamomba Baba kwa jina la Kristo - Yn. 16:23-24.  
Kama tukitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, naye ni Yesu Kristo - 1 Yoh. 2:1.  
Kristo huwasaidia wale wanaojaribiwa - Ebr. 2:17, 18.  
Twamkaribia Mungu kwa ujasiri kwa sababu ya Kuhani wetu aliye Mkuu - Ebr. 10:21-23; 4:14-16.

### **Kumkiri Kristo**

#### Kumkiri Kristo Wakati Mwingine Ni Kazi Ngumu:

Wale waliomkiri Kristo walitengwa na sinagogi la Wayahudi - Yn. 9:22.  
Baadhi ya wakuu walikosa kumkiri Yesu Kristo kwa sababu ya Mafarisayo - Yn. 12:42-43.  
Hata wakati wa mateso. Wakristo wanapaswa kumkiri Kristo - Mt. 10:32, 33.  
Wale wanaomwonea Kristo haya watakataliwa - Mk. 8:38.  
Ikiwa tutamkana, naye pia atatukana - 2 Tim. 2:12; Mt. 10:33.

#### Walakini, Mungu Hutamani Watu Wote Wamkiri Kristo Daima:

Wale wanaomkiri Kristo kama Bwana wataokoka - Rum. 10:9, 10.  
Mungu hukaa ndani ya wale wanaomkiri Kristo kwamba ni Mwana wa Mungu - 1 Yoh. 4:15.  
Kila amkiriye Mwana anaye Baba pia - 1 Yoh. 2:23.  
Kila roho ikiriyo kwamba Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu - 1 Yoh. 4:2.  
Wakristo wanapaswa kuyashika maungamo yao - Ebr. 3:1; 4:14.  
Kila ulimi ukiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana - Flp. 2:9, 10.

#### Kristo Atawakiri Wale Wamkiri:

Atawakiri mbele za Baba yake - Mt. 10:32.  
Atawakiri mbele za malaika wa Mungu - Luka 12:8.  
Yeye ashindaye, Yesu atamkiri mbele za Baba yake na mbele ya malaika - Ufu. 3:5.

#### Mifano Ya Kumkiri Yesu:

Nathanaeli - Yn 1:49.  
Petro - Yn. 6:68, 69; Mt 16:13-18.  
Mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa kwake - Yn. 9:25, 35-38.  
Martha - Yn 11:27.

Stefano - Mdo. 7:52, 59.  
Paulo - Mdo. 9:29.  
Timotheo - 1 Tim. 6:12.  
Baadhi ya Wakristo kule Pergamo - Ufu. 2:13.

### **Kuoana Tena**

#### Je, Tunaweza Kuoana Tena?

Unaweza kuoana tena kwa sababu mbili tu.  
1) Kama mwenzako amekufa - Rum. 7:3-4; 1 Kor. 7:39.  
2) Kama mwenzako ametembea nje ya ndoa - Mat. 5:31-32.

#### Kama Unahaki Ya Kuoana Tena, Kuna Sheria Ambyo Unatakiwa Kufahamu.

Kama mwanamke amefiwa anaweza kuolewa tena, katika Bwana Tu - 1 Kor. 7:39.  
Huwezi kuoana mtu ambayo ameachwa tu bila kufuata maandiko - Mat. 19:9.

### **Kusikia**

Rum. 10:17, Lazima kusikia Neno la Kristo, Mdo 3:37.  
Tusikialo (la kweli) tuamini, Rum. 10:14.  
Tujifunze kutokana na tusikiayo, Yn. 6:45.  
Tuwe watendaji, Yak. 1:22.  
Kuwa baraka kusikia na kutenda, Ufal. 1:3.

### **Kutahayari (Kuaibishwa, Haya)**

Siionei haya Injili - Warumi 1:16.  
Usiuonee haya ushuhuda wa Bwana - 2 Tim. 1:8.  
Sitahayari kwa maana namjua yeye - 2 Tim. 1:12.  
Mkristo asione haya ateswapo - 1 Petro 4:16.  
Sitaibika kamwe kwa neno lolote - Wafilipi 1:20.  
Mtu ye yote atakayemwonea Kristo haya, Yesu naye pia atamwonea haya mtu huyo - Marko 8:38; Mt. 10:33; Luka 9:26.

### **Kuongama Dhambi**

#### Mungu Aliwataka Wana Wa Israeli Waungame Dhambi Zao:

Wale walioleta sadaka ya hatia - Law. 5:5, 6.  
Mungu alipendezwa na wale waliuongama dhambi zao - Law. 26:40-42; Hosea 5:15.  
Yeremia aliwasihi watu waungame dhambi zao - Yer. 3:13.

Danieli aliziungama dhambi zake na zile za watu wake - Dan. 9:1-20.  
Wale waziungamao dhambi zao na kuziacha watapata rehema - Mit. 28:13.

Wakristo Pia Wanapaswa Kuungama Dhambi Zao:

Tukiziungama dhambi zetu, Mungu atatusamehe - 1 Yoh. 1:9.  
Akataaye kuziungama dhambi zake hujidanganya mwenyewe - 1 Yoh. 1:8-10.  
Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi - Yak. 5:16.

Wale Waziungamao Dhambi Zao Wanapaswa:

Kukubali adhabu ya uovu wao - Law. 26:41.  
Kuwa na roho ya unyenyekevu - Yer. 3:25; Usaya 64:6-7; Lk. 18:13.  
Kuacha dhambi zao - Mit. 28:13; Eze. 18:30, 31.  
Kuomba msamaha - Zab. 51:1; 1 Yoh. 1:9.

Mifano Ya Wale Walioziungama Dhambi Zao:

Nehemia - Neh. 9:16-38.  
Danieli - Dan. 9:1-20.  
Daudi - Zab. 32:5; 51:4.  
Yeremia - Yer. 14:20.  
Wale waliobatizwa na Yohana - Mt. 3:6.  
Petro - Luka 5:8.  
Mtoza ushuru - Luka 18:13.  
Mwana mpotevu - Luka 15:21.

**Kweli**

Kweli Hutoka Kwa Mungu:

Mungu wa kweli - Zab. 31:5; Isa 65:16.  
Kristo ni kweli - Yn. 14:6; 1:14; 8:45.  
Roho Mtakatifu ni Roho wa kweli - Yn. 14:17; 16:13.  
Roho Mtakatifu aliwaongoza mitume na kuwaweka katika kweli yote - Yn. 16:13.  
Neno la Mungu ni kweli - Yn. 17:17.  
Hukumu ya Mungu ni ya kweli - Rum. 2:2.  
Kweli ilikuja kwa njia ya Yesu Kristo - Yn. 1:17.  
Kristo alikuja ulimwenguni ili aishuhudie kweli - Yn. 18:37.  
Kweli iko katika Kristo - Efe. 4:21.

Umuhimu Wa Kweli:

Kweli huambatana na utauwa - Tito 1:1.

Huwatakasa wanadamu - Yn. 17:17, 19.  
Wanadamu husafisha roho zao kwa kuitii kweli - 1 Pet. 1:22.  
Viuno ni vya kufungiwa kweli - Efe. 6:14; Zab. 91:4.  
Hudumu milele - 2 Yoh. 2.  
Kanisa ni nguzo na msingi wa kweli - 1 Tim. 3:15.  
Kweli haimo ndani ya wale wasiungama dhambi zao - 1 Yoh. 1:8.  
Wanadamu huzaliwa kwa neno la kweli - Yak. 1:18.  
Kweli huwaweka wenye dhambi huru - Yn. 8:32.  
Aitendaye kweli huja kwenye nuru - Yn. 3:21.

#### Watu Waovu:

Hawana kweli - Hos. 4:1.  
Hawasemi kweli - Yer. 9:5.  
Huzoesha ndimi zao husema uongo - Yer. 9:3-5.  
Hawaitii kweli - Rum. 2:8.  
Hupingana na ile kweli - 2 Tim. 3:8.  
Wameikosa kweli - 1 Tim. 6:5.  
Humfanya Mungu kuwa mwongo kwa sababu hawauamini ushuhuda wake - 1 Yoh. 5:9, 10.  
Huitukana njia ya kweli - 2 Pet. 2:2.  
Kweli imekatiliwa mbali na vinywa vyao - Yer. 7:28.  
Huipinga kweli kwa uovu - Rum. 1:18.  
Waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo - Rum. 1:25.  
Wameikosa ile kweli - 2 Tim. 2:18.  
Wengine hawawezi kabisa kuufikia ujuzi wa kweli - 2 Tim. 3:7.  
Huyaepusha masikio yao wasisikie yaliyo kweli - 2 Tim. 4:4.  
Huyafuata maagizo ya watu wajiepushao na yaliyo kweli - Tito 1:14.

#### Watoto Wa Mungu:

Humwabudu Mungu katika kweli - Yn. 4:24; Zab. 145:18.  
Humtumikia Mungu katika kweli - 1 Sam. 12:24.  
Huenenda mbele zake katika kweli - 1 Fal. 2:4; 2 Fal. 20:3.  
Hufurahi katika kweli - 1 Kor. 13:6.  
Husema kweli kwa kila mtu - Efe. 4:25.  
Huyatafakari yaliyo kweli - Flp. 4:8.  
Huiweka kweli ndani yao - Mit. 3:3.  
Huiandika kweli mioyoni mwao - Mit. 3:3.  
Hupendezwa na kweli iliyo mioyoni mwao - Zab. 51:6.  
Huitii kweli - 1 Pet. 1:21.  
Huupokea upendo wa kweli - 2 The. 2:10.  
Huidhihirisha kweli - 2 Kor. 4:2.  
Hulitumia kwa halali neno la kweli - 2 Tim. 2:15.



Huwa na viuno vilivyofungiwa kweli - Efe. 6:14.  
Husema kweli mioyoni mwao - Zab. 15:1, 2.  
Husema kweli katika upendo - Efe. 4:15.  
Humrejeza mtu aliyepotelea mbali na kweli - Yak. 5:19.  
Huthibitishwa katika kweli - 2 Pet. 1:12.  
Hupenda kweli - 1 Yoh. 3:18.  
Huenenda katika kweli - 2 Yoh. 4; 3 Yoh. 4.  
Ni watenda kazi pamoja na kweli - 3 Yoh. 8.

### **Madhehebu**

#### Madhehebu Ya Wayahudi:

Dhehebu la Mafarisayo - Mdo. 15:5; 26:5.  
Dhehebu la Masadukayo - Mdo. 5:17.  
Wafuasi wa Kristo waliitwa “dhehebu” na adui zao - Mdo. 24:5, 14; 28:22.  
Yesu aliyapinga madhehebu ya Wayahudi kwa sababu waliliacha Neno la Mungu na kufuata mapokeo yao - Mk. 7:7-13; Mt. 15:8, 9.

#### Mungu Hataki Madhehebu Kati Ya Watu Wake:

Mungu anataka umoja wa dini - Yn. 17: 20-23; 1 Kor. 1:10-13; Efe. 4:3-6.  
Kristo hakuanzisha madhehebu mengi yanayotofautiana:  
1. “Kanisa langu” - Mt. 16:18.  
2. “Mwili mmoja” - Efe. 4:4; 1:22, 23.  
Mungu huyapinga madhehebu - 1 Kor. 1:1-13; 10:19; Gal. 5:20; 2 Pet. 2:1.  
Madhehebu yapo kwa sababu watu hufuata mapokeo ya wanadamu badala ya neno la Mungu peke yake - Mk. 7:7-12; Mt. 15:7-9; Rum. 16:17.

#### Angalia Umoja wa Dini.

### **Majaribu Hayatoki kwa Mungu**

#### Hatupaswi Kujaribiwa.

Tuwewangalifu na tuombe tusiingie katika majaribu - Mat. 26:41; Mk. 14:38; Luka 22:40, 46.  
Wakristo dhaifu wataanguka wakati wanajaribiwa na Shetani - Luka 8:13.  
Mungu anabariki yule mtu ambaye anayashinda majaribu - Yak. 1:12.

#### Hatujaribiwa na Mungu.

Shetani anataka kutupa sisi majaribu - 1 Kor. 10:13.  
Hatujaribiwa na Mungu - Yak. 1:13.

### Tunajaribiwa na Shetani.

Mjaribu alikwenda kwa Yesu iliamjaribu - Mat. 4:3, 5, 8.

Shetani alimaliza kumjaribu Yesu akatoka - Luka 4:13.

Paulo aliogopa labda mjaribu alikuwa ana wajaribu watu wa Mungu - 1 Thes. 3:5.

Shetani ni Simba anasubili iliavamia - 1 Pet. 5:8.

### **Upigaji wa Makofi**

Mambo yote yatendeke kwa kujengwa na Mungu - I Kor. 14:26.

### Kuna aina mbili za upigaji makofi, na zote ni makosa kufanyika katika ibaada.

Kwa njia ya kushangilia. Kukubali au kuonyesha furaha - I Kor. 14:16 Sema Amina!

Kisha kuna kupiga makofi kufuata mpigo.

Efe. 5:19- Imba na kushangilia, sio kupiga makofi na kushangilia.

### **Malaika**

#### Asili Na Historia Ya Malaika:

Waliumbwa na Mungu - Neh. 9:6; Kol. 1:16.

Hawahesabiki - Ebr. 12:22.

Humwabudu Mungu daima - Zab. 103:20; Ufu. 5:11-13; 7:11-12.

Humwabudu Kristo daima - Ebr. 1:6; Ufu. 5:11-13.

Humtii Kristo - Efe. 1:21; Kol. 1:16; 2:10; 1 Pet. 3:22.

Roho watumikao - Ebr. 1:14; Mdo. 27:23.

Huwalinda watu wa Mungu daima - Zab. 34:7; 91:11-12; Dan. 6:22; Mt. 18:10.

Watu wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua - Ebr. 13:2.

Mara nyingine waliweza kuonekana kama watu - Mwanzo 18:2, 16.

Hawaoi - Mt. 22:30; Mk. 12:25.

Hutamani kujua kusudi la milele la Mungu katika Injili - 1 Pet. 1:10-12.

Baadhi yao walikosa na wamewekwa katika vifungo vya giza - 2 Pet. 2:4; Yuda 6.

Moto wa milele umetayarishwa kwa ajili ya malaika wa Shetani - Mt. 25:41.

#### Kazi Ya Malaika Katika Agano La Kale:

Walifafahamisha Ibrahimu na Sara juu ya kuzaliwa kwa Isaka - Mwa. 18.

Waliiharibu miji ya Sodoma na Gomora - Mwa. 19:1-13.

Walimwokoia Lutu na binti zake - Mwa. 19:15-16.

Walionekana katika ndoto ya Yakobo - Mwa. 28:10-11.

Walimpa Musa sheria katika mlima Sinai - Mdo. 7:53; Gal. 3:19.

Waliwaongoza Waisraeli kuingia nchi ya ahadi - Kut. 23:23.  
Mmoja alijaribu kumzuia Balaam asitende maovu - Hesabu 22:22-35.  
Waliiokoa Yerusalemu kutokana na ushambulizi wa Waashuri - 2 Fal. 19:35.  
Waliwaokoa Shadraka, Meshaki na Abednego kutokana na tanuru la moto - Dan. 3:13-28.  
Waliifunga midomo ya simba na kumwokoza Danieli - Dan. 6:16-22.

#### Yesu Kristo Na Huduma Ya Malaika:

Malaika alimjulisha Zakaria juu ya kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji - Luka 1:11-12.  
Mmoja alimtokea Mariamu na kumwambia kwamba atamzaa Yesu - Luka 1:26-38.  
Mmoja alimtokea Yusufu kuhusu Yesu - Mt. 1:20.  
Waliwatangazia wachungaji habari za kuzaliwa kwa Yesu - Luka 2:8-13.  
Walimtia nguvu Yesu alipojaribiwa - Mt. 4:11; 22:43.  
Walililinda kaburi la Yesu na wakawa wa kwanza kutangaza ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu - Mt. 28:2-7.  
Walitangaza juu ya kurudi kwa Yesu kwa mara ya pili - Mdo. 1:9-11.  
Watarudi pamoja na Yesu katika mwali wa moto - 2 The. 1:7-11; Mt. 16:27; Marko 8:38.  
Watamsaidia atakapowatenganisha wema na waovu - Mt. 13:41-42.  
Yesu ni bora zaidi kuliko malaika - Ebr. 1:4-14.

#### Mafundisho Ya Yesu Kuhusu Malaika:

Malaika wako mbinguni - Mt. 22:30.  
Watu wa Mungu wako na malaika zao - Mt. 18:10.  
Malaika hufurahi mwenye dhambi mmoja anapotubu - Luka 15:10.  
Watasikia kukiri na kukana kwa watu - Luka 12:8-9.  
Huwapeleka wenye haki Peponi - Luka 16:22.  
Watamsaidia Mungu katika siku ya hukumu - Mt. 13:41; 25:31.  
Wavunaji wa siku ya mwisho ni malaika - Mt. 13:39.  
Watawatenganisha wema na waovu - Mt. 13:41, 49.  
Hawajui siku ya kurudi kwake Bwana - Mt. 24:36.  
Shetani ana malaika zake - Mt. 25:41.

#### Kanisa Na Huduma Ya Malaika:

Malaika waliwafungulia mitume wakatoka gerezani - Mdo. 5:19; 12:7.  
Malaika walimpiga Herode aliyekuwa adui wa kanisa - Mdo. 12:23.  
Walisimama karibu na Paulo na kumtia nguvu - Mdo. 27:23-24.  
Huwahudumia wale waupokeao wokovu - Ebr. 1:14; Mt. 18:10.  
Wakristo watawahukumu malaika - 1 Kor. 6:3.  
Hufurahi mwenye dhambi mmoja anapotubu - Luka 15:7-10.  
Yesu hakuja kuwakomboa malaika, bali wanadamu - Ebr. 2:16.  
Wakristo hawapaswi kuwaabudu malaika - Kol. 2:18; Ufu. 19:10; 22:9.

## **Mambo Ya Milele**

### Mungu Ni Wa Milele:

Mungu wa milele - Kum. 33:27; Isa. 40:28; Rum. 16:26.

Mfalme wa Milele - Yer. 10:10; 1 Tim. 1:17.

Uweza wake ni wa milele - Rum 1:20.

Upendo wake ni wa milele - Yer. 31:3.

Kusudi lake la milele - Efe. 3:11.

Yesu ni wa milele - Yn. 1:1-3; Isa. 9:6.

Roho wa milele - Ebr. 9:14.

Mambo yasiyoonekana ni ya milele - 2 Kor. 4:18.

### Mungu Amewaandalia Watu Wake Mambo Ya Milele:

Maneno yake ni ya milele - Isa. 40:6-8; 1 Pet. 1:24, 25; Mt. 24:35.

Injili ya milele - Ufu. 14:6.

Agano la milele - Ebr. 13:20.

Ukombozi wa milele - Ebr. 9:12.

Wokovu wa milele - Ebr. 5:9.

Faraja ya milele - 2 The. 2:16.

Ufalme wa milele - 2 Pet. 1:11.

Nyumba ya milele - 2 Kor. 5:1; Zab. 23:6.

Makao ya milele - Lk. 16:9.

Uzima wa milele - Yn. 3:16; 5:24; 1 Yoh. 5:11-13; Mk. 10:30; Rum. 6:23.

Furaha ya milele - Isa. 35:10; Mt. 25:21.

Utukufu wa milele - 2 Tim. 2:10; 1 Pet. 5:10.

### Wale Ambao Wamepotea Pia Watapata Mambo Ya Milele:

Dhambi ya milele - Mk. 3:29.

Hukumu ya milele - Ebr. 6:2.

Vifungo vya milele - Yuda 6.

Adhabu ya milele - Mt. 25:46.

Moto wa milele - Mt. 25:41.

Maangamizi ya milele - 2 The. 1:9.

## **Mamlaka Au Uwezo**

### Mamlaka Ya Mungu:

Mungu ndiye Muumbaji na vyote vinavyoonek ana ni mali yake. Anayo mamlaka au uwezo juu ya watu,

malaika na viumbe vyote - Mwa. 1:1; Zab. 135:5-6; Dan. 4:34-35; Zab. 24:1; Mdo. 14:15-17; 17:24-28; 1 Pet. 4:19; Ufu. 4:8-11; 1:8.

#### Mamlaka Ya Yesu Kristo:

Alifundisha kama mtu aliye na mamlaka au uwezo - Mt. 7:24-29; 11:27; Yn. 6:46, 68.

Mamlaka au uwezo wa Kristo hutoka kwa Mungu aliye Baba - Yn. 5:19; 7:16; 8:28; 12:49; Mt. 17:5.

Mungu husema kwa njia ya Kristo, aliye na mamlaka yote - Ebr. 1:1-2; Mt. 28:18; Mdo. 2:36; 4:12; 10:36; Flp. 2:9-11; Efe. 1:20-23; 1 Pet. 3:22; Ufu. 17:14; 19:16.

#### Mamlaka Ya Mitume:

Yesu aliwapa uwezo kwa njia ya Roho Mtakatifu - Yn. 14:26; 15:26; 16:12-14; Mdo. 1:8.

Maneno ya Mitume ni maneno ya Mungu - Gal. 1:8-12; 1 Kor. 14:37; 1 The. 2:13.

Wale wanaowakataa mitume huwakataa Kristo na Mungu pia - Mt. 10:40; Luka 10:16; 1 The. 4:8; Gal. 1:8-9.

#### Baadhi Ya Namna Zingine Za Mamlaka:

##### **Katika Jamii:**

Mwanamume anayo mamlaka juu ya mkewe - 1 Kor. 11:3; 1 Tim. 2:12; Efe. 5:22; 1 Pet. 3:1-6.

Wazazi wanayo mamlaka juu ya watoto wao - 1 Tim. 3:4, 12; Efe. 6:1-3.

##### **Mamlaka Ya Sherikali:**

Wamewekwa na Mungu - Warumi 13:1-6; Yn. 19:11.

Wakristo lazima wawatii wale wenye mamlaka - Rum. 13:1; 1 Pet. 2:13-17; Mt. 22:17-21.

Lakini wanapaswa kumtii Mungu kuliko wanadamu - Mdo. 4:19; 5:29.

Mamlaka Ya Shetani:

Ana uwezo juu ya wale watendao maovu, lakini uwezo huo umeharibiwa na Kristo - Luka 22:53; Kol. 1:13; Ebr. 2:14-15; 1 Yoh. 3:8; Mdo. 26:18; Rum. 16:20; 1 Pet. 2:9; 1 Kor. 10:13.

#### **Mamlaka ya Yesu**

#### Ilitabiriwa Kwamba Ufalme Kwa Wote Kwa Ajili ya Kuufuata Na Kutii.

Kumb. 18:15, 18 - Musa alisema nabii ambaye alikuwa anakuja watu wangemsikia. Unabii huu ulidhihirika katika Mdo 3:22-23.

Dan. 7:14 - Alipewa ufalme na mataifa yote yatamtumikia milele.

#### Yesu Alipewa Mamlaka Yote Mbinguni Na Duniani.

Ebr. 1:2 - Mungu leo anaongea kwa kupitia katika Mwanawe.  
Mt. 28:18 - Mamlaka yote mbinguni na duniani amekabidhiwa Yesu.  
Mt. 17:1-2 - Yesu alikuwa amepewa mamlaka juu ya miili yote ili atoe uzima wa milele.  
Mt. 7:29 - Yesu alifundisha kama mwenye mamlaka.  
1 Kor. 15:24-25 - Yesu atamiliki hadi atakapowaweka adui zake chini ya miguu yake na kukabidhi ufalme kwa Mungu Baba.

### **Je, Manabii Wapo Leo?**

#### Nabii Wetu Wa Mwisho Leo Ni Yesu.

Muda ulipokuwa mzuri Mungu alituma Yesu - Gal. 4:4.  
Yesu alileta neema na kweli - Yn. 1:17.  
Mungu anaongea nasi leo kupitia mwanee - Ebr. 1:1-2.

#### Kuna Nabii Alifuata Yesu?

Kama mtu atahubiri injili yo yote tofauti alaniwe - Gal. 1:6-9.  
Tusiongeze katika amri ya Mungu - Kumb. 4:2.  
Kama hatufuati maneno ya Yesu basi hatuna Mungu - 2 Yoh. 9.  
Tutahukumiwa na maneno ya Yesu - Yoh. 12:48.  
Ukikataa maneno ya Yesu unakataa maneno ya Baba - Lk. 10:16.  
Yesu alileta mambo yote yanayofaa kwa mafundisho - 2 Tim. 3:16-17; 2 Pet. 1:3.  
Tunatakaswa kupitia neno lake - Yoh. 17:17.

### **Maombi (Kusali)**

#### Mafundisho Ya Yesu Juu Ya Maombi:

Wakristo wanapaswa kumwomba Mungu siku zote, wala wasikate tamaa - Lk. 11:5-8; 18:1-8.  
Wanapaswa kuomba kwa mioyo ya unyenyekevu - Lk. 18:10-14.  
Wanapaswa kuomba wakiadini - Mk. 11:24.  
Wanapaswa kuomba wakiwa wenye kusamehe - Mt. 18:21-35.  
Hawapaswi kuomba ili waonekane na watu - Mt. 6:5-8; 23:14; Mk. 12:38-40.  
Wanapaswa kuomba wakikeshwa - Mk. 13:33; 14:38; Mt. 26:41.  
Wanapaswa kuomba ili kondoo wasitawanyike - Mt. 9:36-38.  
Wanapaswa kuwaomba adui zao - Mt. 5:44; Lk. 6:28.  
Wanapaswa kuomba kwa ajili ya mahitaji ya kila siku - Mt. 6:11; Lk. 11:3.  
Wanapaswa kuomba kwamba wasishindwe na majaribu - Mt. 6:13; Lk. 11:4.  
Wanapaswa kuomba ili wampokee Roho Mtakatifu, au wajazwe Roho Mtakatifu - Lk. 11:13; Efe. 5:18.

#### Maombi Ya Yesu:

Alipobatizwa - Lk. 3:21.  
Alipokwenda nyikani - Lk. 5:16; 6:12.  
Alipofuata uongozi wa Baba katika uchaguzi wa mitume wake - Lk. 6:12, 13.  
Alipoyalisha makutano mengi - Mt. 14:13-21; Yn. 6:1-13.  
Alipotoa shukrani - Lk. 1:-21; Yn. 11:41; Mt. 26:27.  
Wakati wa kuteswa kwake - Yn. 12:20-28.  
Alipowaombea wengine - Yn. 17:6-26; Lk. 22:31-34; 23:34.  
Wakati sura yake ilipogeuka - Lk. 9:29.  
Katika mlima wa Mizeituni - Lk. 22:39-45; Ebr. 5:7-9.  
Msalabani - Mt. 27:46; Lk. 23:46.

#### Njia Ya Kuomba:

Katika jina la Kristo - Yn. 14:13. (Yeye tu ndiye mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu - 1 Tim. 2:5.)  
Tunapaswa kukaa ndani ya Kristo - Yn. 15:7.  
Maneno ya Kristo yanapaswa kukaa ndani yetu - Yn. 15:7.  
Tukiisha kuzishika amri zake - 1 Yoh. 3:22.  
Sawasawa na mapenzi yake - 1 Yoh. 5:14, 15.  
Tukiisha kuwasamehe wenzetu - Mt. 6:15.  
Kwa utimilifu wa imani - Ebr. 10:22; 11:6; Mk. 11:24.  
Kwa kumtii Mungu - Lk. 22:42.  
Kwa ujasiri - Ebr. 4:14-16.  
Usiku na mchana - 1 The. 3:10; 1 Tim. 5:5.  
Bila kukoma - 1 The. 5:17; Kol. 4:2.  
Katika kila neno - Flp. 4:6.

#### Maombi Kwa Wengine:

Wafalme na wote wenye mamlaka - 1 Tim. 2:2.  
Wahubiri - Ebr. 13:18; Kol. 4:3.  
Watakatifu wote - Ebr. 6:18; 3:14-19; Flp. 1:4.  
Watu wote - 1 Tim. 2:1.  
Watu wa taifa letu - Rum. 10:1.  
Wagonjwa - Yak. 5:14.  
Wanaotuudhi - Mt. 5:44.  
Watuoneao - Lk. 6:28.  
Ndugu atendaye dhambi - 1 Yoh. 5:16.  
Kuombeana - Yak. 5:16.  
Walakani, hatuwezi kuwaombea wao ambao wameifanya migumu mioyo yao -  
Yer. 7:13-16; 14:10-14.

#### Mifano Ya Kuwaombea Wengine:

Ibrahimu aliiombea Sodomu - Mwa. 18:23-32.  
Musa aliwaombea Israeli - Kut. 32:11-14.  
Samweli aliwaombea wana wa Israeli - 1 Sam. 7:5; 12:23.  
Sulemani aliwaombea watu wake wakati wa kuzinduliwa kwa hekalu - 1 Fal. 8:30-36.  
Danieli aliziungama dhambi za Waisraeli kisha akawaombea - Dan. 9:3-19.  
Yesu aliwaombea wale waliomsulubisha - Lk. 23:34.  
Stefano aliwaombea wale waliompiga kwa mawe - Mdo. 7:60.  
Kanisa lilimwomba Petro - Mdo. 12:5.  
Petro na Yohana waliwaombea Wasamaria - Mdo. 8:15.  
Paulo aliwaombea Wakristo wa sehemu mbalimbali - Efe. 1:16; Kol. 1:9-12; 2 The. 1:11, 12.  
Paulo aliwataka Wakristo wamwombea - Efe. 6:18, 19; Kol. 4:3; Rum. 15:30-32.  
Roho Mtakatifu huwaombea watu wa Mungu - Rum. 8:26, 27.

#### Watu Wanaweza Kuomba Katika Hali (Vikao) Mbalimbali:

Wakiwa katika hali ya kusimama - 1 Fal. 8:22; Mk. 11:25.  
Wakiwa wamepiga magoti - Zab. 95:6; Lk. 22:41; Mdo. 20:36.  
Kupomoka kifudifudi, kiusouso - yaani kuanguka kifulifuli - Hes. 16:22; Yosh. 5:14; Mt. 26:39.  
Kwa kukunjua mikono - Isa. 1:15.  
Kwa kuinua mikono juu - Zab. 28:2; 1 Tim. 2:8.  
Kwa kuinua macho juu kuelekea mbinguni - Yn. 11:41; Yn. 17:1.

#### **Maongozi Ya Mungu**

##### Juu Ya Viumbe Vyote:

Yeye ni mwema kwa watu wote - Zab. 145:9.  
Huvihifadhi vyote - Neh. 9:6.  
Huvipa chakula vyote vyenye mwili - Zab. 136:25; 147:9.  
Huwalinda ndege wa angani - Mt. 6:26; 10:29.  
Viumbe vyote humtegemea - Zab. 104:27, 28; 36:6.  
Huwanyesha mvua na kuwaangazia jua na kuwapa nyakati za mavuno waovu na wema - Mt. 5:45; Mdo. 14:15-17.  
Aliziweka nyakati na kuweka mipaka kwa makazi ya mataifa yote - Mdo. 17:26.

##### Uongozi Maalum Juu Ya Watoto Wake Waaminifu:

Sisi tupo mbele za uso wake kila wakati - Zab. 139:1-5.  
Nyakati zetu ziko mikononi mwake - Zab. 31:15.  
Hutulisha maisha yetu yote - Mwa. 48:15.  
Hutufunika kwa mbawa zake - Zab. 91:4.  
Huwaongoza waamini katika njia nzuri - Mwa. 24:48-50; Kum. 8:2-15; Isa. 63:13.  
Huzitimiza ahadi zake - Hes. 26:63-65; Yoshua 21:45.  
Mungu ni mlinzi mwaninifu wa watu wake - Zab. 121:8; Isa. 27:3.



Hutuokoa kutoka kwenye ubaya - Zab. 91:3.  
Anajua hesabu ya nywele zetu vichwani - Mt. 10:30; Lk. 21:18.  
Watauwa wake hulindwa milele - Zab. 37:28.  
Malaika zake huwalinda wenye haki katika njia zao zote - Zab. 91:11.  
Wakati mwingine njia ya Mungu huonekana kuwa na kina kirefu na isiyojulikana - Zab. 73:16, 17; 77:19; Rum. 11:33.  
Mungu humfanya mwema aepukane na uovu - Mwa. 45:5-7; 50:20; Flp. 1:12.  
Katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema - Rum. 8:28.

### **Mapenzi (Kusudi, Nia)**

#### Yesu Alikuwa Kuyafanya Mapenzi Ya Mungu:

Alikuwa ayafanye mapenzi ya Mungu - Ebr. 10:7.  
Hakufuata mapenzi yake mwenyewe bali ya Mungu - Yn. 5:30.  
Chakula cha Yesu kilikuwa ni kuyatenda mapenzi ya Mungu - Yn. 4:34.  
Aliomba “Mapenzi yako yatimizwe” - Mt. 26:42; Lk. 22:42.

#### Mapenzi Ya Mungu Kwetu Sisi:

Ni kwamba hata mmoja wetu asipotee - Mt. 18:14; Yn. 6:39.  
Hapendi mtu yeyote apotee - 2 Pet. 3:9.  
Tunapaswa kuishi kulingana na mapenzi ya Mungu - 1 Pet. 4:2.  
Hutufanya kuwa wakamilifu katika kila tendo jema ili tupate kuyafanya mapenzi yake - Ebr. 13:21.  
Mapenzi ya Mungu ni kwamba tutoe shukrani kwa kila jambo - 1 The. 5:18.  
Tunapaswa kuwa wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu - Kol. 4:12.  
Mapenzi ya Mungu ni utakatifu wetu - 1 The. 4:3.  
Wakristo huteswa kwa mapenzi ya Mungu - 1 Pet. 4:19.  
Walakini, tunapaswa kuteswa kwa kutenda mema wala si maovu - 1 Pet. 3:17.  
Kwamba tuvizibe vinywa vya watu wapumbavu kwa kutenda mema - 1 Pet. 2:15.  
Tuombe sawasawa na mapenzi yake - 1 Yoh. 5:14.

#### Watu Wa Mungu Huyafurahia Mapenzi Ya Mungu:

Kuyafanya mapenzi yako mema ndiyo furaha yangu - Zab. 40:8.  
Unifundishe kuyatenda mapenzi yako - Zab. 143:10.  
“Mapenzi ya Bwana na yatendeke” - Mdo. 21:14; Mt. 6:10.  
Huendelea kusema “Bwana akipenda” - Yak. 4:15.  
Husafiri kulingana na mapenzi ya Mungu - Rum. 1:10; 15:32; 1 Kor. 4:19.  
Hujitoa wenyewe kwa mapenzi ya Mungu - 2 Kor. 8:5.  
Huyatenda mapenzi ya Mungu kwa moyo - Efe. 6:6.  
Hufahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Mungu - Efe. 5:17.

Tunabarikiwa Kulingana Na Mapenzi Ya Mungu:

Kwa mapenzi ya Mungu vitu vyote viliumbwa - Ufu. 4:11.  
Kwa mapenzi ya Mungu tulizaliwa kwa Neno la Kweli - Yak. 1:18.  
Wale wayatendao mapenzi yake wataingia mbinguni - Mt. 7:21.  
Yeye ayatendaye mapenzi yake ataishi milele - 1 Yoh. 2:17.  
Tukiisha kuyatenda mapenzi yake, tutaipokea ahadi - Ebr. 10:36.  
Tuliokolewa na dunia hii mbovu iliyopo sasa kwa mapenzi ya Mungu - Gal. 1:4.  
Paulo aliipokea ujumbe wake kwa mapenzi ya Mungu - 1 Kor. 1:1; 2 Tim. 1:1.  
Atafutaye kuyatenda mapenzi ya Mungu atayajua mafunzo ya Yesu - Yn. 7:17.  
Roho Mtakatifu hutuombea kulingana na mapenzi ya Mungu - Rum. 8:27.  
Ajuaye mapenzi ya Mungu lakini hayatendi ataadhibiwa vikali sana - Lk. 12:47.

**Mapokeo (Desturi, Mila)**

Mapokeo (desturi) katika Agano Jipya maana yake ni mafundisho ya kupokezana ama kwa maandiko au kwa maneno.

Mapokeo Ya Wayahudi:

Desturi hizo pia huitwa:  
“Mapokeo ya wazee” - Mt. 15:2; Gal. 1:14.  
“Mapokeo ya wanadamu” - Mk. 7:8.  
“Maagizo ya wanadamu” - Mk. 7:7.

Kwa sababu ya mapokeo yao:

Walilitangua Neno la Mungu - Mt. 15:6.  
Waliiacha amri ya Mungu - Mk. 7:8.  
Waliihalifu amri ya Mungu - Mt. 15:3.  
Waliikataa amri ya Mungu - Mk. 7:9.  
Walilifanya neno la Mungu kuwa halina maana - Mk. 7:13.  
Walimwabudu Mungu bure - Mt. 15:9.

Mapokea (Mafundisho) Yaliyotolewa Na Paulo: 1 Kor. 11:2; 2 Thes. 2:15; 3:6.

Mapokeo Ya Wanadamu:

Kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu - Kol. 2:8.  
Kwa jinsi ya maagizo na mafundisho ya wanadamu - Kol. 2:20-23.

**Je, Maria ni Mama wa Mungu?**

### Roho Au Mwili Ilikuwapo Kwanza?

Yesu alisema Mungu ni Roho - Yoh. 4:24.

Roho haina mwili na mifupa - Lk. 24:39.

Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, kilichozaliwa kwa roho ni roho - Yoh. 3:6.

- 1) Mariamu alizaa mwili wa Yesu siyo roho yake.
- 2) Yesu alikuwepo katika hali ya roho toka mwanzo - Yoh. 1:14-17.
- 3) Vitu vyote viliumbwa na Yesu, hata Mariamu - Kol. 1:16-17.
- 4) Kwa sababu Yesu ni Mungu na Mungu ni Roho, Mariamu ni wa mwili basi Mariamu alizaa mwili wa Yesu, sio Roho. Roho yake ilikuwepo kabla ya Mariamu kwa hiyo Mariamu siyo Mama wa Mungu.

### **Marudi Ya Kikristo**

#### Mwanzo Wa Adabu (Marudi).

Ndugu yako akikukosea - Mt. 18:15-17.

Ni vyema kupatana - Mt. 5:23, 24.

Tunapaswa kujaribu kuwasaidia wale wanorudi dhambini - Gal. 6:1.

#### Kuacha Kushirikiana Na Ndugu:

Tunapaswa kumwonya mara nyingi kujaribu kumsaidia - Gal. 6:1; Tito 3:10.

Wazee wa Kanisa huchukuwa jukumu la kuacha kushirikiana na ndugu kwa sababu:

- 1) Roho Mtakatifu amewafanya kuwa waangalizi wa kundi la Mungu - Mdo. 20:28.
- 2) Wazee wanapaswa kutoa hesabu ya kundi lao - Ebr. 13:17.

Kuacha kushirikiana na ndugu ni kazi ya washiriki wote wa Kanisa - 1 Kor. 5:4-5; 1 Tim. 5:20; 2 The. 3:6.

Kitendo hiki kinapaswa kutendeka kwa upendo kwa kusudi la kumsaidia - 1 Kor. 10:12; 1 Yoh. 2:1.

Msimhesabu ndugu aliyeachwa kama adui - 2 Thes. 3:15.

#### Maana Ya Kuacha Ushirkiano Na Ndugu: Kushirikiana Naye Ambako Kutamfanya Aendelee Na Dhambi Yake Kuachwe.

Msile na watu kama hawa - 1 Kor. 5:11.

Baada ya kuonywa mara nyingi yafaa akataliwe - Tito 3:10.

Mazungumzo yo yote naye yafaa yawe ya kumwonya na kumsihi kurudi kwa Kristo - 2 Thes. 3:14-15.

#### Sababu Ya Kuacha Ushirikiano:

Ili kuokoa roho ya Mkristo aliyeanguka - 1 Kor. 5:6; 1 Tim. 1:19-20.

Ili kulitunza kanisa liwe safi - 1 Tim. 5:20.

Ni Nani Anayefaa Kuachwa:

Mtu mzushi - Tito 3:10; Rum. 16:17.

Waasherati, wenye tamaa, waabudu sanamu, walafi, walevi na wanyang'anyi watukanaji - 1 Kor. 5:11.

Waendao bila utaratibu. Yeye aendeleaye kutenda yaliyo kinyume na sheria ya Mungu - 2 Thes. 3:6.

**Mashindano (Fitina, Ugomvi)**

Sababu Ziletazo Fitina Kati Ya Watu:

Kuchukiana huleta fitina - Mit. 10:12.

Kiburi huleta mashindano - Mit. 13:10.

Mwenye nafsi ya kutamani huchochea fitina - Mit. 28:25.

Mtu mshupavu huondokeshwa fitina - Mit. 16:28.

Kuchochea hasira huleta ugomvi - Mit. 30:33.

Walevi huleta ugomvi - Mit. 23:29, 30.

Mtu wa hasira huchochea ugomvi - Mit. 15:18.

Wapumbavu hutaka ugomvi - Mit. 20:3; 18:6.

Afunikaye kosa hupenda mashindano - Mit. 17:9.

Pasipo uchongezi fitina hukoma - Mit. 26:20.

Fitina hutokana na tamaa za mwili - Yak. 4:1.

Maswali ya upumbavu yasiyo na elimu huzaa magomvi - 2 Tim. 2:23; 1 tim. 6:4.

Watu wamkataao Mungu wamejawa na fitina - Rum. 1:19.

Kitu Cha Aibu: Fitina Kati Ya Watu Wa Mungu:

Wakorinto walikemewa kwa sababu ya fitina kanisani - 1 Kor. 1:11; 3:3; 2 Kor. 12:20.

Palipo wivu na ugomvi, ndipo palipo machafuko - Yak. 3:14-16.

Hayo ni matendo ya mwili - Gal. 5:19-21.

Wengine wanahubiri habari za Kristo kwa sababu ya husuda na fitina - Flp. 1:15.

Njia Za Kuzuia Ugomvi Au Fitina:

Tunapaswa kujiepusha na magomvi pamoja na mashindano - Tito 3:9; Mit. 20:3.

Kufanya mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano - Flp. 2:3, 14.

Asiye mwepesi wa hasira hutuliza mashindano - Mit. 15:18; 17:27; Yak. 1:19.

Usifanye urafiki na mtu mwenye hasira nyingi - Mit. 22:24; 20:3; 1 Kor. 15:33.

Njia ya upendo - 1 Kor. 13:4.

Tufuate kielelezo cha Kristo - Flp. 2:1-8.

**Mauti, Kifo**  
**(Maana yake ni “mtengano.”)**

### Kifo Cha Mwili:

Ni matengano ya mwili na roho - Yak. 2:26; Mhu. 12:7.  
Kifo kiliingia duniani kwa sababu ya dhambi - Mwa. 2:17; Rum. 5:12.  
Kila mtu hufa kwa sababu ya Adamu - 1 Kor. 15:21, 22; Mwa. 2:17; Rum. 5:12.  
Watu wamewekewa kufa - Ebr. 9:27; Mhubiri 8:8; 9:5.

### Kifo Cha Kiroho:

Ni matengano ya Mungu na mwanadamu kwa sababu ya dhambi - Isa. 59:1, 2; Efe. 2:1-2.  
Wenye dhambi wamekufa kwa sababu ya makosa yao - Kol. 2:13.  
Wenye dhambi wamefarikishwa na uzima wa Mungu kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao - Efe. 4:18.  
Yule “mwana mpotevu” alikuwa “amekufa” - Luka 15:24-32.  
Nia ya mwili ni mauti - Rum. 8:6.  
Aishiye kwa anasa amekufa - 1 Tim. 5:6.  
Wakristo wakiishi kwa kufuata mambo ya mwili watakufa - Rum. 8:12, 13; 6:1, 2, 16, 23.

### Kifo Cha Milele:

Mshahara ya dhambi ni mauti - Rum. 6:23.  
Wenye dhambi wanastahili kufa (wataka kufa) Rum. 1:32.  
Mwisho wa tamaa mbaya ni mauti - Yak. 1:14-15.  
Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto - Ufu. 20:14, 15; 21:8.  
Ni adhabu ya milele - Mt. 25:41, 46.  
Ni uharibifu wa milele - 2 The. 1:7-10.

### Kifo Cha Kristo:

Alionja mauti ili kwamba amharibu Shetani ambaye alikuwa na nguvu za mauti - Ebr. 2:14, 15.  
Alionja mauti kwa ajili ya kila mtu - Ebr. 2:9.  
Aliibatili mauti na kuufunua uzima na kutokuharibika - 2 Tim. 1:10.  
Alishinda mauti kwa ufufuo wake - Mdo. 3:15.  
Yeye ndiye Mkuu wa uzima - Mdo. 3:15.  
Ni Bwana wa waliokufa na waliohai - Rum. 14:9.  
Yesu ndiye ufufuo na uzima - Yn. 11:25.

### Kwa Hiyo, Wakristo:

Wamefunguliwa kutoka katika hofu ya mauti - Ebr. 2:15.  
Wameachwa huru mbali na sheria ya dhambi na mauti - Rum. 8:2.  
Wametoka mautini na kuingia uzimani - Yn. 5:24; 1 Yoh. 3:14.  
Wamepewa uzima - Efe. 2:1; Kol. 2:13.  
Wale walishikao neno la Kristo hawataona mauti milele - Yn. 8:51; 11:25, 26.

Mauti haiwezi kuwatenganisha na upendo wa Mungu - Rum. 8:38-39.  
Washindao hawatapatikana na madhara ya mauti ya pili - Ufu. 2:11; 20:6.  
Kufa kwa miili yao huitwa “kulala” tu - 1 Kor. 15:18; 1 Thes. 4:13, 14.

#### Vifungu Vilivyopendekezwa Kusomwa Wakati Wa Mazishi:

Wakati Mkristo amekufa: 1 The. 4:13, 14; Isa. 57:1, 2; Ayubu 19:25-27; Yoh. 11:25, 26.  
Wakati Mtoto amekufa: 2 Sam. 12:18-21; Zab. 14:1, 2; 127:3-5; Yer. 9:21; Mt. 18:2, 3; Mk. 10:13-16.  
Wakati mtu amekufa katika matatizo makubwa: Mt. 5:4, 11, 12; Yn. 21:18, 19; Mdo. 7:54-60; Ufu. 6:9-11.  
Wakati Mzee amekufa: Hes. 23:10-23; Yos. 23:14; Amu. 8:32; 1 Fal. 2:1-4; Ayu. 14:4-5; Zab. 90:9, 10; Mhu. 3:1, 2; Isa. 38; Ebr. 9:27.  
Vifungu vingine muhimu; Mwa. 3:17-19; Zab. 23; 90:12; 116:15; Ayu. 1:21; 17:1; Mhu. 9:5; 12:7; 1 Kor. 15:35-58; 2 Kor. 1:4, 5; 5:8, 10; Flp. 1:23; 1 tim. 6:7; 2 Tim. 4:6-8; Ebr. 9:27; Yak. 4:14; 1 Pet. 5:7.

### **Mbingu**

#### Mbinguni Ni Makao Ya Mungu:

Uangalie kutoka makazi yako matakatifu mbinguni - Kum. 26:15.  
Bwana, Mungu wa Mbingu - Yona 1:9.  
Baba yenu aliye mbinguni - Mt. 5:34; 23:22.  
Mbingu ni kiti cha enzi cha Mungu - Mt. 5:34; 23:22.  
Malaika wake wako mbinguni - Mt. 24:36; 26:30; 18:10; Lk. 2:15.  
Jeshi la mbinguni humwabudu - Neh. 9:6.  
Kunakuwa na furaha mbinguni kwa mwenye dhambi mmoja atubuye - Lik. 15:7, 10.

#### Yesu Kristo Ni Wa Mbinguni:

Alishuka duniani kutoka mbinguni - Yn. 3:13; 6:38.  
Alirudi mbinguni baada ya kufufuka kutoka kwa wafu - Mk. 16:19; Lk. 24:51; Mdo. 1:11; 1 Pet. 3:22; Ebr. 1:3; 8:1.  
Atakuja tena kutoka mbinguni - 1 Thes. 1:10; 4:16; 2 The. 1:7.

#### Waamini Wa Agano La Kale Wataishi Mbinguni:

Walikiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi - Ebr. 11:13-15.  
Waitamani nchi iliyo bora, yaani ya mbinguni - Ebr. 11:16.  
Ibrahimu, Isaka, Yakobo na manabii wa Mungu watakuwa katika ufalme wa Mbinguni - Mt. 8:11; Lk. 13:28.

#### Wakristo Waaminifu Wataishi Mbinguni Milele Na Milele:

Wao ni washiriki wa mwito wa mbinguni - Ebr. 3:1.  
 Uraia wao uko mbinguni - Flp. 3:20.  
 Majina yao yameandikwa mbinguni - Lk. 10:20; Ebr. 10:23.  
 Wanalo tumaini mbinguni - Kol. 1:5.  
 Wanao urithi waliowekewa mbinguni - 1 Pet. 1:4.  
 Hujiwekea hazina yao mbinguni - Mt. 6:20.  
 Wanayo hazina ya milele mbinguni - Lk. 12:33; Mt. 19:21; Mk. 10:21.  
 Wanayo thawabu kubwa mbinguni - Mt. 5:12; Lk. 6:23.  
 Wale wafanya mapenzi ya Baba ndiyo watakaolingia katika ufalme wa mbinguni - Mt. 7:21-23.  
 Wataingia katika ufalme wake wa mbinguni - 2 Tim. 4:18.  
 Wataingia katika ufalme wa milele wa Bwana - 2 Pet. 1:11.  
 Wanayo nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni - 2 Kor. 5:1.  
 Yesu alikwenda mbinguni kuwaandalia makao - Yn. 14:1-6.  
 Hakuna njaa, wala kiu, wala tabu yeyote mbinguni - Ufu. 7:16-17; 21:4.  
 Mateso ya wakati huu hayawezi kulinganishwa na utukufu wa mbinguni - Rum. 8:18; 2 Kor. 4:14-16.  
 Watabadilishwa wafanane na Bwana Yesu - 1 Kor. 15:50-54; 1 Yoh. 3:2; Flp. 3:20-21.

### **Mfano (Kielelezo)**

#### Tumeonywa Na Mifano Ya Uovu.

Malaika waliokosa - 2 Pet. 2:4; Yuda 6.  
 Kaini - Mwa. 4:13-15; 1 Yoh. 3:12; Yuda. 11.  
 Watu wa nyakati za Nuhu - Mwa. 6:5, 6; 2 Pet. 2:5; Luka 17:26, 27.  
 Watu wa Sodoma - Mwa. 13:13; 19:13; 2 Pet. 2:5; Luka 17:28-29.  
 Esau - Ebr. 12:16, 17; Mwa. 25:27-34.  
 Balaamu - 2 Pet. 2:15; Yuda 11; Ufu. 2:14.  
 Nabii wa Yuda - 1 Fal. 13:11-34.  
 Wana wa Israeli - 1 Kor. 10:12; Ebr. 3:15-19; Yuda 5.  
 Dema - 2 Tim. 4:10.  
 Diotrefe - 3 Yoh. 9.  
 Waandishi na Mafarisayo - Mt. 23:1-12.

#### Twatiwa Nguvu Na Mifano Mizuri.

Ibrahimu, kielelezo cha imani - Ebr. 11:8-10; 17-19; Rum. 4:18-23.  
 Ayubu, kielelezo cha uvumilivu - Yak. 5:11; Ayubu 1:20-22; 2:9, 10.  
 Yusufu, kielelezo cha utakatifu na msamaha - Mwa. 39:8-10; 50:15-21.  
 Musa, kielelezo cha upole - Hes. 12:3.  
 Daudi, kielelezo cha kumwabudu Mungu - Zab. 23:24.  
 Danieli, kielelezo cha ujasiri - Dan. 6:7-10, 22.  
 Petro, kielelezo cha ujasiri - Mdo. 4:19-20; 5:29.

Paulo, kielelezo cha kujitolea - Flp. 1:21; 1 Kor. 10:33; 9:19-23; 11:1; 2 Kor. 12:15.  
Yohana, kielelezo cha upendo - 1 Yoh. 3:14-18; 4:17-21.

Yesu Kristo - Kielelezo Cha Mambo Yote:

Uaminifu - Luka 23:46; 1Pet. 2:22-23.  
Uvumilivu - Ebr. 12:1-3; 1 Pet. 2:21.  
Unyenyekevu - Yn. 13:4-17.  
Kusali sana - Marko 1:35; Luka 22:41-44.  
Ujasiri - Luka 9:51; 11:39-52.  
Bidii - Yn. 2:13-17.  
Kujitoa - 2 Kor. 8:9; Flp. 2:7.  
Upendo - Yn. 15:13; 10:11; Gal. 2:20.  
Kusamehe - Luka 23:34; 1 Tim. 1:12-17.

Yesu Kristo Kielelezo Cha Mambo Yote:

Uaminifu - Luka 23:46; 1 Pet. 2:22-23.  
Uvumilivu - Ebr. 12:1-3; 1 Pet. 2:21.  
Unyenyekevu - Yn. 13:4-17; Flp. 2:5-8.  
Kusali sana - Marko 1:35; Luka 22:41-44.  
Ujasiri - Luka 9:51; 11:39-52.  
Bidii - Yn. 2:13-17.  
Kujitoa - 2 Kor. 8:9; Flp. 2:7.  
Upendo - Yn. 15:13; 10:11; Gal. 2:20.  
Kusamehe - Luka 23:34; 1 Tim. 1:12-17.

Wakristo Pia Wanapaswa Kuwa Mifano Mizuri:

Wazee wa Kanisa - 1 Pet. 5:3; Ebr. 13:7; 1 Tim. 3:7.  
Waalimu - 2 Tim. 2:2; Yak. 3:1.  
Wahubiri - 2 Thes. 3:9; 1 Tim. 4:12.  
Wazazi - 2 Tim. 1:5; Efe. 6:4.  
Watumishi - Tito 2:10.  
Wanawake - 1 Pet. 3:1-6.  
Wakristo wote - Mt. 5:13-16; Flp. 2:14-16; 1 Pet. 2:11, 12; 1 Kor. 10:32; Kol. 4:5, 6.

**Mifano Ya Yesu**

Mifano Inayo Husu Ufalme Wa Mungu:

Mbegu ikuayo yenyewe - Mk. 4:26-29.  
Punje ya haradali - Mk. 4:30-32; Mt. 13:31, 32; Lk. 13:18, 19.



Chachu katika mikate - Mt. 13:33; Lk 13: 20, 21.  
Hazina iliyositirika - Mt. 13:44.  
Lulu ya thamani kubwa - Mt. 13: 45, 46.  
Karamu kubwa - Lk. 14:15-24.  
Karamu ya arusi - Mt. 22:1-14.  
Wafanya kazi katika chamba la Mizabibu - Mt. 20:1-16.  
Wana wawili - Mt. 21:28-32.  
Wapangaji waovu - Mt. 21:33-46; Mk. 12:1-12; Lk. 20:9-18.

Mifano Inayo Husu Maisha Ya Haki:

Wajenzi wenye hekima na wapumbavu - Mt. 7:24-27; Lk. 6:46-49.  
Mpanzi - Mt. 13:1-9; Mk. 4:1-9; 14:20; Lk. 8:4-15.  
Wadeni wawili - Lk. 7:36-50.  
Mdeni asiye na huruma - Mt. 18:21-35.  
Msamaria mwema - Lk. 10:25-37.  
Rafiki asiyeacha kuomba - Lk. 11:5-13.  
Mjane shupavu - Lk. 18:1-8.  
Tajiri mpumbavu - Lk. 12:13-21.  
Mtini usiozaa - Lk. 13:1-9.  
Viti vya mbele - Lk. 14:7-11.  
Mnara - Lk. 14:28-30.  
Mfalme mwenye hekima - Lk. 14:31-35.  
Wakili dhalimu - Lk. 16:1-3.  
Farisayo na mtoza ushuru - Lk. 18:9-14.  
Tajiri na Lazaro - Lk. 16:19-31.

Mifano Inayo Husu Pendo La Mungu:

Kondoo Iliyopotea - Lk. 15:1-7; Mt. 18:12-14.  
Shilingi Iliyopotea - Lk. 15:8-10.  
Mwana mpotevu - Lk. 15:11-32.  
Wadeni wawili - Lk. 7:36-50.

Mifano Inayo Husu Hukumu:

Magugu shambani - Mt. 13:24-30, 36-42.  
Juya baharini - Mt. 13:47-50.  
Wanawali kumi - Mt. 25:1-13.  
Talanta - Mt. 25:14-30.  
Mafungu ya fedha - Lk. 19:11-27.  
Kondoo na Mbuzi - Mt. 25:31-46.

## Mimba

### Tunauhai Kabla Ya Kuzaliwa.

Mungu alifahamu Nabii Yeremia tumboni na Mungu alimtakasa tumboni - Yeremia 1:5.

Mungu alifahamu Isaka na Esau tumboni mwa Mama yao - Rum. 9:11.

### Mungu Anaona Mtoto Tumboni Ni Kitu Chenye Uhai.

Kwa mtu ambaye anaharibu mimba Mungu alisema Uhai kwa Uhai - Kut. 21:22-25.

Mungu anaona watoto ambao wanakufa kabla ya kuzaliwa kuwa ni watoto siyo mwili bila roho kama mwanadamu wanavyodai leo - Ayu. 3:16.

## Mitume Walikufa Namna Gani?

Yohana - Alikufa kwa kifo cha kawaida.

Mathayo - Alikufa kwa panga hapa Afrika.

Yakobo, mtoto wa Zebedayo - Walitoa kichwa chake kule Yerusalemu.

Yakobo, mdogo wa Yesu - Alitupwa toka juu ya hekalu na akauawa kwa fimbo.

Filipo - Alinyongwa kwenye mji wa Hieropolis, Phygia kule Asia Ndogo.

Bartholomayo - Alichomwa na moto.

Andrea - Alisulubiwa msalabani.

Tomaso - Aliuawa na mkuki.

Thadayo - Alipigwa na mishale.

Simoni - Alisulubiwa kule Uajemi.

Petro - Alisulubiwa miguu juu.

Mathiya - Alipigwa na mawe halafu wakatoa kichwa.

Paulo - Wakatoa kichwa chake kule Rumi.

Yuda - Alijiua wenyewe.

## Mitume Wapo Leo?

Yesu Aliwachagua Mitume Kumi Na Wawili (Kwa mfano wa Makabila ya Israeli kumi na mbili) - Mat. 10:1-4.

Yuda moja wapo wa wale kumi na wawili alijiua mwenyewe - Mat. 27:3-5.

Kabla ya kanisa mitume kumi na moja walitaka kuchagua mwingine - Mdo. 1:20.

Kabla ya kuchagua mwingine walikuwa na sifa zilizotakiwa kwa yule ambaye alitakiwa kuchukua nafasi ya Yuda - Mdo. 1:21-22.

- 1) Mtu aliyetakiwa kuwepo wakati Yesu alipokuwa pamoja nao - Mdo. 1:21.
- 2) Alitakiwa awe ameuona ubatizo ya Yohana - Mdo. 1:22.
- 3) Alitakiwa kuwa shahidi wa ufufuo - Mdo. 1:22.
- 4) Hakuna mtu leo anazosifa hizi.

## **Miujiza Ya Mungu Kupitia Kwa Watumishi Wake**

### Miujiza Ya Musa Na Haruni:

Fimbo ilibadilika ikawa nyoka - Kut. 4:3.  
Mkono ukawa na ukoma - Kut. 4:6.  
Maji yakabadilika kuwa damu - Kut. 4:9; 7:20.  
Pigo la vyura - Kut. 8:6.  
Pigo la chawa - Kut. 8:16.  
Pigo la inzi - Kut. 8:20-24.  
Pigo la ugonjwa wa tauni kwa mifugo - Kut. 9:3-6.  
Pigo la majipu kwa wanadamu na wanyama - Kut. 9:8-11.  
Pigo la mvua ya mawe - Kut. 9:22-26.  
Pigo la nzige - Kut. 10:12-19.  
Giza nene lililowafanya watu wapapasepapase - Kut. 10:21-23.  
Wazaliwa wa kwanza waliuawa (wanadamu na wanyama) - Kut. 2:29, 30.  
Bahari iligawanyika - Kut. 14:21-25.  
Wamisri walifunikwa na bahari - Kut. 14:26-31.  
Maji machungu yalibadilika kuwa matamu - Kut. 15:22-24.  
Walipata maji mwambani - Kut. 17:3-6.  
Watu waliponywa kwa nyoka wa shaba - Hes. 21:8-9.

### Miujiza Ya Eliya:

Aliizuia mvua kwa maombi yake - I Fal. 17:1; Yak. 5:17.  
Chakula na mafuta ya mjane viliongezeka - I Fal. 17:14-16.  
Alimfufua mtoto kutoka kwa wafu - I Fal. 17:19-23.  
Sadaka ya kuteketezwa iliteketezwa na moto - I Fal. 18:30 - 39.  
Askari waliteketezwa na moto 2 Fal. 1:9, 10.  
Aliomba mvua ikanyesha - I Fal. 18:41-45; Yak. 5:18.  
Aliyapiga maji yakagawanyika - 2 Fal. 2:8.  
Alipanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli - 2 Fal. 2:11, 12.

### Miujiza Ya Elisha:

Aliyapiga maji yakagawanyika - 2 Fal. 2:14.  
Aliyatakasa maji machafu - 2 Fal. 2:19-22.  
Aliyazidisha mafuta ya mjane - 2 Fal. 4:1-7.  
Alimfufua mtoto kutoka kwa wafu - 2 Fal. 4:32-37.  
Alimponya Naamani ugonjwa wa ukoma - 2 Fal. 5:10-14.  
Gehazi aliadhibiwa kwa ukoma - 2 Fal. 5:20--27.  
Chuma cha shoka kilielea majini - 2 Fal. 6:1-7.  
Washami walipigwa kwa upofu - 2 Fal. 6:18.

Aliombea washami wakafumbuliwa macho wakaona - 2 Fal. 6:20.  
Mtu aliyekufa alifufuka - 2 Fal. 13:20, 21.

#### Miujiza Ya Petro:

Alimponya kiwete - Mdo. 3:1-8.  
Aliwaponya wagonjwa na waliopagawa na pepo - Mdo. 5:15, 16.  
Alimponya Ainea - Mdo. 9:32-35.  
Alimfufua Tabitha kutoka kwa wafu - Mdo. 9:36-42.  
Aliyaponya magonjwa ya kila aina - Mdo. 5:15, 16.

#### Miujiza Ya Paulo:

Aliomba Elima mchawi akawa kipofu - Mdo 13:9-12.  
Alimponya mtu aliyekuwa kiwete tangu tumboni mwa mamaye - Mdo. 14:8-10.  
Alimponya kijakazi aliyekuwa na pepo wa uaguzi - Mdo. 16:16-18.  
Alimponya Eutiko kwa kumfufua kutoka kwa wafu - Mdo. 20:8-12.  
Alipoumwa na nyoka hukupata madhara yo yote - Mdo. 28:3-6.  
Alimponya babaye Publio - Mdo. 28:7,8.  
Aliyaponya magonjwa ya kila aina - Mdo. 28:9; 19:11, 12; 14:3.

### **Moyo**

#### Kazi Ya Moyo:

Kinywa cha mtu huyanena yaujazyoyo moyo wake - Mt. 12:3-4, Luka 6:45.  
Mawazo mabaya hutoka moyoni - Mk. 7:21-23.  
Hufikiri mioyoni mwao - Mk. 2:8.  
Hukusudia mioyoni mwao - Lk. 21:14; Mdo 11:23; 2 Kor. 9:7.  
Wana mioyo mizito - Lk. 24:25.  
Hufadhaika mioyoni mwao - Yn. 14:1.  
Neno la Mungu hupandwa mioyoni - Lk. 8:11, 12.  
Huchomwa mioyoni mwao kwa sababu ya huzuni - Mdo. 2:37.  
Huchomwa mioyoni kwa sababu ya ghadhabu - Mdo. 5:33; 7:54.  
Kristo huishi mioyoni mwao kwa sababu ya imani katika Kristo - Efe. 3:17.  
Hazina yako ilipo, ndipo na moyo wako ulipo - Mt. 6:21; Lk. 12:34.

#### Tabia Za Moyo Mbaya:

Moyo uwazao mawazo mabaya - Mit. 6:18.  
Moyo mkaidi - Mit. 11:20.  
Moyo ujaa maovu - Mhubiri 9:3.  
Moyo unaothibitishwa kutenda maovu - Mhu. 8:11.

Moyo huwa mdanganiyifu kuliko vitu vyote - Yer. 17:9.  
Moyo ukaao mbali na Mungu - Isa. 29:13; Mt. 15:8.  
Hukuukaza moyo wake amtafute Mungu - 2 Mambo ya Nyakati 12:14.  
Mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza - Rum. 1:21.  
Hufanya makosa moyoni - Zab. 95:10.  
Moyo wa kumwacha Mungu - Kum. 29:18; Yer. 17:5.  
Moyo usio na toba - Rum. 2:5.  
Moyo mbovu wa kutokuamini - Ebr. 3:12.  
Ugumu wa moyo - Efe. 4:18.  
Moyo usiotahiriwa - Law. 26:41; Mdo. 7:51.  
Moyo uliodanganyika - Isa. 44:20; Yak. 1:26.  
Moyo uliogawanyika - Hos. 10:2.  
Moyo mgumu - Eze. 3:7; Marko 10:5.  
Moyo wenye majivuno - Mit. 18:12; Yer. 48:29.  
Moyo wa kutamani - Yer. 22:17; 2 Pet. 2:14.  
Moyo mpumbavu - Mit. 12:23.  
Moyo ununao juu ya Mungu - Mit. 19:3.  
Moyo wa kuasi na ukaidi - Yer. 5:23.  
Moyo wa jiwe - Eze. 36:26; 11:19.  
Uzinzi wa moyoni - Mt. 5:28.

#### Tabia Za Moyo Mwema:

Moyo uliokazwa kumtafuta Bwana - 2 Mambo ya Nyakati 19:3.  
Moyo uliyo imara katika kumtumaini Bwana - Zab. 112:7.  
Moyo safi - Zab. 24:4; Mt. 5:8.  
Moyo uliyo mnyofu na mwema - Lk. 8:15.  
Moyo uliyovunjika - Zab. 34:7; 51:17.  
Moyo mtiifu - Rum. 6:17.  
Moyo uliojawa na neno la Mungu - Zab. 119:11.  
Moyo uliotahiriwa - Kum. 30:6; Rum. 2:29.  
Moyo unaomtamani Bwana - Zab. 84:2; 27:8.  
Moyo mwaminifu - Neh. 9:8.  
Moyo mpole na mnyenyekevu - Mt. 11:29.

#### Mungu:

Huijaribu mioyo - 1 Mambo ya Nyakati 29:17; Yer. 12:3; Ufu. 2:23.  
Huzijua siri za moyo - Zab. 4:21; Yer. 20:12; Ebr. 4:12; Lk. 16:15.  
Huitafuta mioyo - Rum. 8:27.  
Huutazama moyo - I Sam. 16:7.  
Huufungua moyo - Mdo. 16:14.  
Hutoa moyo mpya - Eze. 36:26; 18:31.

Hung'aa moyoni - 2 Kor. 4:6.  
Huutia moyo nguvu - Zab. 27:14.  
Huufanya moyo imara - I The. 3:13.  
Hutuma Roho Mtakatifu aingie mioyoni mwa watoto wake - Gal. 4:6.

Wanadamu Wanapaswa :

Kuitengeneza mioyo yao kwa Mungu - I Sam. 7:3.  
Kumpa Mungu mioyo yao - Mit. 23:26.  
Kuielekeza mioyo yao wapate kufahamu - Mit. 2:2.  
Kuiongoza mioyo yao - Mit. 23:19.  
Kuamini mioyoni mwao - Rum. 10:9.  
Kumtumikia na mioyo yao yote - Kum. 11:13.  
Kuisafisha mioyo yao - Yak. 4:8.  
Kuwa na moyo wa huruma - Efe. 4:32.  
Kuulinda moyo kuliko vitu vyote - Mit. 4:32.  
Kuenenda katika kweli mbele za Mungu kwa moyo wao wote - I Fal. 2:4.

**Msalaba Wa Kristo**

Kifo Msalabani Kilidharauliwa Na Watu:

Kwa Wayunani kilikuwa ni aibu - I Kor. 1:23.  
Kwa Wayahudi kilikuwa ni kikwazo - I Kor. 1:23; Kum. 21:23; Gal. 3:13; I Pet. 2:8.

Yesu Aliuvumili a Msalaba Kwa Ajili Yetu:

Aliutoa uhai wake kabisa - Yn. 10:18.  
Alifanywa laana kwa ajili yetu - Gal. 3:13.  
Aliustahimili msalaba kwa ajili ya furahi iliyowekwa mbele yake - Ebr. 2:12.

Neno La Msalaba Ni Nguvu Inayokoa Watu:

Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu ili tuokolewe - 1 Kor. 15:1-4.  
Maneno yanayoonekana kama upuzi, ni maneno ya Mungu yanayowaokoa wenye dhambi - 1 Kor. 1:18; 1:23-24.

Utukufu Wetu Uko Katika Msalaba Wa Yesu:

Tunapaswa tusijue neno lo lote ila Yesu Kristo naye amesulubiwa - 1 Kor. 2:2.  
Tunahitaji kuona fahari juu ya msalaba wa Yesu Bwana wetu - Gal. 6:14.

**Msamaha**

Mungu Ni Mungu Yuko Tayari Kuwasamehe Wenye Dhambi Watubuo Kweli Kweli - Neh. 9:17; Kut. 34:6-7.

Msamaha wa Mungu ni mkamilifu:

- 1) Huziweka dhambi zetu mbali nasi - Zab. 103:12.
- 2) Huzifuta kabisa dhambi zetu - Isa. 43:25; Mdo. 3:19.
- 3) Huzitupa dhambi zetu zote katika vilindi vya bahari - Mika 7:19.
- 4) Hutusamehe maovu yetu yote - Zab. 103:3; makosa yote - Kol. 2:3; dhambi zote na udhalimu wote - 1 Yoh. 1:9.
- 5) Hazikumbuki dhambi kamwe - Isa. 43:45; Yer. 31:34; Ebr. 8:12.

Je! Watu husamehewa kwa njia gani?

- 1) Wenye dhambi ambao hawajawa Wakristo: Wanapaswa kumwamini Yesu Kristo - Mdo. 10:43. Wanapaswa kutubu (kuacha) dhambi - Mdo. 2:38; 3:19. Wanapaswa kumkiri Kristo ya kuwa ni Bwana - Rum. 10:9, 10. Wanapaswa kubatizwa katika Kristo - Mdo. 2:38; 22:16. Hivyo, wameoshwa katika damu ya Kristo na dhambi zao zimesamehewa - Efe. 1:7; Kol. 1:14.
- 2) Wakristo watendapo dhambi:
  - a) Wanapaswa kutubu - Mdo. 8:22.
  - b) Wanapaswa kuziungama dhambi zao - 1 Yoh. 1:9.
  - c) Wanapaswa kuenenda nuruni kuliko kuenenda gizani - 1 Yoh. 1:5-7.
  - d) Hivyo, nao pia wamesamehewa kwa njia ya damu ya Kristo, na mioyo yao kutakaswa kwa njia ya neema ya Mungu.

Wakristo Pia Wanapaswa Kuwasamehe Wengine:

Sababu za kuwasamehe wengine:

- 1) Kwa sababu ya huruma za Mungu.
- 2) Ili kwamba nasi tuweze kusamehewa - Mk. 11:25; Mt. 6:14, 15.
- 3) Kwa kuwa hayo ni mapenzi ya Mungu - Efe. 4:32; Kol. 3:13; Mt. 18:21-35.
- 4) Hivyo ni kufuata mifano ya Kristo - Luka 23:34.
- 5) Ni fahari ya mtu - Mit. 19:11.

Msamaha unapaswa kuwa:

- 1) Na kuchukulinana - Kol. 3:13.
- 2) Na huruma - Mwa. 45:5-11; Rum. 12:20.
- 3) Na upendo pamoja na maombi - Mt. 5:44.
- 4) Kila mara - Mt. 18:22; Luka 17:4.
- 5) Sehemu ya maombi (yaani uwe pamoja na maombi) Marko 11:25.

Mifano ya msamaha:

Yusufu - Mwa. 50:20,21

Stefano - Mdo 7:60

Paulo - 2 Tim. 4:16.

Baba ya mwana mpotevu - Luka 15:11-32.

## **Mtumishi (Mhudumu)**

### Mtumishi Ni Mtu Amtumikiaye Mwingine Na Kufanya Mapenzi Yake:

Watumishi wa mfalme - Mt. 22:13.

Watumishi wa karamu - Yn. 2:5.

Waisraeli walikuwa watumishi wa Mungu - Isa. 41:8; 43:10.

Manabii wa Mungu walikuwa watumishi wake - 2 Fal. 7:19; 21:10; Yer. 29:19.

Wahudumu (watumishi) wa agano jipya - 2 Kor. 3:6.

Watumishi wa haki - 2 Kor. 11:15.

Mhudumu wa Injili - Efe. 3:7; Kol. 1:23.

Watumishi wa Shetani - 2 Kor. 11:14, 15.

### Yesu Kristo Alikuwa Mtumishi:

Alijinyenyekeza mwenyewe ili kwamba awe mtumishi - Lk. 22:27; Yn. 13:5.

Mhudumu wa agano la kutahiriwa - Rum. 15:8.

Mtumishi wa Mungu - Isa. 42:1; Mt. 12:18; Isa. 52:13; 53:11; Mdo. 8:32-35.

### Huduma Kanisani:

Mhudumu wa Kanisa - Kol. 1:24, 25.

Watumishi wa Mungu - 2 Kor. 6:4; 1 The. 3:2.

Watumishi wa mitume - Mdo. 13:5; 19:22.

Wakristo wote ni watumishi wa Mungu na Kristo - Yn. 12:26; Kol. 3:24; 1 The. 1:9; Ebr. 12:28; Ufu. 7:15.

Lakini kanisani kuna baadhi ya wanaoteuliwa kuwa watumishi maalum ikiwa wanazo sifa zitakiwazo - Flp. 1:1; 1 Tim. 3:8-13. Tafadhali kumbuka Mdo. 6:1-6.

Fibi, mtumishi wa kike wa kanisa - Rum. 16:1.

Atafutaye kuwa mkubwa anapaswa kuwa mtumishi wa wote - Mt. 20:26.

### Wafalme Wa Dunia Ni Watumishi Wa Mungu:

Koreshi, mfalme wa Uajemi - Isa. 45:1-6; 2 Nya. 36:22, 23; Ezra 1:1-4.

Nebukadreza, mfalme wa Babeli - Yer. 25:9; 27:6; 43:10.

Daudi - 2 Sam. 3:18; 1 Fal. 3:6.

Watumishi wa serikali - Rum. 13:4.

### Wajibu Wa Watumishi Kwa Bwana Zao.

Kuwaheshimu - Malaki 1:16.

Kuwatii - 1 Pet. 2:18.

Wawe waaminifu - Lk. 16:10-12; 1 Kor. 4:2.



### Mifano Wa Watumishi Waaminifu:

Yusufu - Mwa. 39:3, 4; Mdo 7:10.  
Musa - Ebr. 3:5; Hes. 12:7.  
Kalebu - Hes. 14:24.  
Ayubu - Ayu. 1:8; 2:3.  
Samweli - I Sam. 3:9, 10.  
Watumishi wa akida wa Kapernaumu - Mt. 8:9.  
Watumishi wa Kornelio - Mdo. 10:7.

### **Mungu Baba**

Watu wa duniani wanaweza kujua kwamba Mungu yupo kwa kuona muumbo wake - Rum. 1:19-23; Zab. 19:1-4. Walakini hawawezi kuijua tabia yake au mapenzi yake bila ufunuo wake upatikanao katika Biblia Takatifu. Mungu amejifunua mwenyewe katika maandiko ya manabii na hasa kwa njia ya Mwanawe Yesu Kristo - Ebr. 1:1-3; Yn. 14:9.

### Tabia Za Mungu:

#### 1. Mungu ni wa milele:

Zab. 102:24-27.	Yer. 10:10.
Zab. 90:1-4	1 Tim. 1:17.
Kutoka 3:13,14.	Ufu. 1:8.
Isa. 57:15.	Ufu. 4:8,9

#### 2. Mungu ni muumba wa vitu vyote:

Mwa. 1:1.	Mdo. 17:24.
Neh. 9:6.	Ebr. 11:3.
Zab. 8:3.	1 Pet. 4:19.
Mhubiri 12:1	Ufu. 4:11.

#### 3. Mungu anajua kila kitu:

Ayubu 37:16.	1 Mambo ya Nyakati 28:9.
Zab. 147:4,5.	Mt. 10:29, 30.
Zab. 139: 2-4.	Rum. 11:33-36.

#### 4. Mungu yuko mahali pote:

Yer. 23:23,24.	Ebr. 4:13.
Yer. 16:17.	Mdo. 17:28, 29.
Zab. 139:8-12,23,24.	

#### 5. Mungu ndiye mwenye uwezo wote:

Mwa. 1:3, 11.  
Zab. 33:8, 9.  
Yer. 23:17  
Isa. 40:21-31.

Mt. 19:26.  
Ufu. 11:17.  
Ebr. 13:5,6.

6. Mungu habadiliki:

Malaki 3:6.  
1 Sam. 15:29.

Hes. 23:19.  
Yak. 1:17.

7. Mungu ni mwaminifu:

Kum. 7:6.  
Zab. 100:5  
1 Kor. 1:9; 10:13.  
1 The. 5:23, 24.  
2 The. 3:3.  
Ebr. 10:23; 6:17,18.

1 Yoh. 1:9.  
Rum. 3:3-5.  
Tito 1:2.  
2 Tim. 2:11-13.  
1 Pet. 4:19.

8. Mungu ni mwenye wivu:

Kutoka 20:5; 34:14.  
Yoshua 24:19.  
Kum. 4:24

Ebr. 10:31; 12:29.  
Mt. 6: 33.  
Kol. 3:1, 2.

9. Mungu ndiye aitafutaye mioyo:

1 Mambo ya Nyakati 28:9.  
1 Fal. 8:39.  
1 Sam. 16:7.  
Mdo. 1:24.

Rom. 8:27.  
Luka 16:15.  
Ufu. 2:23.

10. Mungu hana upendeleo:

Kum. 10:17.  
2 Nya. 19:7  
Mdo. 10:34, 35.  
Rum. 2:11.

Gal. 2:6.  
Efe. 6:9.  
Kol. 3:25.  
1 Pet. 1:17.

11. Mungu ni mwenye rehema:

Kum. 10:17.  
Kutoka 34:6.  
Zab. 145:8, 9.  
Mt. 5:45.

Luka 6:36.  
Rum. 2:4.  
Tito 3: 4, 5.  
Luka 15:11 -24.

12. Mungu ni mtakatifu:

Isa. 6:3.  
Ufu. 4:8.

1 Yoh. 1:5.  
Law. 11: 45.

Yak. 1:13.                                      1 Pet. 1:15, 16.

13. Mungu ni upendo:

1 Yoh. 4:7, 8, 19.                              Rum. 5:8.

Efe. 2:4-7.                                      Yn. 3:16.

Ebr. 12: 6, 7.                                      1 Yoh. 3:1.

Waandishi Wa Agano Jipya Walifundisha Umoja Wa Mungu Jinsi Unavyoelezwa Katika Agano La Kale Na Pia Walifundisha Kwamba Mungu ni “Baba Na Mwana Na Roho Mtakatifu.”

Kweli hiyo ilifunuliwa hasa wakati wa kuja kwake Yesu Kristo na Roho Mtakatifu. Walithibitisha kwamba wako watatu katika mmoja. Nafsi watatu asili moja.

Maandiko yanayothibitisha ukweli huo.

- 1) Mt. 1:18-23; Lk. 1:35.
- 2) Mt. 3:16-17; Marko 1:9-11; Yn. 1:32-34.
- 3) Yn. 14:7-23.
- 4) Yn. 6:5-15.
- 5) Mt. 28:19.
- 6) Efe. 2:18; 3:2-5, 14, 17; 4:4-6; 5:18-20.
- 7) 1 Kor. 12:4-6.
- 8) 2 Kor. 13:14.
- 9) Ebr. 2:3-4; 6:4-6; 10:29-31.
- 10) 1 Pet. 1:2; 4:13-19.
- 11) 1 Yoh. 5:3-8.
- 12) Yuda 20, 21.
- 13) Ufu. 1:4-6.

Yesu Kristo Alimdhahirisha Mungu Kwa Ukamilifu:

Yesu alitwa Imanueli, “tafsiri yake ni, Mungu pamoja nasi” - Mt. 1:23.

1. Neno alikuwako kwa Mungu hapo mwanzo, (naye, “alikuwa Mungu,”) akafanyika mwili na akamfunua Baba - Yn. 1:1, 2, 14, 18.
2. Mwana humfunua Baba - Mt. 11:25-27.
3. Aliyemwona Mwana amemwona Baba pia - Yn. 14:7-11.
4. “Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana” - Kol. 1:15.
5. Yeye ni mng’ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake - Ebr. 1:3.

Tunamwonaje Mungu Katika Kristo?

1. Yesu alionyesha kwamba Mungu huwapenda wenye dhambi na anataka waokolewe - Marko 2:15-17; Mt. 23:37; Luka 23:34.
2. Yesu alionyesha kwamba Mungu huwatafuta wenye dhambi na anataka waokolewe - Luka 19:10; Yn. 9:35; Rum. 8:32; 1 Yoh. 4:10.

3. Yesu alionyesha kwamba Mungu humpenda kila mtu na hufurahi mmoja atubupo - Luka 15:1-32.

### **Umoja wa Mungu (Baba, Mwana, Roho).**

#### Wakati Wa Uumbaji.

Mwa. 1:1 - Hapo mwanzo Mungu aliumba.

Mwa. 1:2 - Roho wa Mungu akatulia juu ya uso wa maji.

Yn. 1:1, 7, 14 - Neno ambalo ni Yesu, Alikuwa mwanzo na alikuwa Mungu.

1 Kor. 8:6 - Vitu vyote kwa Baba na Yesu.

#### Agano Jipya Lataja Umoja Wa Watatu.

Mt. 3:13-17 - Yesu akiwa amebatizwa, Roho Mtakatifu alishuka kama hua na Baba asema, angalia pia Mk. 1:9-11.

Mt. 28:18-20 - Kubatizwa katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Yn. 14:25-26 - Yesu anaongea juu ya Baba kutuma Roho ya Kweli.

Yn. 15:26 - Yesu akizungumza juu ya umoja wa Yeye na Baba yake.

Yn. 17:11 - Yesu akizungumza juu ya Baba kumtuma Roho ya Kweli.

Mdo. 7:55-59 - Kabla ya kifo cha Stefano, akiwa amejaa Roho Mtakatifu alitazama juu na kumwona Yesu na Mungu wakiwa wamekaa juu ya kiti cha enzi.

2 Kor. 13:14 - Paulo akiuliza (akiomba)kuhusu neema ya Yesu, upendo wa Muingu na ushirika wa Roho Mtakatifu uwe na Wakorintho.

1 Tim. 5:8 - Wako watatu wanaoshuhudia mbinguni: Baba, Neno na Roho Mtakatifu, hawa watatu ni umoja.

### **Mwenendo Wa Maisha (Tabia - Desturi).**

#### Wakristo Wanapaswa Kuenenda Inavyostahili Wito Wao - Efe 4:1.

Ulivyo wajibu wao kwa Mungu - 1 The. 2:12.

Ulivyo wajibu wao kwa Bwana - Kol. 1:10.

Katika Roho - Gal. 5:16, 25; Rum. 8:4.

Mwenendo wa utakatifu - Tito 2:3.

Inavyoipasa Injili - Flp. 1:27.

Katika upya wa uzima - Rum. 6:4; 2 Kor. 5:17.

Katika kweli - 2 Yoh.. 4; 3 Yoh. 4.

Katika Bwana - Kol. 2:6.

Kwa kumpendeza Mungu - 1 The. 4:1.

Kwa imani - 2 Kor. 5:7.

#### Kuenenda Katika Upendo - Efe. 5:2:

Kuenenda katika upendo mtu na mwenzake - Rum. 14:15.  
Kuenenda kwa hekima mbele yao walio nje - Kol. 4:5; Efe. 5:15.  
Kuenenda kwa adabu mbele yao walio nje - 1 The. 4:12; 1 Pet. 2:12.  
Kuenenda katika matendo mema - Efe. 2:10.  
Pamoja na roho ya upole na utulivu - 1 Pet. 3:4.  
Ili kwamba tuwe kielelezo kwa wengine - 2 Tim. 3:10; 1 Tim. 4:12.  
Kuenenda jinsi Yesu alivyoenenda - 1 Yoh. 2:6.

Kama Watoto Wa Nuru - Efe. 5:8.

Kuenenda pamoja na Mungu - Mwa. 5:24; 6:9.  
Katika njia zake zote - YOSHUA 22:5.  
Katika nuru ya Mungu - Isa. 2:5.  
Katika nuru ya uso wa Bwana - Zab. 89:15.  
Kwa kujinyenyekesha mbele za Mungu - Mika 6:8.  
Kwa kuzifuata amri zake - 2 Yoh. 6.  
Katika nuru - 1 Yoh. 1:7.  
Iliyohusika na mchana - Rum. 13:13.  
Mwenendo safi na wa hofu - 1 Pet. 3:2; 1:15.  
Katika maisha ya utakatifu na utauwa - 2 Pet. 3:11.  
Kama watu waifuatao haki - 1 Pet. 2:24.  
Kiasi, haki na utauwa - Tito 2:12.

Hawapaswi Kuenenda Kama Mataifa Waenendavyo - Efe. 4:17.

Katika shauri la wasio haki - Zab. 1:1.  
Katika makosa na dhambi - Efe. 2:1, 2.  
Katika ufisadi, na tamaa, na ulevi - 1 Pet. 4:3.  
Katika uasherati na tamaa za upotevu - Rum. 13:13; Yuda 18.  
Kwa kufuata mambo ya mwili - Rum. 8:4; 13:14.  
Katika ugomvi na wivu - Rum. 13:13.  
Ushirika mbaya - 1 Kor. 15:33.  
Katika giza - Yn. 8:12; 1 Yoh. 1:6.  
Kwa kutakabari (kujivuna) - Dan. 4:37.  
Kama watoto wasiotii - 1 Pet. 1:14.  
Bila utaratibu - 2 The. 3:6, 11.  
Kwa hila - 2 Kor. 4:2.  
“Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda,” - Efe. 5:15.

Mkristo Hapaswi Kufuata Mapokeo Na Mila Zinazopinga Mafundisho Ya Kristo.

Mkristo hujitoa kabisa kwa Mungu - Mt. 6:24; 22:37; Rum. 12:1-2.

Mkristo anapaswa kuwa kiumbe kipya - Rum. 12:1.  
Asifuatishe namna ya dunia hii - Rum. 12:1, 2.  
Wakristo wanapaswa kuyaacha mafundisho ya awali ya ulimwengu - Gal. 4:8-11.  
Tumekufa pamoja na Kristo ili tuyaache mafundisho na hekima za dini za ulimwengu huu - Kol. 2:20-23.  
Kuyarudia mafundisho au mapokeo ya wanadamu ni hatari - Ebr. 6:4-6; 2 Pet. 2:20-22.  
Kuyafuata mapokeo ya dini za wanadamu (kimila) ni kuzini juu ya Mungu na kuyatumikia mashetani - Yer. 3:1, 6, 9; 1 Kor. 10:20-22.  
Paulo alijisifia Bwana kuliko urithi wa kabila lake - Flp. 3:4-11.

## **Mwili**

### Mwili Uwezo Ukawa Chombo Kisicho Haki:

Mwili wa dhambi - Rum. 6:6.  
Mwili wa mauti - Rum. 6:12.  
Mwili uliokufa kwa sababu ya dhambi - Rum. 8:10.  
Wasio na Mungu huvunjiana heshima ya miili yao wenyewe - Rum. 1:24.  
Afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe - 1 Kor. 6:18.  
Matendo ya kimwili humtenganisha mwanadamu na Mungu - Gal. 5:19-21.  
Matendo ya kimwili lazima yafishwe - Rum. 8:12-13; Gal. 5:24.  
Mwili unapaswa kumtii Bwana - 1 Kor. 9:27.  
Mwili waweza kutupwa Jehanum - Mt. 5:29.

### Lakini Mwili Unaweza Tena Kuwa Chombo Chenye Haki:

Mwili si kwa zinaa, bali ni kwa Bwana - 1 Kor. 6:13.  
Mkristo humtukuza Mungu katika mwili wake - 1 Kor. 6:20.  
Kristo huadhimishwa katika miili ya watu wake - Flp. 1:20.  
Mwili hutolewa kama dhabihu iliyo hai - Rum. 12:1.  
Mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu - 1 Kor. 6:19.  
Mwili utakombolewa - Rum. 8:23.  
Mwili wa Mkristo utabadilishwa - Flp. 3:20-21; 1 Yoh. 3:2.  
Mkristo hapaswi kusumbukia mahitaji ya mwili - Luka 12:22.  
Mkristo huupamba moyo kuliko mwili - 1 Pet. 3:3-4.

### Yesu Na Mwili Wake:

Kristo aliuchukua mwili wa mwanadamu na akafanana na mwanadamu katika mambo yote - Yn. 1:14; Ebr. 2:14-18; 4:15.  
Aliweza kusikia njaa, kiu na maumivu - Luka 4:2; Yn. 19:28; 1 Pet. 2:21; 3:18; 4:1.  
Aliutoa mwili wake ili amtakase wanadamu - Ebr. 10:10.  
Alizichukua dhambi zetu katika mwili wake - 1 Pet. 2:24.  
Mwili wake ulizikwa - Mt. 27:58-60; Marko 15:46.

Mwili wake ulifufuliwa kutoka kwa wafu - Mdo. 2:31-32; Luka 24:39.

Katika Chakula cha Bwana, mkate ni mfano wa mwili wake - Mk. 14:22; Luka 22:19; Mt. 26:26; 1 Kor 11:24; 10:16.

Ye yote alaye Chakula cha Bwana kwa njia isiyofaa atakuwa amejipatia hatia ya mwili wa Bwana - 1 Kor. 11:27.

#### Kanisa La Bwana Ndilo Mwili Wa Kristo:

Kanisa limefananishwa na mwili - Rum. 12:4-5; 1 Kor. 12:12.

Kanisa ndilo mwili wa Kristo - Efe. 1:22-23; Kol. 1:18.

Tuliitwa katika mwili mmoja - Kol. 3:15.

Tulibatizwa ili kwamba tuingie katika mwili mmoja - 1 Kor. 12:13; Rum. 6:3-4.

Kristo ndiye Mwokozi wa mwili - Efe. 5:23; Mdo. 20:28.

Wenye dhambi hupata kushirikiana na Mungu katika mwili wa Kristo - Efe. 2:26.

### **Mwito**

#### Mungu Huita Kwa Njia Gani?

Kufuatana na kusudi lake - Rum. 8:28.

Kufuatana na neema yake - 2 Tim. 1:9.

Katika Kristo nguvu ya Mungu - 1 Kor. 1:24.

Kwa njia ya Injili - 2 The. 2:4.

Roho na Bibi - Arusi wasema, "Njoo!" - Ufu. 22:17.

#### Asili Ya Mwito Wetu Ni Nini?

Si kufuatana na hekima ya wanadamu - 1 Kor. 1:26.

Mwito mkuu wa Mungu - Flp. 3:14.

Mwito mtakatifu - 2 Tim. 1:9.

Katika amani - 1 Kor. 7:15.

Wengine huukataa mwito wao - Mt. 22:3-6.

Waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache - Mt. 22:14.

Tunapaswa kuufanya imara mwito wetu - 2 Pet. 1:10.

#### Kwa Nini Tunaitwa?

Ili tuingie katika nuru - 1 Pet. 2:9.

Ili tuwe wateule wa Yesu - Rum. 1:6.

Ili tuingie katika ushirika wa Kristo - 1 Kor. 1:9.

Tuwe katika utakaso - 1 The. 4:7.

Tupate kuwa huru - Gal. 5:13.

Kwa utukufu na wema wake - 2 Pet. 1:3.

Tuingie katika uzima wa milele - 1 Tim. 6:12.  
Tuwe na tumaini moja - Efe. 4:4.  
Tuingie katika karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo - Ufu. 19:9.  
Tuenende kama unavyostahili, katika maisha mema - Efe. 4:1.  
Kupata mateso - 1 Pet. 2:20, 21.  
Tufuate mfano wa Kristo - 1 Pet. 2:21.

### **Nani Alijenga Kanisa?**

#### Yesu Kristo Mwana Wa Mungu Pamoja Na:

Nitalijenga kanisa langu - Mt. 16:18.  
Tulijengwa juu ya mitume, manabii na Yesu Kristo - Efe. 2:20.  
Majina ya mitume - Ufu. 21:14.

### **Ndoa**

#### Ndoa Ilianzishwa Na Mungu:

Mungu hakutaka mwanamume aishi peke yake - Mwa. 2:18.  
Alimuumba mwanamke awee msaidizi wa mwanamume - Mwa 2:18-22.  
Ndoa ya kwanza ilianzishwa na Mungu - Mwa. 2:23, 24; Mt. 19:5, 6.  
Mungu ni shahidi wa ndoa - Malaki 2:14.  
Ndoa iheshimiwe na wote - Ebr. 13:4.  
Ni njia ya kuzuia zinaa - 1 Kor. 7:1-5.  
Ni njia ya kuzuia tamaa mbaya - 1 Kor. 7:7-9.  
Kilichounganishwa na Mungu, mwanadamu asikitenganishe - Mt. 19:6.

#### Dhambi Katika Ndoa - - Kuwa Na Wanawake Zaidi Ya Mke Mmoja:

Hapo mwanzo mungu alimpa Adamu mke mmoja - Mwa. 1:27, 28; 2:22, 23.  
Mungu aliona kwamba hawa wawili wawe mwili mmoja - Mwa. 2:24; Mt. 19:4, 5.  
Kuo wake wengi kulianzishwa na ukoo mbovu wa Kaini - Mwa. 4:19.  
Ingawaje baadhi ya wanaume wa Agano la Kale walikuwa na wake wengi, waliona taabu nyingi kwa kufanya hivyo:

- 1) Ibrahimu - Mwa. 16:4-6; 21:9, 10.
- 2) Daudi - 2 Sam. 13:1-38; 2 Sam. 15:18.
- 3) Sulemani - 1 Fal. 11:1-8.

Yesu Kristo aliikataa tabia hii ya kuo wake wengi, alifundisha kwamba ndoa inapaswa kuwa jinsi ilivyokuwa hapo mwanzo ilipoanzishwa na Mungu - Mt. 19:4, 5.  
Roho Mtakatifu alifundisha kwamba kila mwanamume anapaswa kuwa na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke anapaswa kuwa na mume wake mwenyewe - 1 Kor. 7:1-3.  
Yeyote atakayeoa mke mwingine, au atakayeolewa na mwanamume mwingine wakati mke au mume wake



bado yu hai, azini - Rum. 7:2, 3.

Utukufu wa mwanamke wa Kikristo hauruhusu ndoa ya wake wengi - 1 Pet. 3:7; Mt. 7:12.

Mtu aliye na wake zaidi ya mmoja hawezi kuwa mzee, au msaidizi wa kanisa - 1 Tim. 3:2, 12.

### Dhambi Katika Ndoa---Kutengana Au Talaka:

Wale waoao, au waolewao bila kufanya dhambi ni:

- 1) Wale ambao hawajawahi kuo au kuolewa - 1 Kor. 7:9; Mwa. 12:18.
- 2) Wale ambao walioa, au waliolewa, lakini mkewe au mumewe akafa - Rum. 7:2, 3.
- 3) Wale waliooa au waliolewa, lakini wameachana na wenzao kwa sababu ya uasherati - Mt. 19:9.

**KUMBUKA:** Tunapaswa kujua kwamba wakati mwingine mume au mke humsababisha mwenzake atende dhambi kwa sababu ya kukosa kutimiza wajibu wake kwa mwenzake - Efe. 5:22, 23; 1 Kor. 7:1-5. Mfano: Waume waendao nchi za mbali na kuwaacha wake zao kwa muda mrefu.

Wale watendao dhambi wanapooa au wanapolewa ni:

- 1) Wale wenye mume au mke aliye hai na hawajaachana kwa sababu ya uasherati - Mt. 19:9; Rum. 7:2,3.
2. Wale waoao au waolewao na aliyeachwa, lakini sio kwa sababu ya uasherati - Mt. 5:32.

### Wajibu Wa Nyumba Ya Kikristo:

Wajibu wa mume kwa mkewe:

- 1) Anapaswa kumpenda mkewe kama mwili wake mwenyewe - Efe. 5:25-29.
- 2) Anapaswa kumfurahia mkewe - Mit. 5:18.
- 3) Anapaswa kumpendeza mkewe na kumtunza kama Kristo alitunzavyo kanisa - Efe. 5:27; 1 Kor. 7:33.
- 4) Hapaswi kuwa na uchungu kwa mkewe - Kol. 3:19.
- 5) Anapaswa kumtunza kama “chombo kisicho na nguvu,” Kumpa mke heshima, na kumsaidia katika maisha ya Kikristo “kama warithi pamoja wa neema ya uzima” - 1 Pet. 3:7.
- 6) Anapaswa kuwatumza walio wake - 1 Tim. 5:8.
- 7) Anapaswa kujua kwamba, “hana amri juu mwili wake, bali mkewe” - 1 Kor. 7:4.

Wajibu wa mke kwa mume wake:

- 1) Anapaswa kumtii mumewe - Mwa. 3:16; Kol. 3:18; Efe. 5:22-24.
- 2) Anapaswa kumheshimu - 1 Kor. 11:3; Efe. 5:33.
- 3) Anapaswa kufanya kazi pamoja naye – Tit. 2:5.
- 4) Anapaswa kujua kwamba “hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe” - 1 Kor. 7:1-5.
- 5) Anapaswa kumpendeza mumewe - 1 Kor. 7:34.

Wajibu wa Wazazi kwa Watoto wao:

- 1) Hawapaswi kuwachokoza watoto wao Efe. 6:4.
- 2) Hawapaswi kuwachokoza, wasije wakakata tamaa - Kol. 3:21.

- 3) Wanapaswa kuwalea kwa adabu na maonyo ya Bwana - Efe. 6:4.
- 4) Wanapaswa kuonyesha mifano mizuri - 2 Tim. 1:5; Flp. 2:14-16.
- 5) Wanapaswa kuwafundisha njia ya kweli - Mit. 22:6; Kum. 6:7; 2 Tim. 3:15; Mt. 28:19,20.

Wajibu wa Watoto kwa Wazizi wao:

- 1) Wanapaswa kuwatii - Kol. 3:20; Efe. 6:1; Lk. 2:51, 52.
- 2) Wanapaswa kufuata maagizo yao - Mit. 6:20-23; 1 Tim. 3:4. Tafadhali kumbuka Warumi 1:30; 2 Tim. 3:2.
- 3) Wanapaswa kuwaheshimu na kuwsaidia - Efe. 6:2, 3; Mk. 7:10-13.

### **Ndoto**

Katika Agano la Kale na Jipya baadhi ya ndoto zilitoko kwa Mungu.

“Mungu akamwambia (Ibrahimu) katika ndoto . . .” - Mwa. 20:6.  
 “. . . Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu.” Mwa. 41:25.  
 “. . . malaika wa Bwana alimtokea (Yusufu) katika ndoto - Mt. 1:20; 2:13, 19.  
 Mungu aliwaonya mamajusi katika ndoto - Mt. 2:12.  
 Tafsiri ya ndoto, au maagizo ndani yake yalitoka kwa Mungu na wala si yule aliyeota - Mwa. 40:8; Dan. 2:27, 28; Mt. 1:20.

Baadhi ya ndoto hazitoki kwa Mungu:

Ndoto nyingine hazina thamani - Isa. 29:8.  
 “Kwa maana doto huja kwa sababu ya shughuli nyingi . . .” - Mhu. 5:3.  
 “. . . wanaotabiri kwa mioyo yao wenyewe . . .” - Eze. 13:1-3.  
 “. . . Je! Hamkuona maono ya bure? . . .” - Eze 13:6-8.  
 Baadhi ya ndoto zilikuwa za uongo - Zek. 10:2; Eze. 22:28.  
 Ndoto yo yote iliyowapotosha watu kutoka kwa Mungu na ufunuo wake haikutoka kwake.

Hatari za Ndoto:

Ndoto inaweza ikampoteza mtu aabudu Mungu wa uongo - Kum. 13:1-3; Eze. 12:24.  
 Ndoto ziwapo nyingini, maneno ya ubatili huwa mengi - Mhu. 5:7.  
 Mwotaji wa ndoto anaweza akafundisha mafundisho yaliyo kinyume na Mungu - Kum. 13:1-5.  
 Ndoto zinaweza zikautia mwili uchafu - Yuda 8.  
 Ndoto zinaweza zikamfaanya mtu kuyakataa mamlaka na kuyatukana matukufu - Yuda 8.

Mungu Anataka Tumfuate Mwanawe Na Neno Lake Badala Ya Ndoto.

Mungu hasemi nasi kwa njia ya ndoto sasa bali husema nasi kwa njia ya Mwanawe na neno lake - Ebr. 1:1, 2; 2 Yoh. 9; Yuda 3, 4, 8.  
 Ndoto hazina maana sana kuliko neno la Mungu - Kum. 13:3; Yer. 23:23-28; Eze. 12:224, 25; 2 Tim.

16:17.

Imani yetu inategemea Kristo na neno lake wala si ndoto - Rum. 10:17; 1 Kor. 3:11;; 2 Pet. 1:16.

Hatusimani kwa kutegemea ndoto au maono - Kol. 2:18.

Neno la Mungu hutukamilisha kabisa - 2 Tim. 3:16, 17; Gal. 1:8, 9; Ufu. 22:18.

## **Neema**

### Mungu Ni Mungu Wa Neema:

Mungu wa neema yote - 1 Pet. 5:10.

Kiti chake cha enzi ni kiti cha neema - Ebr. 4:16.

Roho wa neema - Ebr. 10:29.

Injili ya neema yake - Mdo. 20:24.

Wingi wa neema yake umedhihirishwa katika Kristo - Efe. 2:7.

Utukufu wa neema yake - Efe. 1:6.

Neno la neema yake - Mdo 14:3; 20:32.

Neema yake ni kwa wote - Tito 2:11

### Neema Ya Mungu Ni:

Kubwa (nyingi) - Mdo. 4:33.

Nyingi - Efe. 1:7; 2:7.

Ya kuzidi - 2 Kor. 9:14.

Ya namna nyingi - 1 Pet. 4:10.

Ya kutosha - 2 Kor. 122:9.

Nyingi sana - Rum. 5:15.

Ya kweli - 1 Pet. 5:12.

Yenye utukufu - Efe. 1:6.

Yenye uwezo - 1 Kor. 15:10.

### Neema Ndiyo Asilli Au Msingi Wa:

Uchaguzi - Rum. 11:5.

Mwito - Gal. 1:15.

Kuhesabiwa haki - Rum. 3:24; Tit. 3:7.

Imani - Mdo. 18:27.

Msamaha wa dhambi - Efe. 1:7.

Wokovu - Mdo. 15:11; Efe. 2:5,8.

Faraja ya milele na tumaini jema - 2 The. 2:16.

### Neema Ya Kristo:

Neema ya Mungu ilikuja kwa njia ya Kristo - Yn. 1:17.

Neema ya Mungu imetolewa kwa njia ya Kristo - 1 Kor. 1:4; Rum. 3:24.

Kristo amejaa neema - Yn. 1:14.  
Maneno yake yalikuwa ni maneno ya neema - Luka 4:22.  
Neema ya Kristo ilizidi kwa wenye dhambi - 1 Tim. 1:14, 15.  
Alijitoa mwenyewe kwa sababu ya neema yake - 2 Kor. 8:9.  
Kwa neema ya Mungu, Yesu alikufa kwa ajili ya kila mtu - Ebr. 2:9.

#### Wototo Wa Mungu:

Hupokea neema kutoka kwa Kristo - Yn. 1:16.  
Wako chini ya neema - Rum. 6:14.  
Huhesabiwa haki kwa neema, siio kwa matendo ya sheira - Gal. 2:21; 5:4.  
Hupata nguvu kwa njia ya neema - 1 Kor. 15:10.  
Hupata neema ya kuwasaidia wakati wa mahitaji - Ebr. 4:16.  
Ni warithi wa neema ya uzima - 1 Pet. 3:7.

#### Jukumu La Wale Waipokeao Neema Ya Mungu:

Msiipoke e neema ya Mungu bure - 2 Kor. 6:1.  
Iweni na wingi wa neema - 2 Kor. 9:8.  
Kuwa imara kwa neema - Ebr. 13:9.  
Kuwa hodari katika neema - 2 Tim. 2:1.  
Kukua katika neema 2 Pet. 3:18.  
Maneno yawe na neema - Kol. 4:6; Efe. 4:29.  
Kujinyenyekesha ili waipokee neema - Yak. 4:6; 1 Pet. 5:5.  
Kufurahi kwa kuiona neema ya Mungu - Mdo. 11:23.  
Kumwambia Mungu kwa neema mioyoni mwenu - Kol. 3:16.  
Kuangalia sana wasiipungukiwe na neema ya Mungu - Ebr. 122:15.  
Wasiibadili neema ya Mungu kuwa ufisadi - Yuda 4; Rum. 6:1, 15.  
Kumtumikia Mungu kwa neema - Ebr. 12:28.

### **Njia Moja Kwa Baba**

#### Yesu Kristo Ndiye Njia Ya Pekee:

Yesu alisema yeye ndiye njia - Yn. 14:6.  
Yesu mwenyewe atamfunua Baba - Mat. 11:27.  
Tunaweza kuwa na neema kupitia kwa Yesu - Rum. 5:2.  
Yesu ndiyo mlango - Rum. 10:9.  
Kama tusipodumu katika mafundisho ya Yesu basi hatuna Mungu - 2 Yoh. 9.  
Yeye tu anastahili kufungua kitabu na kukomboa wanadamu - Ufu. 5:8-9.

### **Pasaka**

Ni Sikukuu Katika Agano La Kale Kwa Kukumbuka Uhuru Waliopewa Toka Katika Nchi Ya Misri:

Pasaka ilianzishwa - Kut. 12.

Walitakiwa kushiriki Pasaka mara moja kwa mwaka - Kumb. 16:1.

Leo Yesu Kristo Ndiye Pasaka Wetu Na Tunashiriki Mauti Yake Kila Jumapili:

Yesu Kristo nidye pasaka wetu - 1 Kor. 5:7.

Tunatakiwa kushiriki meza ya Bwana kwa kumkumbuka Yesu - 1 Kor. 11:23-27.

Wakristo wa karne ya kwanza walishiriki Meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma - Mdo. 20:7.

**Pepo (Mashetani)**

Mwanzo Na Hali Ya Pepo:

Mwanzo wao haujulikana kwa kweli. Inawezekana kwamba Shetani na pepo walikuwa malaika mbingunii mwaanzoni. Walitenda dhambi ya majivuno na kumwasi Mungu. Baadaye wakatupwa chini duniani. Angalia Lk. 10:18; 1 Tim. 3:6; 2 Pet. 2:4; Ufu. 12:7-9.

Pepo ni roho - Mt. 8:16; Lk. 10:17, 20.

Pepo ni wabaya - Mt. 10:1; Mk. 1:27; Mdo. 8:7

.

Kazi ya Pepo:

Wao ni waatumishi wa Shetani na kwa hivyo humsaidia katika kazi yake - Mt. 10:25; 12:24, 27; Mk. 3:22; Lk. 11:15, 18, 19.

Hufanya vita juu ya Wakristo - Efe. 2:2; 6:122.

Huwajaribu Wakristo - 1 Kor. 7:5.

Huzuia mahubiri ya Injili - Mk. 4:15; Mdo. 16:16-18; 1 The. 2:18.

Huwapoteza watu kwa mafundisho ya uongo - 1 Fal. 22:21-23; 1 Tim. 4:1.

Huwaonea watu - Mdo. 10:38; Efe. 5:16; 6:11, 12.

1. Wanaweza kusababisha magonjwa na Mateso - Ayubu 1:5-10; Mt. 9:33; 12:22; Lk. 9:37-42; 13:11.
2. Wanaweza kumfanya mtu kupotewa na akili - 1 Sam. 16:14; Mk. 5:1-15; Lk. 8:35. Kumbuka, si magonjwa yote yaliyosababishwa na pepo.
3. Mungu huwazuia - Ayubu 1:6-12; 1 Kor. 10:13.
4. Wakati mwingine huwaingia wanadamu na wanyama pia - Mt. 4:24; Mk. 5:8-14; Lk. 8:2; Mdo. 8:7, 16:16.
5. Kataka Agano Jipya mtu mwenye papo aliweza kulia (Mk. 1:23). Kujiumiza mwenyewe (Mk. 5:5). Na kuwa na kifafa (Mk. 9:20).

Wasiomtii Mungu wako chini ya utawala wa pepo - Efe. 2:2.

Wakati mwingine Mungu aliwatumia pepo wabaya kutimiza makusudi yake. Waamuzi 9:23; 1 Sam. 16:14; Angalia 1 The. 2:9-11.

Aina tatu za kazi zinazohusiana na pepo ambazo zinapaswa kuepukwa na Wakristo.

1. Kutabiri mambo yajayo kwa kutumia uganga wa kienyeji kama vile kutazama maini ya

- wanyama - Eze. 21:21; Mwa. 44:5; Isa. 47:13-15.  
 2. Kuabudu mashetani - Kum. 32:16, 17; 1 Kor. 10:20.  
 3. Kuzungumza na wafu - Law. 19:31; 20:6, 27; Kum. 18:10, 11; 1 Sam. 28:7-25; 1 Nya. 10:13, 14; Isa. 8:19.

Angalia somo linalohusu uchawi.

### Yesu Ana Uwezo Juu Ya Pepo.

Mara kwa mara alikemea na kuondoa pepo - Mk. 1:23-27; 3:11, 12; 5:1-20; 7:25-30; 9:11, 17-29.  
 Aliwapa mitume uwezo huo - Mdo. 5:16; 8:7; 16:16-18.  
 Yesu alimshinda Shetani - Kol. 2:15.

### Wakristo Hawana Haja Ya Kuwaogopa Pepo.

Wakristo, kwa sababu ya Yesu, hawapaswi kuwaogopa pepo kwa maana uwezo wa Kristo, aliyemshinda Shetani, hufanya kazi ndani yao - Kol. 2:15; Efe. 6:12-18; Rum. 8:31-39.  
 Uwezo wa Wakristo juu ya pepo ni katika Yesu; kwa njia ya maombi na kufunga - Mt. 17:21; Efe. 4:27; 6:10-20; Yak. 4:7; 1 Pet. 5:8, 9; 1 Kor. 10:13; Ufu. 17:14.  
 Mkristo ana roho watumikao ambao wametumwa kumhudumia - Ebr. 1:14.  
 “. . . .aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye alilye duniani” - 1 Yoh. 4:4.

### Mwisho Wa Pepo.

Moto waa milele - Mt. 25:41.  
 Ziwa la moto na kiberiti - Ufu 20:10.  
 Mateso - Mt. 8:29.

## **Petro Ni Nani?**

### Petro alikiri kwa hali ya juu sana katika Biblia na kukana kwa hali ya juu sana.

Mt. 16:18 - Kukiri kwake ilikuwa kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Kukiri huko kulihusu maneno aliyosema Yesu kulijenga Kanisa lake kuhusiana na maneno aliyoyasema Petro na sio juu ya Petro.  
 Zab. 118:22 - Mwandishi anabashiri kwamba yeye aliyekataliwa atakuwa jiwe kuu la pembeni, taz. Mt. 21:42; Mdo. 4:11.  
 Efe. 2:20 - Yesu mwenyewe ndiye jiwe kuu la pembeni. Ambalo mtume Petro akiwa mmoja alijengwa juu yake.  
 1 Pet. 2:5-9 - Jiwe kuu la pembeni lilijengwa (liliwekwa) Sayuni.  
 1 Kor. 3:11 - Hutuonyesha kwamba Kristo ndiye aliyeweka msingi.  
 Mt. 26:69-75 - Alimkana Kristo mara tatu.  
 Yn. 1:42 - Mmoja aliyelitwa na Yesu pia aliitwa kefa.  
 Gal. 2:14 - Paulo anamkemea Petro kwa kitendo chake.  
 1 Kor. 9:5 - Petro alikuwa na mke.

I Pet. 5:1 - Petro alikuwa mzee wa Kanisa. Ili kuwa mzee wa Kanisa mtu alipaswa kuwa mume wa mke mmoja, Tit. 1:5,6.

I Pet. 1:1- Anajieleza kuwa yeye ni mtume tu.

Mt. 8:14 - Petro alikuwa na mama-mkwe.

## **Roho Mtakatifu**

### Majina Yake:

“Roho Mtakatifu” - Mt. 3:11; 28:19.

“Roho wa Mungu” - Flp. 3:3; 1 Kor. 6:11.

“Roho wa Bwana” - Isa. 61:1; Lk. 4:18; Mdo 5:9.

“Roho wa Kristo” - Rum. 8:9; Flp. 1:19.

“Msaidizi” - Yn. 14:16, 26.

“Roho wa kweli” - Yn. 14:17; 16:13.

“Roho wa Neema” - Ebr. 10:29.

“Roho” - 1 Tim. 4:1; Mdo. 2:4.

Tabia Zake: Yeye Sio Nguvu Tu, Bali Ni Mtu Au Nafsi. Anaweza Kufikiri, Kujua, Kupenda, Kutendewa Mabaya Na Kuhuzunika, Na Kufanya Mambo Mengi Ambayo “Nguvu” Haiwezi Kufanya.

“Nia ya Roho ilivyo” - Rum. 8:27.

Anajua - 1 Kor. 2:11.

Huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu - 1 Kor. 2:10.

Kama apendavyo yeye - 1 Kor. 12:11.

Walikatazwa na Roho Mtakatifu - Mdo. 16:6.

Upendo wa Roho - Rum. 15:30; 5:5.

Roho anena waziwazi - 1 Tim. 4:1; Mdo. 8:29.

Hushuhudia - Yn. 15:26, 27; Mdo. 20:23; Rum. 8:16.

Hutuombea - Rum. 8:26, 27.

Msimhuzunisha Roho wa Mungu - Efe. 4:30.

Watu waalijaribu kumdanganya Roho Mtakatifu - Mdo 5:3.

Watu wanaweza wakamkufuru - Mk. 3:29.

Anaweza kutendewa jeuri - Ebr. 10:29.

### Kazi Zake:

Kazi ya kuwaongoza wasemaji wa Mungu wasiiache njia ya kweli katika kuhubiri kwao na maandiko yao. 2 Pet. 1:19-21; 2 Tim. 3:16, 17; Mt. 10:19, 20; Yn. 14:26; 16:13; Mdo. 2:1-4; 1 Kor. 2:9-13.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu:

1. Mitume wa Yesu Kristo walibatizwa katika Roho Mtakatifu ili kwamba waongozwe katika kweli yote na waweze kuyakumbuka yote Yesu aliyowafundisha - Yn. 14:26; 16:13; Lk. 24:49; Mdo 1:1-8; 2:1-4; 4:33; 6:6; 10:39-41.
2. Kornelio na nyumba yake walibatizwa katika Roho Mtakatifu ili kuthibitisha kwamba Mataifa

walikubaliwa na Mungu sawasawa na Wayahudi - - kwa njia ya Injili - - mbali na sheria ya Musa. - Mdo 10:1-48; 11:1-18; 15:7-11.

**KUMBUKA:** Kwa Kweli, Mitume wa Kristo waliongozwa katika kweli yote, na sasa tunayo kweli hiyo katika Biblia, kitabu kitakatifu cha Mungu. Na jinsi ilivyothibitishwa hapo zamani kwamba Mataifa wamekubaliwa na Mungu sawasawa na Wayahudi, bado tunao ushahidi huo katika Biblia. Kwa sababu hiyo, kazi hiyo ya ubatizo wa Roho Mtakatifu ilitimilika, na hakuna ubatizo wa aina hiyo siku hizi. Paulo aliandika kwamba kuna “Ubatizo mmoja” (Efe. 4:5), na ubatizo huo ni katika maji “kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu”, “kwa msamaha wa dhambi.” Ubatizo huo unapaswa kuhubiriwa kwa Mataifa yote mpaka mwisho wa kizazi hiki Mt. 28:19, 20; Mk. 16:15, 16; Mdo. 2:38; 8:36-38; 10:48; Efe. 5:26; Tito 3:5; 1 Pet. 3:20, 21. Wakristo wote wana Roho Mtakatifu ndani yao, wakiwa hekalu la Mungu (1 Kor. 3:16; 6:19, 20), na wanasaidiwa naye sana lakini hawabatizwi katika Roho Mtakatifu kama Mitume na Kornelio walivyobatizwa.

Vipawa (Karama) vya Roho Mtakatifu, vya aina mbalimbali, vilitolewa kwa kuwekewa mikono ya mitume. Mitume hawa walichaguliwa wawe mashahidi wa kufufuka ke Yesu (Mdo. 1:1-8, 21, 22; 10:39-41). Pia walikuwa na uwezo wa kutoa nguvu za Roho Mtakatifu kwa wengine. Mitume walifanya hivyo kwa kuwawekea mikono yao juu yao. (Mdo. 6:6, 8; 8:5-24; 19:1-7). Kwa kuwa walikuwa wakiyafunua mapenzi ya Mungu. Bwana “alilithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo: - Mk. 16:20; Ebr. 2:3,4. Huuhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi - Yn. 16:8. Je! Anaendelea kuuhakikishia ulimwengu wa dhambi kwa jinsi gani?

1. Watu walichomwa mioyo yao kwa mahubiri ya Petro aliyeongozwa na Roho Mtakatifu - Mdo. 2:4, 36, 37.
2. “Upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu” - Efe. 6:17.
3. Neno la Mungu li hai na litendaje - Ebr. 4:12.
4. Mahali ambapo Injili haijhubiriwa, watu hawamjui Yesu Kristo na hawajahakikishiwa kwa habari ya dhambi zao.

Roho Mtakatifu huishi ndani ya Wakristo kama hekalu la Mungu - Mdo. 2:38; 5:32; Gal. 4:6, 1 Kor. 3:16, 17; 6:19; Efe. 2:20-22. Kwa kuishi ndani ya mioyo ya Wakristo, Roho Mtakatifu huzaa tunda la Roho (Gal. 5:22, 23), ambalo ni:

1. Upendo - 1 Kor. 13:1-6; Kol. 3:14.
2. Furaha - Rum. 14:17; 15:13; Flp. 4:4.
3. Amani - Yn. 14:27; Rum. 5:1; Flp. 4:6, 7.
4. Uvumilivu - Efe. 4:2; Kol. 3:12.
5. Utu wema (kuwa na huruma) - Kol. 3:12; 1 Pet. 3:8.
6. Fadhili - Efe. 4:25-31; Rum. 15:14.
7. Uaminifu - Tito 2:10; Ufu. 2:10.
8. Upole - Efe. 4:2; 1 Pet. 3:4; 5:5, 6.
9. Kiasi - Mdo. 24:25; 2 Pet. 1:6.

Roho Mtakatifu hutombea - Rum. 8:26, 27.

1. “Msaidizi,” jinsi Yesu alivyo “Mwombezi” - Yn. 14:26; 1 Yoh. 2:1.
2. “Msaidizi mwingine” - - wa aina iyo hiyo - Yn. 14:16; Ebr. 7:25.
3. “Faraja ya Roho Mtakatifu” - Mdo. 9:31. Kanisa la Bwana liliimarishwa na kuongezeka kwa



sababu ya Roho Mtakatifu, kama Msaidizi wake, aliwafariji Wakristo na kuwatia nguvu.

3. Yesu Kristo pekee ndiye “Mpatanishi” kati ya Mungu nasi - 1 Tim. 2:5. Mpatanishi ni mtu “aendaye kati” ya watu wawili, na kuwafanya washirikiane, (yaani msuluhishi) - Efe. 2:11-16; 2 Kor. 5:18, 19. Yesu pekee ndiye aliyeitamiliza kazi hiyo.
4. Lakini Roho Mtakatifu pia ni “Msaidizi” abakiye kwa upande wa mtu na kumwombea. Hivyo ni kusema kwamba, ingawaje hatujui kuomba ipasavyo, Roho Mtakatifu huyafanya maombi yetu kuwa na maana na kuyawasilisha mbele za Mungu.

Kumkufuru Roho Mtakatifu: - Mt. 12:31, 32; Mk. 3:22-30.

1. Mfano wa Waisraeli - 2 Nya. 36:15, 16; Yer. 7:8-16; 24-28; Hes. 15:27-31. Waisraeli waliifanya migumu mioyo yao kwa kulikataa kwa kusudi neno la Mungu mpaka “kukawa hakuna kuponywa,” na Yeria akaambiwa kwamba asiwaombee hata kidogo!
2. Katika Agano Jipya - Rum. 1:21-31; Efe. 4:17-19; 1 Tim. 4:1, 2; Ebr. 3:7, 15; 6:1-6; 10:26-29; 12:25. Maandiko haya yanafundisha kwamba wakati watu wanayakataa kwa kusudi maneno ya Roho Mtakatifu, na kuendelea kufanya dhambi kwa kusudi, wanaweza kuifanya migumu mioyo yao mpaka washindwe kutubu ili wasamehewe. Kwa njia hii, humfanyia jeuri Roho Mtakatifu na kutenda “dhambi ya milele.”

Angalia “kipawa cha Roho Mtakatifu.”

### **Roho Mtakatifu Na Neno Lililoandikwa**

#### Je! Biblia Ni Kitabu Cha Aina Gani?

Tunapaswa kuiruhusu Biblia iseme juu ya tabia yake yenyewe:

1. 2 Tim. 3:16, 17 - Mungu aliyevuta pumzi Maandiko Angalia Mt. 4:4.
2. 2 Pet. 1:19-21 - Maandiko matakatifu hayakutokana na wanadamu na hekima yao bali yalitokana na Mungu Angalia Gal. 1:11, 12 pia.
3. Yn. 10:35 - Yesu alifundisha kwamba Maandiko hayawezi kutanguka.

Haya maandiko yametajwa hivi katika Biblia:

1. “Maandiko Matakatifu” - Rum. 1:2.
2. “Neno la Mungu” - Rum. 3:2; 9:6.
3. “Maandiko Matakatifu” (yaliyotengwa mbali na maandiko mengine) - 2 Tim. 3:15.

Maneno ya maandiko hayo na Maneno ya Mungu:

1. Rum. 9:17.
2. Gal. 3:8; Mwa. 18:17, 18.
3. Mdo. 4:25.
4. Mdo. 28:25.
5. 2 Pet. 3:15, 16.

#### Nia Ya Kristo Kuhusu Maandiko Matakatifu:

Maandiko yavuta pumzi na Roho Mtakatifu - Mt. 22:43; Mk. 12:36.

Maandiko yalimshuhudia Yeye - Yn. 5:39, 46, 47; Lk. 24:25-27, 44-47.

Aliamini miujiza (ishara) iliyoandikwa katika Agano la Kale:

1. Juu ya Muumba, alikiamini kitabu cha Mwanzo - Mt. 19:4-6.
2. Kuhusu Safina ya wakati wa Nuhu, Lk. 17:26, 27.
3. Musa na kijiti kilichowaka moto - Mk. 12:26.
4. Yona na Nyangumi. Hadithi hii ni ya kweli na hutumiwa kama mfano wa kufufuka kwake kutoka kwa wafu - Mt. 12:39-41.
5. Kristo aliyatumia Maandiko wakati alipojaribiwa na Shetani - Mt. 4:1-10.
6. Maandiko "lazima yatimizwe" hata kwa kifo msalabani - Mt. 26:24, 54, 56; Mk. 14:27.

#### Roho Mtakatifu Huzungumza Kwa Njia Ya Neno La Mungu:

Katika Agano la Kake, kwa manabii - Yer. 2:1, 2; Eze. 2:1, 2; Hos. 1:1; Yoeli 1:1; Mika 3:8; Neh. 9:20, 30. Agano Jipya hushuhudia kwamba Agano la Kale lilitoka kwa Mungu - Mdo. 1:16; 7:51-53; Mk. 12:36; Ebr. 3:7; 9:8; 10:15; 1 Pet. 1:11; 2 Pet. 1:21.

Kwa mitume na manabii wa Agano Jipaya:

1. Ahadi ya Yesu - Yn. 15:26; 16:7-13; Mt. 10:19, 20.
2. Kutimizwa kwa ahadi hiyo - Mdo. 2:1-47; Gal. 1:11, 12; Efe. 3:5; 1 The. 2:13.

#### Roho Mtakatifu Huwahakikishia Wenye Dhambi Makosa Yao Na Kuwageuza Wamwelekee Mungu Kwa Njia Ya Neno:

Ushuhuda (ushahidi) wa Roho ni kwa njia ya maandiko:

1. 1 Pet. 1:10-12; 2 Pet. 1:20, 21.
2. Efe. 3:5.
3. Ebr. 3:7; 9:8; 10:15-17.
4. Ufu. 2:7, 11, 29; 3:6, 13, 22.

Roho Mtakatifu Huzihakikisha dhambi kwa njia ya neno:

1. Kuhakikisha - Yn. 16:7-11; 2 Tim. 3:16, 17; 4:2.
  - a) Kwa dhambi - Yn. 3:18; 8:24.
  - b) Kwa haki - Mdo. 2:22, 23, 33; 3:14; 7:52; 1 Pet. 3:18; 1 Yoh. 2:1.
  - c) Kwa hukumu - Yn. 12:31, 32; Ebr. 2:14, 15.
2. Mdo. 2:36, 37; Efe. 6:17; Yn. 3:5; Tito 3:5.
3. Ebr. 4:12; 1 Pet. 1:23; Yak. 1:21; Yn. 17:17.

Mifano ya Roho Mtakatifu katika kuwageuza Wenye Dhambi:

1. Katika siku ya Pentekoste - Mdo. 2.
2. Wasamaria - Mdo. 8:5-12.
3. Towashi wa Kushi - Mdo. 8:26-39.
4. Kornelio - Mdo. 10:1-48; 11:1-18.
5. Mlinzi wa jela huko Filipi - Mdo. 16:25-34.
6. Wakorintho - Mdo. 18:8; 1 Kor. 4:15; 6:9-11.

KUMBUKA: Mahali ambapo neno la Mungu halijafika, wenye dhambi hawajahakikishiwa dhambi zao na hawajatubu. Kwa sababu hii, tunalo jukumu kubwa kwa kuihubiri Injili kwa kila kiumbe ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kuwahakikishia dhambi zao na kuwaongoza waje kwa Yesu awezaye kuwaokoa.

## **Sabato**

Siku Ya Sabato Ilikuwa Ni Jumamosi, Wala Sio Siku Kwanza Ya Juma (Jumapili):

“Siku ya saba ni Sabato” - Kut. 20:10.

“Siku ya saba ni Sabato” - Kut. 31:15.

“Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza juma” - Mt. 28:1.

Sabato Ilijulikana, Kwa Mara Ya Kwanza, Karibu Na Mlima Sinai:

Mungu aliitunza sabato ya kwanza, lakini hakuna ushahidi wa kuonyesha kwamba aliwapa wanadamu waitunze - Mwa. 2:3.

Maandiko hayaonyeshi kwamba Adamu, Nuhu, Ibrahimu au Yakobo waliitunza sabato.

Mfano wa kwanza Watu waliopewa sabato ni Waisraeli walipopigilia hema zao karibu na Mlima Sinai - Kut. 16:4, 5, 22-30.

Mungu aliwajulisha Waisraeli kuhusu sabato Mlimani Sinai kwa Mkono wa Musa - Neh. 9:13,14.

Mungu alizitoa sabato wakati Wairaeli walipokuwa jangwani - Eze. 20:10-12.

Sabato ilikuwa ni ishara kati ya Mungu na Waisraeli, wala sio mataifa yote - Kut. 31:12-17.

Aliwapa siku ile ambayo Mungu alipumzika hapo mwanzoni - Kut. 20:11; 31:17.

Sabato Ilitolewa Kwa Waisraeli Pekee:

Ilitolewa kwa watu wale ambao Mungu aliwatoa Misri - Kut. 20:2, 8-11.

“Akawaita Israeli wote” akawapa sabato na amri zingine - Kum. 5:1.

Mungu hakufanya agano hili na baba zao - Kum. 5:1-21.

Waisraeli walipewa sabato kwa kuwa waliokolewa kutoka utumwani Misri - Kum. 5:15.

Kristo Aliitunza Sabato Pamoja Na Sheria Zote Za Kiyahudi:

Yesu alizaliwa Myahudi, “Alizaliwa chini ya sheria” - Gal. 4:4.

Alipata kutahiriwa, na dhabihu zikatolewa pia. “Kama ilivyo torati ya Musa” - Lk. 2:22-39.

Aliwafundisha Wayahudi kwamba wanapaswa kushika sheria za kutoa dhabihu - Mt. 8:2-4.

Alizishika sikukuu za Kiyahudi kama Pasaka na sikukuu ya vibanda - Lk. 22:8, 15; Yn. 7:2.

Aliweza kukutana na Wayahudi katika masinagogi yao - Lk. 4:15, 20.

Alifundisha hekaluni mwao - Mt. 26:55.

Aliitunza sabato kwa sababu aliitii sheria yote - Gal. 4:4.

Lakini msalabani aliitimiza sheria nzima na kuiondoa - Yn. 19:28-30; Efe. 2:14-17; Kol. 2:14-16.

Aliliondoa agano la kwanza, ili kwamba aweze kulisimamisha la Pili - Ebr. 8:6-13; 10:9, 10.

Sheria ilibadilishwa - Ebr. 7:12.

Sheria (torati) ilikuwa mwalimu (kiongozi) wa kuwaleta watu kwa Kristo, lakini Wakristo hawaendelei kumtii huyo mwalimu (kiongozi) - Gal. 3:24, 25.

#### Wakristo Hawakupewa Sabato:

Paulo alihubiri au alihoji ana na Wayahudi katika siku ya sabato kwa sababu alikuweza kuwapata watu wengi siku hiyo, kwa maana Wayahudi walikutanika siku hizo za sabato - Mdo. 13:14, 42; 17:2, 3; 18:4. Walakini, hatusomi mahali po pote kwamba “aliitunza” sabato . . . Kuhubiri siku ya sabato ni tofauti na “kuitunza” sabato.

Wakristo hawana sheria kwamba waitunze sabato.

Hakuna mfano wote wa Wakristo wa kwanza kuitunza sabato.

Wakristo hawahukumwi juu ya Sabato na mambo mengine ya Kiyahudi - Kol. 2:14-17; Rum. 6:14.

Raha ya sabato iliyobaki kwa watu wa Mungu ni ile itakayokuwa mbinguni - Ebr. 4:1-11; 11:13-16.

#### Biblia Husema Juu Ya Siku Ya Kwanza Ya Juma Kwamba:

Kristo alifufuka kutoka kwa wafu katika siku ya kwanza ya juma - Mk. 16:1-9; Lk. 24:1, 13, 21, 46.

Hivyo, alidhihirishwa kuwa mwana wa Mungu katika siku ya kwanza ya juma - Rum. 1:4.

Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, Kristo alikutanika mara kwa mara na mitume wake katika siku ya kwanza ya juma - Yn. 20:1, 19, 26.

Kanisa la Mungu lilianzishwa wakati wa Pentekoste, siku ya kwanza ya juma - Law. 23:15; Mdo. 2:1-47.

Roho Mtakatifu alikuja na kuanza kazi yake katika siku hiyo ya kwanza ya Juma - Mdo. 2:1-4.

“Yapata roho 3,000,” “Malimbuko” ya Injili (Law. 23:17) zilizidishwa kanisani siku hiyo - Mdo. 2:41, 47.

Kanisa la Bwana lilikutanika katika siku ya kwanza ya juma ili kushiriki chakula cha Bwana na kufanya mambo mengine - Mdo. 20:7; 2:42; 1 Kor. 16:2; 11:23-33.

Katika Agano Jipya tuna mambo mapya:

1. Agano Jipya - Ebr. 8:13; 10:9, 10.
2. Kanisa jipya - Mt. 16:18; Efe. 1:20-23.
3. Maagizo mapya - 1 Kor. 14:37; Mk. 16:15, 16.
4. Siku mpya - Mdo. 20:7; 1 Kor. 16:1, 2.
5. Jina jipya kwa hiyo siku mpya na Kuriakos (Kiyunani) - Ufu. 1:10.

#### **Sheria za Musa.**

#### Unabii wa baadhi ya manabii wakuu kuhusu mwisho wa Sheria ya Musa.

Eze. 7:26 - Unabii kuwa sheria ilitoweka.

Yer. 31:31-33 - Mungu atafanya sheria mpya.

Hos. 2:11 - Mungu atasababisha furaha zote za Israeli; sikukuu, mwandamo wa miezi, sabato na makusanyiko yake yote kukoma.

Kumb. 18:15 - Musa amaeleza kwamba Nabii alikuwa anakuja kama yeye na asikilizwe nasi, angalia Mdo. 3:22-23.

### Mungu Aliiona Ilikuwa na Hitilafu na Akaiondoa.

Ebr. 8:6-13 - Mungu aliona hitilafu katika Agano la Kwanza na akaweka Sheria mpya.  
Kol. 2:13-15 - Akaiondoa sheria ya Musa kwa kuigongaomea msalabani.  
Ebr. 10:4 - Maana isingewezekana damu ya wanyama kuondoa dhambi zetu.  
Yn. 1:17 - Sheria ilitolewa na Musa bali neema na kweli zililetwa na Yesu Kristo.  
Gal. 3:23-29 - Sheria ilikuwa ya kuwaleta watu kwa Kristo.  
Gal. 3:10 - Kazi ya Sheria ni Laana.  
Rum. 7:6 - Kuokolewa toka sheria na kutumika katika upya wa Roho.  
Ebr. 1:2 - Leo azumgumza nasi kwa njia ya Mwana wake sio Musa!  
2 Kor. 3:3-16 - Paulo anatufundisha vibao vya mawe, Agano la Kale na Torati ni huduma za mauti.

### **Sheria Za Yesu**

Leo Mungu anazungumza kwa njia ya Yesu - Ebr. 1:1,2; Pia Taz. 17:5; Yn. 12:48.  
Ufunuo wa neema na kweli ya Mungu vilikuja kwa njia ya Yesu - Yn. 1:17; Tit. 2:1.  
Yesu ni njia, kweli na uzima - Yn. 6:63.  
Kifo chake kiliwezesha Agano Jipya - Ebr. 9:15-18.  
Agano Jipya ni sheria kamilifu ya uhuru - Yak. 1:25.  
Ilitolewa kwa wote - Mt. 28:19; Mk. 16:15.  
Imewekwa wakfu kwa damu - 1 Kor. 5:7; Ebr. 10:10, 19, 20; 1 Pet. 1:19.  
Agano Jipya kuokoa leo - Ebr. 7:25.  
Imewekwa na Mwana wa Mungu - Ebr. 2:1-4.

### **Shetani, (Mchongezi, Ibilishi)**

#### Majina Yake:

Shetani - "Adui" - Ayubu 1:6-12; Zek. 3:1; Mt. 13:39; 1 Pet. 5:8.  
Mshitaki - Ufu. 12:10.

#### Tafadhali angalia 1 Tim. 3:11.

Mjaribu - Mt. 4:3; 1 The. 3:5.  
Beelzebuli - "mkuu wa pepo" - Mt. 12:24-28; Mk. 3:22.  
Mwovu - Mt. 13:19, 38; 1 Yoh. 2:14; 3:12; 5:18, 19.  
Mdanganyaji wa ulimwengu - Ufu. 12:9.  
Joka kubwa - Ufu. 12:3, 9; 20:2.  
Baba wa uongo - Yn. 8:44.  
Mkuu wa ulimwengu - Yn. 14:30; 12:31.  
Mungu wa dunia hii - 2 Kor. 4:4.

#### Historia yake:

Aliumbwa na Mungu, akajitukuza mwenyewe, akamwasi Mungu, akawa adui yake. Tafadhali kumbuka: - Mwa. 1:31; 2 Pet. 2:4; Yuda 6; Mt. 25:41; 1 Tim. 3:6.

Aliwasababisha Adamu na Hawa kutenda dhambi - Mwa. 3:1-6; Yn. 8:44; 2 Kor. 11:3.

Alimtesa Ayubu - Ayubu 1-2; Pia angalia Lk. 13:16; 2 Kor. 12:7; Mdo. 10:38.

Huzipofusha akili za wasioamini - 2 Kor. 4:4; 1 Yoh. 5:19; Rum. 1:21-31.

Alimjaribu Yesu - Lk. 4:1-13; Ebr. 4:15.

Alisumbua na kuwapoteza watu wengine - Mt. 16:23; Lk. 22:31, 32; Yn. 8:44.

Hujaribu kuizuia kazi ya Mungu isitendeke - Mk. 4:15; Mdo. 5:3; 13:10; 2 The. 2:18; 2 Kor. 2:11.

### Tabia Zake:

Ana uwezo mkubwa wa kudanganya - 2 The. 11:3; Mwa. 3:1; 2 The. 2:10 -12.

Amedhihirika kama:

1. Nyoka - 2 Kor. 11:3.

2. Malaika wa nuru (Hujigeuza kuwa mfano wa malaika wa nuru) - 2 Kor. 11:14.

3. Simba angurumaye - 1 Pet. 5:8.

Huendelea kuwaribu watu kwa njia tatu (1 Yoh. 2:16):

1. Tamaa ya mwili - 1 Pet. 2:11; Rum. 13:14; Gal. 5:19-21.

2. Tamaa ya macho - Mit. 27:20; Mhu 5:10; Mwa. 3:6.

3. Kiburi cha uzima - 1 Yoh. 2:16; Yak. 4:6, 7; Mwa. 3:6.

Shetani hutenda kazi:

1. Katika dini za uongo - 2 Kor. 11:13-15; 1 Tim. 4:1; Ufu 2:9; 19:20.

2. Katika mashule ambako Mungu na Neno lake limekataliwa.

3. Katika serikali zimbatazo Mungu na kuizuia kazi yake - Ufu. 13:1-10.

4. Katika sehemu ambazo hufanywa karamu za ulevi na ulafi - Rum. 13:13, 14; Mit. 23:20; 1 Pet. 4:3, 4.

### Vita Kati Ya Wakristo Na Shetani:

Si vita vya kimwili - Efe. 6:10-12.

Yesu alimshinda shetani katika mauti yake kwa kufufuka kutoka kwa wafu - Lk. 10:18; Ufu. 12:9; Ebr. 2:14, 15; 1 Yoh. 3:8.

Wakristo nao pia watamshinda katika Kristo - Yak. 4:7; Efe. 4:27; 6:11-19; 1 Pet. 5:8, 9; 1 Kor. 10:13; Ufu. 17:14.

## **Kutoa Shukrani**

### Kielelezo Cha Kristo:

Kwa Kikombe - Mt. 26:27; 1 Kor. 11:24.

Kwa kuwa Mungu Baba aliyasikia maombo yake - Yn. 11:41.

Kwa kuwa Mungu aliyafunua mapenzi yake kwa watoto wachanga - (wanyenyekevu) - Mt. 11:25.

### Viumbe Vya Mbinguni Humshukuru Mungu Daima:

Kwa kuwa Mungu ndiye Muumba wa vyote - Ufu. 4:9-11.  
Kwa kuwa anastahili kutukuzwa na kutolewa shukrani - Ufu. 7:11, 12.  
Kwa sababu ya uweza wake - Ufu. 11:16, 17.  
Kwa sababu ya ukombozi katika Kristo - Ufu. 5:9-14.

Kutoa Shukrani kunapaswa Kufanywa:

Kwa Mungu katika Kristo - Rum. 1:8; Kol. 3:17; Ebr. 13:15.  
Kwa Kristo - 1 Tim. 1:12.  
Katika jina la Kristo - Efe. 5:20.  
Tumwabudupo Mungu nyumbani mwetu - Dan. 6:10.  
Katika mikutano ya hadhara - Zab. 35:18.  
Kwa kila jambo, maana hayo ni mapenzi ya Mungu - 1 The. 5:18.  
Kila wakati - Efe. 1:16; 5:20; 1 The. 1:2.  
Wakati tuukumbukapo Utakatifu wa Mungu - Zab. 30:4; 97:12.  
Pamoja na maombezi - 1 Tim. 2:1.  
Pamoja na kusali na kuomba - Flp. 4:6; Kkol. 4:2.  
Kabla ya kula - Yn. 6:11; Mdo. 27:35.  
Bila kukoma - Kol. 2:7.

Watakatifu (Watu Wa Mungu) Hutoa Shukrani Kwa Sababu Ya:

Wema wa Mungu - Zab. 106:1; 107:1; 136:1.  
Fadhili za Mungu ambazo ni za milele - Zab. 136:1-3.  
Kristo - “Kipawa tusichoweza kukisifu kama ipasavyo” - 2 Kor. 9:15; Rum. 8:32.  
Wokovu kutoka utumwani katika Kristo - Rum. 7:24, 25.  
Ushindi juu ya mauti - 1 Kor. 15:57.  
Uongozi wa Mungu - 2 Kor. 2:14.  
Wale waitiio Injili - Rum. 6:17.  
Uwezo mkuu wa Neno la Mungu - 1 The. 2:13.  
Neema Wakristo waliyopewa - 1 Kor. 1:4; Kol. 1:3-5.  
Imani ya Wakristo - Rum. 1:8.  
Bidii ya moyo - 2 Kor. 8:16.  
Furaha ya kuwageuza watu wanwelekee Mungu - 1 The. 3:9.  
Ushirikiano wa ndugu - Mdo. 28:15.  
Mahitaji ya mwili - Rum. 14:6, 7; 1 Tim. 4:4, 5.  
Ushirika katika kuieneza Injili - Flp. 1:3-5.

Kuacha Kutoa Shukrani Ni Dhambi:

Wamkataao Mungu hawamshukuru - Rum. 1:21.  
Wengine huacha kutoa shukrani ingawaje Mungu huwapa yaliyo mema - Lk. 6:35.

Wenye ukoma tisa waliacha kutoa shukrani - Lk. 17:11-19.

### **Sikukuu (Karamu Na Sherehe)**

#### Sikukuu Za Wayahudi:

Pasaka - - siku kuu ya mikate isiyotiwa chachu. Ilikuwa ukumbusho wa kuokolewa kwa wana wa Israeli (Wayahudi) kutoka utumwani nchini Misri - Kutoka 12:1-20; 13:6-10; Luka 22:15; Marko 14:12-16; Yn. 2:13; 6:14; 11:55; 13:1.

Pentekoste - - siku kuu ya mavuno (malimbuko) au “sikukuu ya majuma” - Kut. 23:16; Law. 23:15-21; Hes. 28:26; Kum. 16:16; Mdo. 2:1; 20:16; Law 23:33-36; Kum. 16:13-17; Yn. 7:2.

Siku ya kupiga tarumbeta - Hes. 29:1; Law. 23:24.

Sikukuu ya Upatanisho - Law. 23:26-31; Kut. 30:10; Ebr. 9:7-28.

Siku ya karamu na furaha - - sikukuu ya kupelekeana zawadi - - katika ukumbusho wa kuokolewa kwa Wayahudi katika siku za Esta - Esta 9:17-28 (Yaani sikukuu za Puri).

Wengine wanapenda giza kwa kuwa matendo yao ni maovu - Yn. 3:19.  
Kwa sababu ya matendo maovu, Kaini alimuua nduguye - 1 Yoh. 3:12.  
Wanadamu ni adui za Mungu kwa sababu ya matendo yao Maovu - Kol. 1:21.  
Mtu asipomsamehe ndugu yake ni mwovu - Mt. 18:32.  
Mtu mvivu ni mwovu - Mt. 25:26.  
Kujitukuza ni uovu - Yak. 4:16.  
Maneno maovu hutoka katika moyo mbovu - Mt. 12:33-37; Luka 6:45.  
Maovu yote hutoka moyoni - Marko 7:21-23.  
Uovu hutokana na tamaa mbaya - Yak. 1:13-15.  
Watu wabaya watazidi kuwa waovu - 2 Tim. 3:13.

#### Msamaha Wa Waovu:

Mungu alimtuma Yesu awaondoe watu maovuni - Mdo. 3:26.  
Yesu aliwaokoa na dunia hii mbovu iliyopo sasa - Gal. 1:14.  
Waovu wanapaswa kuacha kutenda mabaya - Isa. 1:16.  
Wakiacha kutenda dhambi wataishi - Eze. 33:11-15.  
Dhamiri mabaya huoshwa kwa damu ya Yesu - Ebr. 10:22.

#### Wakristo Hawapaswi Kutenda Maovu:

Vita vyetu ni juu ya pepo wabaya wa ulimwengu huu - Efe. 6:10-17.  
Hawapaswi kunena maovu - Efe. 4:29, 31; 1 Pet. 3:10.  
Wanapaswa kustahimili watendewapo maovu - 1 Pet. 2:20-23; 3:9.  
Hawapaswi kutamani mambo maovu - 1 Kor. 10:6.  
Katika uovu wanapaswa kuwa watoto wachanga - 1 Kor. 14:20.  
Wanapaswa kuweka mbali ubayo uzidio - Yak. 1:21.  
Wanapaswa kuweka mbali uovu wote - 1 Pet. 2:16.  
Hawapaswi kuwa na moyo mbovu wa kutokuamini kwa kujitenga na Mungu - Ebr. 3:12.  
Wanapaswa kulichukia lilio ovu - Rum. 12:9.  
Wanapaswa kuushinda ubaya kwa wema - Rum. 12:21.

### **Upendo**

#### Upendo Wa Mungu Kwa Wanadamu:

Mungu ni Upendo - 1 Yoh. 4:7, 8.  
Ni kwa watu wote - Yn. 3:16.



Ni kwa watu wasiostahili pendo lake - Rum. 5:8; Mt. 5:45; 1 Yoh. 4:10.  
Ni pendo lenye wingi wa rehema - Efe. 2:4.  
Ni pendo lenye kujitoa - 1 Yoh. 4:9, 10; Yn. 3:16.  
Huwaletoa watu wokovu na utakaso - 2 The. 2:13.  
Hutuwezesha kuwa washindi - Rum. 8:37  
Wakati mwingine linaweza kuadhibu - Ebr. 12:6.

#### Upendo Wa Wanadamu Kwa Mungu:

Unapaswa kuwa upendo unazidi vitu vyote - Mt. 6:24.  
Hii ni amri iliyo ya kwanza na kuu - Mt. 22:37-39.  
Hutokana na shukrani - Lk. 7:42, 47.  
Ni mtiifu - Yn. 14:15, 21, 24; 1 Yoh. 2:5.  
Huimarika kwa kuwasaidia wengine - 1 Yoh. 4:12, 20; 3:14.

#### Upendo Wa Wanadamu Kwa Wengine:

Mambo yote yanapaswa kutendeka katika upendo - 1 Kor. 16:14.  
Mkristo anapaswa kuenenda katika upendo - Efe. 5:2  
Anapaswa kuufuata upendo - 1 Kor. 14:1.  
Upendo hulijenga na hulikuza kanisa - Efe. 4:16.  
Nia ya viongozi kanisani inapaswa kuwa ya upendo - 2 Kor. 12:15; 1 Tim. 4:12; 2 Tim. 3:10.  
Wakristo wanapaswa kuwapenda viongozi wao - 1 The. 5:13.  
Upendo unapaswa kuanzia nyumbani - Efe. 5:25, 28, 33; Tito 2:4.  
Unapaswa kuwa upendo kwa ndugu wote - 1 Pet. 1:22; 2:17.  
Unapaswa kuwafikia jirani zetu - Lk. 10:27; Rum. 13:9-10.  
Unapaswa kuendelea hata kwa adui zetu - Lk. 6:27, 28; Mt. 5:44.

#### Tabia Za Upendo Wa Kikristo:

Pendo lisilo na unafiki - Rum. 12:9; 1 Pet. 1:22.  
Halimfanyii jirani neno baya - Rum. 13:10.  
Hudhihirika kwa matendo mema - Ebr. 6:10; 1 Yoh. 3:18.  
Kuvumilia - 1 Kor. 13:4; Efe. 4:2.  
Husamehe - 2 Kor. 2:8.  
Wakati mwingine hukemea - 2 Kor. 2:4.  
Huongoza kwa uhuru - Gal. 5:13; Rum. 14:5.  
Hutufanya tuishike kweli - Efe. 4:15.  
Hutubidisha - 2 Kor. 5:14.  
Upendo ni kifungo cha ushirika wa Kikristo - Flp. 2:2; Kol. 2:2.  
Pendo ndilo ulimilifu wa sheria - Rum. 13:10.  
Ni kifungo cha ukamilifu - Kol. 3:14.  
Ni tunda la Roho - Gal. 5:22.

Ni kithibitisho cha ufuasi wetu - Yn. 13:34, 35.  
Pendo ni kuu kuliko mambo yote - 1 Kor. 13:13.

#### Upendo Unaweza Ukatumiwa Vibaya:

Pendo la dunia - 1 Yoh. 2:15-17; 2 Tim. 4:10.  
Kujipenda mwenyewe - 2 Tim. 3:2.  
Kupenda utukufu wa wanadamu - Yn. 12:42, 43; Lk. 11:43.  
Kupenda giza - Yn. 3:19.

### **Urafiki wa Dunia**

#### Mungu Anachukizwa Na Watu Wanaofanya Urafiki Na Ulimwengu.

Rafiki ya ulimwengu ni adui wa Mungu - Yak. 4:4.  
Usiupende ulimwengu - 1 Yoh. 2:5.

#### Mungu Atauhukumu Ulimwengu.

Atauhukumu ulimwengu - Zab. 9:8.  
Wote wanaoishi ulimwenguni ni lazima wamwogope Mungu - Zab. 33:8.  
Atauhukumu ulimwengu kwa haki - Zab. 98:9; Mdo. 17:31.  
Mungu atauadhibu ulimwengu kwa uovu wake - Isa. 13:11.

#### Mungu Anataka Watu Wa Ulimwengu Wawe Wenye Haki.

Mungu anajiandaa kwa watu wanaomsibili yeye - Isa. 64:4.

### **Usemi**

#### Uwezo Wa Usemi:

Kuna wakati wa kunena na wakati wa kunyamaza - Mhu. 3:7.  
Uwezo wa uzima na mauti u katika ulimi - Mit. 18:21.  
Mtu huyanena yaujaza moyo wake - Mt. 12:34.  
Azuiaye kinywa chake na ulimi wake hujilinda nafsi yake - Mit. 21:23.  
Maneno yapendezayo ni kama sega la asali, ni tamu nafsini - Mit. 16:24.  
Usemi wa mtu humtambulisha - Mt. 26:73.  
Musa alikosa kuingia nchi ya Kanaani kwa sababu alisema yasiofaa kwa midomo yake - Zab. 106:33.  
Vitokavyo kinyvani ndivyo vimtiavyo mtu unajisi - Mt. 15:18.  
Wanadamu watatoa hesabu ya kila neno walinalo lisilo maana - Mt. 12:36.  
Kwa maneno yake mtu huhesabiwa haki au huhukumiwa - Mt. 12:37.

Yeyote amkufuruye Roho Mtakatifu hatasamehewa - Mt. 12:32.

Watu Wa Mungu Hawapaswi Kusema:

Maneno laini na ya kujipendekeza (ya udanganyifu) - Rum. 16:18; Mit. 29:5.  
Mabaya wala hila - 1 Pet. 3:10.  
Neno lolote lililo ovu - Efe. 4:29; Kol. 3:8.  
Maneno ya kudanganyana - Kol. 3:9; Yak. 4:11.  
Maneno ya upuzi wala ubishi - Efe. 5:4; 1 Tim. 5:13.  
Ushuhuda wa uongo na kukufuru - Mt. 15:18; Mit. 6:19; 19:9; 25:18.  
Laana - Yak. 3:9; Mit. 20:20.  
Maneno ya kuapa - Yak. 5:12.  
Maneno ya kusingizia - 1 Tim. 3:11; tito 3:2.  
Maneno ya uongo - Mit. 6:17; 12:22; 14:5; 17:4; Efe. 4:25.  
Maneno ya kupanda mbegu za fitina kati ya ndugu - Mit. 6:19; 17:9.  
Maneno ya uchongezi - Mit. 18:8; 11:13; 20:19; 26:20; 1 Tim. 5:13.  
Maneno ya ghadhabu (hasira) - Mit. 15:1, 18; 16:32; 29:22; Yak. 1:19, 20.

Bali Usemi Wa Wakristo Unapaswa Kuwa Wa:

Maneno ya kweli na kiasi - Mdo. 26:25.; Efe. 4:25.  
Neno la Mungu pasipo hofu - Flp. 1:14.  
Maneno mema yawezayo kuwajenga watu - Efe. 4:29.  
Maneno yawezayo kuwatia nguvu walio dhaifu - 1 The. 5:14.  
Maneno yawezayo kuwafariji wenye huzuni - 1 The. 4:17.  
Maneno yenye neema siku zote - Kol. 4:6.  
Maneno yenye uzima yasioweza kuhukumiwa makosa - Tito 2:8; Mit. 12:18.  
Kutoa shukrani - Efe. 5:4; Yak. 3:9.  
Maneno yasiyo na manung'uniko wala mashindano - Flp. 2:14.  
Upole na hofu - 1 Pet. 3:15.  
Kielelezo kwao waaminio - 1 Tim. 4:12.

**Ustahimilivu (Saburi, Uthabiti)**

Mifano Ya Watu Wastahimilivu:

Ayubu - Yak. 5:11.  
Musa - Ebr. 11:27.  
Paulo, kwa ajili ya wateule - 2 Tim. 2:10.  
Yesu aliustahimili msalaba - Ebr. 12:2, 3.

Ustahimilivu (Uthabiti) Ni Kitu Cha Maana Katika Maisha Ya Watoto Wa Mungu:

Huzaa matunda kwa uvumilivu - Lk.k 8:15.  
Huishi maisha ya subira - Lk. 21:19.  
Kwa saburi, wao hukaa katika tumaini - Rum. 15:4.  
Hungojea kwa saburi - Rum. 8:25.  
Hupiga mbio kwa saburi katika mashindano yaliyowekwa mbele yao - Ebr. 12:1.  
Wana saburi katika kutenda mema - Rum. 2:7.  
Wanapaswa kuifuata saburi - 1 Tim. 6:11; 2 Tim. 3:10.  
Wanapaswa kuzidisha saburi katika maisha yao - 2 Pet. 1:6.  
Kristo anajua sabira yao - Ufu. 2:2, 3, 19.

Wakristo Wanapaswa Kuwa Wastahimilivu (Wenye Saburi) Katika Mateso Na Majaribu:

Wanapojaribiwa - Yak. 1:12.  
Wateswapo kwa sababu ya matendo yao mema - 1 Pet. 2:20.  
Katika dhiki - Rum. 12:12.  
Katika mashindano makubwa ya maumivu - Ebr. 10:32.  
Katika adha na dhiki - 2 The. 1:4.  
Dhiki huleta saburi - Rum. 5:3.  
Kujaribiwa kwa imani huleta saburi - Yak. 1:2-4.

Thawabu Ya Walio Wastahimilivu:

Wana heri - Yak. 5:11.  
Wataokoka wakati wa mwisho - Mt. 10:22; Mk. 13:13; Mt. 24:13; 2 Tim. 2:12.

**Utajiri (Mali)**

Mali Hutoka Kwa Mungu:

Baraka za Mungu hutajirisha - Mit. 10:22.  
Mali ni taji ya wenye hekima - Mit. 14:24.  
Mungu hutoa nguvu za kupata utajiri - Kum. 8:17, 18; Mhu. 5:19; 6:2; Mwa. 13:2; Zab. 112:1-3; 1 Tim. 6:17.

Lakini Wanadamu Wameonywa Juu Ya Utajiri Wa Dunia:

Hawapaswi kujifaidisha kwa mali za hila - Mit. 22:16; 28:6, 20; 21:6; Amosi 2:6, 7; 5:11, 12; 8:4-6; Yoeli 3:3; Law. 19:36; Kum. 25:13-16; Lk. 19:8.  
Hawapaswi kusahau kwamba mali hutoka kwa Mungu - Kum. 8:17; Hos. 2:8.  
Hawapaswi kuzitegemea mali zao - Mit. 11:28; Zab. 52:7; 1 Tim. 6:17; Mk. 10:23-27.  
Hawapaswi kuutumainia utajiri kuliko mambo ya Kiroho - Mit. 23:4, 5; 15:27; Lk. 12:21; Ufu. 3:17.  
Hawapaswi kusahau kwamba mali ya kunia hii sio ya milele - Mit. 11:4; 23:4, 5; 27:24; 1 Tim. 6:17; Lk. 12:13-21; 1 Tim. 6:6-10.

“Udanganyifu wa mali” - Mt. 13:22; Lk. 18:22, 23.

Sifa njema ni bora kuliko mali nyingi - Mit. 22:1, 2; 13:7; Lk. 12:20, 21.

Wanapaswa kuridhika na walivyo navyo - 1 Tim. 6:8; Ebr. 13:5; Flp. 4:11, 12; Mit. 30:8, 9.

### Wajibu Wa Wenye Mali

Kutoa kuna heri kuliko kupokea - Mdo. 20:35; 2 Kor. 8:9.

Changizo kwa watakatifu maskini - 1 Kor. 16:1, 2; 2 Kor. 8:9.

Watende mema na mali zao - 1 Tim. 6:17-19.

Wawe waaminifu kwa mali zao - Lk. 16:9-11.

Wanapaswa kujiwekea hazina mbinguni - Mt. 6:19-21; Lk. 12:33; 1Tim. 6:19.

### Utajiri Wa Neema Na Baraka Za Mungu:

Utajiri wa neema yake - Efe. 2:7; 1 Kor. 1:27; 2:2, 3; Flp. 4:19.

Utajiri wa kweli ni wa Kiroho:

1. Utajiri wa milele mbinguni - Lk. 12:33; Mt. 6:20; 19:21.
2. Mali ya kweli - Lk. 16:11.
3. Tajiri mbele za Bwana - Ufu. 2:9.
4. Matajiri wa imani - Yak. 2:5.
5. Tukitajirisha wengi - 2 Kor. 6:10.

## **Utumwa**

### Utumwa Wa Mwili:

Waisraeli waliokolewa kutoka utumwani nchini Misri - Kut. 20:2; Kum. 4:20; 5:15; 6:21; Zab. 78:105.

Israeli alikuwa na watumwa nchini Kanaani - Kut. 21:1-11; Law. 25:35-46; Kum. 15:12-15.

Ukristo haukuuamamiza utumwa wa mwili kwa kutumia nguvu (kulazimisha) au ujeuri bali kwa mafundisho yaliyoibadilisha mioyo ya watu - Efe. 6:5-9; Kol. 3:22; 4:1; 1 Tim. 6:1, 2; Filemoni 8-21.

### Kuna Utumwa Mwingine Ambao Ni Wa Kutisha Sana:

Watumwa wa dhambi - Yn. 8:34; Rum. 6:16.

Wale walio katika utumwa wa Shetani kwa hofu ya mauti - Ebr. 2:14, 15.

Mtego wa Ibilisi - 1 Tim. 3:7; 2 Tim. 2:26.

Kuwa katika uchungu kama nyongo na kifungo cha uovu - Mdo. 8:23.

Watumwa wa Miungu wa uongo - Gal. 4:8.

Watumwa wa mapokeo ya ulimwengu - Gal. 4:3.

Watumwa wa uharibifu - 2 Pet. 2:19.

Watumwa wa tamaa na anasa za namna nyingi - Tito 3:3.

Waalimu wa uongo hutafuta kuwatia Wakristo utumwani - Gal. 2:4.

Yesu Kristo Alikuwa Ili Awe Fidia (Ukombozi) Kwa Wale Walio Chini Ya Utumwa Wa Dhambi:

Kulingana na Maandiko Masihi (Kristo) alikuwa aje kuwaweka watu huru - Isa. 61:1, 2; 42:6, 7.  
Yesu Kristo aliyatimiza Maandiko haya - Lk. 4:18-21; Yn. 8:36; Efe. 4:8.  
Yesu, kwa kujitoa mwenyewe, alitwaa namna ya mtumwa - Flp. 2:7.  
Kristo alituletea uhuru - Gal. 5:2; Yn. 8:36.  
Kristo huwaweka huru mateka kwa Neno la Kweli - Yn. 8:32; Rum. 8:2.  
Wakristo wamewekwa huru mbali na utumwa wa dhambi - Rum. 6:18, 22.  
Wakristo hawapokei roho ya utumwa iletayo hofu - Rum. 8:15.

Kwa Hiyo, Wale Waliofidiwa Ni Watumwa Wa Mungu:

Wakiisha kununuliwa na Mungu, Wakristo wote ni watumwa wake - 1 Kor. 6:19, 20; Ufu. 1:5, 6; 2:20; 7:3; 22:3.

Wao ni watumwa wa:

- 1) Mungu - Rum. 6:22.
- 2) Kristo - Yn. 13:13-16.
- 3) Watu wengine - Flp. 2:5-9; Mt. 20:27; Mk. 10:44.

Wajumbe (wale watumwao) wa Kristo kama watumwa wake - 2 Kor. 4:5; Gal. 1:10; Yak. 1:1; 2 Pet. 1:1; Ufu. 1:1.

**Uvivu**

Uvivu Humfanya Mtu Kuwa Katika Hali Mbaya Ya Maisha.

Umaskini - Mit. 6:9-11.  
Uharabu - Mit. 18:9.  
Vitapotea vitu vyote - Mat. 25:26-30.

Onyo La Upole Kinyume Cha Kuwa Mvivu.

Tumia muda nzuri - Efe. 5:16.  
Fanya kazi kwa bidii - Neh. 6:3.  
Fanya kazi usiku na mchana - 1 Thes. 2:9.  
Jali Chungu - Mit. 6:6-8.  
Usipofanya kazi, basi huli - 2 The. 3:10-12.

**Uvumilivu**

Mungu ni Mvumilivu:

Kwa sababu hii, anataka watu wapate kutubu - Rum. 2:4; Eze. 18:23, 32.  
Anataka kila mtu aokolewe - 2 Pet. 3:9, 15.  
Huudhihirisha uvumilivu wake katika kuzisamehe dhambi - Rum. 3:25.

### Mifano Ya Uvumilivu Wa Mungu:

Katika Siku za Nuhu - 1 Pet. 3:20.  
Kwa Waisraeli - Zab. 78:38; Isa. 48:9.  
Watu wa Yerusalemu - Mt. 23:37.  
Kwa Paulo - 1 Tim. 1:12-16.

### Watu Wa Mungu Pia Wanapaswa Kuwa Wavumilivu:

Kwa kuwa Mungu alikuwa mvumilivu kwao - Mt. 18:21-35.  
Kama wateule wa Mungu, wao hujivika uvumilivu - Kol. 3:12; Efe. 4:2.  
Wanapaswa kuwa na mwenendo wa uvumilivu - 2 Tim. 3:10.  
Wanapaswa kuwa na mwenendo wa uvumilivu - 2 Tim. 4:2.  
Wanapaswa kuwa wavumilivu kwa watu wote - 1 The. 5:14.  
Upendo huvumilia - 1 Kor. 13:4.  
Ili waweze kuzirithi ahadi kwa imani na uvumilivu - Ebr. 6:12.  
Wavumilie hata kuja kwake Bwana - Yak. 5:7-10.  
Ni tunda la Roho - Gal. 5:22.

## **Uzima Wa Milele**

### Uzima Wa Milele Kufuatana Na Ahadi Ya Mungu:

Ni ahadi ya Mungu - Tito 1:2; 1 Yoh. 2:25.  
Ni kipawa cha Mungu - Rum. 6:23; 1 Yoh. 5:11.  
Atakayeichukia nafsi yake katika ulimwengu huu ataiponya katika uzima wa milele - Yn. 12:25.  
Adumuye katika kutenda mema atapata uzima wa milele - Rum. 2:6, 7.  
Mwisho wa kutakaswa ni uzima wa milele - 1 Yoh. 3:15.  
Wakristo wanapaswa kuushika uzima wa milele - 1 Tim. 6:12.  
Wengine hujiona nafsi zao kuwa hawastahili uzima wa milele - Mdo. 13:46.

### Uzima Wa Milele Hupatikana Kwa Njia Ya Kristo Tu:

Yeye hutoa maji ya uzima wa milele - Yn. 14:14.  
Yeye ndiye chakula cha uzima wa milele - Yn. 6:27, 54.  
Maneno yake ni ya uzima wa milele - Yn. 6:68.  
Yeye hutoa uzima wa milele - Yn. 17:2, 3.  
Yenye ndiye uzima wa milele - 1 Yoh. 5:20.  
wale wamwaminio Yesu Kristo ndio wanaopewa uzima wa milele - Yn. 3:16; 5:24.  
Wale wanaomtii wanao uzima wa milele sasa - Ebr. 5:9.  
Wale wayasikiao maneno ya Kristo, Na kumfuata wanao uzima wa milele - Yn. 10:27, 28.

## **Uzinzi (Uasherati)**

### Wakristo Hawapaswi Kufanya Uzinzi:

Kwa kuzuia uzinzi, kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe - 1 Kor. 7:2.  
Ye- yote amwachaye mkewe, isipokuwa kwa uasherati amfanya kuwa mzinzi - Mt. 19:9; 5:32.  
Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya kama vile uzinzi na uasherati - Mt. 15:19; Marko 7:21-22.  
Mwili si kwa zinaa - 1 Kor. 6:13.  
Msishrikiane na wazinzi - 1 Kor. 5:9-11.  
Kanisa halipaswi kushrikiana na wazinzi - 1 Kor. 5:1-13.  
Epukana na uasherati - 1 The. 4:3.  
Ikimbieni zinaa - 1 Kor. 6:18.  
Fisheni (yaani acheni) uasherati - Kol. 3:5.  
Wala tusifanye uasherati - 1 Kor. 10:8.  
Wengine hawautubii uasherati wao - 2 Kor. 12:21; Ufu. 9:21.

### Adhabu Ya Wazinzi:

Mungu atawahukumu wazinzi na waasherati - Ebr. 13:4.  
Wazinzi na waasherati hawataurithi Ufalme wa Mungu - 1 Kor. 6:9-10; Gal. 5:19-21.  
Hawatauingia Mji Mtakatifu - Ufu. 22:15.  
Watapata sehemu yao katika ziwa liwakalo moto na kiberiti - Ufu. 21:8.

## **Vipawa (Karama)**

### Kila Kipawa Chema Au Kilicho Kamili Hutoka Kwa Mungu:

Vipawa vyema hutoka juu, hushuka kwa Baba asiyebadilika - Yak. 1:17.  
Hutoa mvua na nyakati za mavuno hata kwa wasio haki - Mdo. 14:17; Mt. 5:45.  
Huwapa watu wake mahitaji yao ya kimwili - Mt. 6:25-34.  
Huwapa wale wamwombao na watafutao, na huwafungulia wabishao - Mt. 7:7-9.  
Huwapa mema wao wamwombao - Mt. 7:11.  
Hutukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa - 2 Pet. 1:3.  
“Maji yaliyo hai” ni kipawa cha Mungu - Yn. 4:10-14.  
Wokovu ni kipawa cha Mungu - Efe. 2:8, 9.  
Wakristo wamekionja kipawa cha mbinguni - Ebr. 6:4.  
Huwapa hekima wao waombao kwa imani - Yak. 1:5-8.  
Huwapa wanyenyekevu neema izidiyo - Yak. 4:6.  
Huwapumzisha waliolemewa - Mt. 11:28; Ufu. 14:13.

### Yesu Kristo Ndiye Kipawa kikuu Cha Mungu:

Ametolewa awe agano la watu, na nuru ya mataifa - Isa. 42:6.



Mungu hukuacha kumtoa Mwana wake mwenyewe - Rum. 8:32.  
Alimtoa Mwanawe kwa sababu ya upendo - Yn. 3:16.  
Kristo alitolewa awe kipatanisho kwa dhambi zetu - 1 Yoh. 4:10.  
Yeye ni mkate uliyo hai uliotolewa kutoka mbinguni - Yn. 6:27, 50, 51.  
Kipawa cha Mungu ni uzima wa milele katika Kristo - Rum. 6:23.  
Yeye ni kipawa cha Mungu “kisichosemekana” - 2 Kor. 9:15.

#### Roho Mtakatifu Hutolewa Kwa Wale Wanaomtii Mungu:

Baba huwapa Watoto wake Roho Mtakatifu - Luka 11:13; 1 The. 4:8.  
Waamini waliobatizwa wenye toba ya kweli hupokea Roho Mtakatifu kama kipawa - Mdo. 2:38.  
Hutolewa kwa wote wamtii Mungu - Mdo. 5:32.  
Hutumwa mioyoni mwao kwa kuwa wao ni watoto wake - Gal. 4:6.  
Kwa njia ya Roho Mtakatifu pendo la Mungu humiminwa Mioyoni mwao - Rum. 5:5.

### **Vipawa Vya Mungu**

#### Vipawa Vya Maisha Ya Duniani:

Mvua nyakati za mavuno (matunda) - Law. 26:4, 5; Isa. 30:23; Mdo. 14:17.  
Vitu vyote vilivyo vyema - Zeb. 34:10; 1 Tim. 6:17; Yak.1:17.  
Vyakula na mavazi - Mt. 6:25-33.  
Tunapaswa kuomba tupate chakula chetu cha kila siku - Mt. 6:11.  
Tunapaswa kukumbuka kwamba vitu vyote hutoka kwa Mungu - Kum. 8:7-20.  
Tunapaswa kutoa shukrani kila mara - 1 Tim. 2:1; Flp. 4:6; 1 The. 5:18.

#### Vipawa Vitakatifu Vyenye Asili Ya Kiroho:

Yesu Kristo - Yn. 3:16; 4:10; 6:32, 33; 2 Kor. 9:15.  
Roho Mtakatifu - Mdo. 2:38; 5:32; Luka 11:13.  
Neema - Yak. 4:6; 1 Pet. 5:5.  
Toba - Mdo. 11:18; Rum. 2:4.  
Raha - Mt. 11:28; 2 The. 1:7; Ufu. 14:13.  
Hekima - Mit. 2:9; Yak. 1:5.  
Utukufu - Zab. 84:11; Yn. 17:22.  
Uzima wa milele - Yn. 6:27; Rum. 6:23.  
Mambo yote - Rum. 8:32.

### **Vyombo Vya Muziki**

Vyombo viliundwa na mstari wa Kaini (mstari wa kimwili) - Mwa. 4:21.  
Katika sheria ya Kwanza ambayo iliondolewa Daudi alikuwa baba wa vyombo vya muziki - Amosi 6:5.

Lakini Mungu aliona muziki huo kuwa ni “kelele,” - Amosi 5:23.

Katika sheria mpya tumeamuriwa kuimba na vyombo ambavyo Mungu aliviumba, SAUTI ZETU - Efe. 5:19; Kol. 3:17; Mdo. 16:25; Rum. 15:9.

### **Waangalizi (Wazee)**

#### Waangalizi (Maaskofu), Wazee, Na Wachungaji Ni Mamoja:

Mdo. 20:17-28.

“Akawiate “wazee” wa kanisa” - (mst. wa 17).

Hawa wameitwa “waangalizi” - (katika mst. wa 28).

“Kulilisha” (kazi ya wachungaji) kanisa - (mst. 28).

1 Pet. 5:1, 2:

“Wazee walio kwenu” - (mst. 1).

“Lichungeni kundi” la Mungu lililo kwenu - (mst. 2).

“Na kulisimamia” (mst. 2).

Tito 1:5-7:

“Na kuweka wazee katika kila mji” - (mst. 5).

“Maana imempasaa skofu awe mtu asiyeshtakiwa” - (mst. 7).

“Kwa kuwa ni wakili wa Mungu” - (mst. 7).

#### Kulikuwako Na Wingi Wa Wazee Au Waangalizi (Maaskofu) Katika Kanisa Moja:

“Walipokwisha kuwachagua wazee katika kila kanisa” - Mdo. 14:23.

“Wakawapelekea wazee” - Mdo. 11:30.

“Na awaite wazee wa kanisa” - Yak. 5:14.

“Akawaita wazee kanisa” - Mdo. 20:17.

“Pamoja na Maaskofu na Mashemasi” - Flp. 1:1.

“Kwa kuwekewa mikono ya wazee” - 1 Tim. 4:14.

“Wazee walio kwenu” - 1 Pet. 5:1.

**Tafadhali Kumbuka:** Hakuna mahali popote ambapo Mungu alimweka mzee mmoja au mchungaji mmoja (pasta) juu ya makundi mengi.

#### Kazi Ya Waangalizi Wa Kanisa:

Huliangalia kundi la Mungu - Mdo. 20:28.

Kama mawakili wa Mungu, huwatunza watu wake - Tito 1:7; Tafadhali angalia Ebr. 13:17.

Hulichunga kundi la Mungu kama wachungaji - 1 Pet. 5:2; Mdo 20:28.

Huwakemea waalimu wa uongo - Tito 1:9.

Huwaonya Wakristo kila mara wasije wkapotea - Tito 1:9.

#### Wajibu Wa Kanisa Kwa Wazee Wake:

Kanisa linapaswa kuwatambua na kuwaheshimu wazee - 1 The. 5:12, 13.  
Linapaswa kuuiga mwenendo wao wa maisha - Ebr. 13:7.  
Linapaswa kuwatii na kuwanyenyekea - Ebr. 13:17.  
Linapaswa kuwahesabiu kuwa wana stahili heshima maradufu - 1 Tim. 5:17, 18.  
Halipaswi kukubali mashtaka juu ya wazee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watutu - 1 Tim. 5:19.  
Wale wadumuo katika kutenda dhambi liwakemee mbele ya wote - 1 Tim. 5:20.

Sifa Zitakiwazo Kwa Waangalizi Wa Kanisa: (Soma Kwa Uangalifu Maandiko Yafuatayo):

1 Tim. 3:1-7.  
Tito 1:5-9.  
1 Pet. 5:1-3.

**Tafadhali Kumbuka:** Kanisa linapaswa kufundisha kwa ukamilifu tabia za wazee kulingana na Biblia halafu liangalie na kuchagua kutoka kati ya Wakristo wale ambao wana tabia za wazee wa kanisa na wale wanataka kazi hiyo. Uchaguzi huu ufanywe na kanisa lote likisaidiana na mhubiri au wahubiri - Tafadhali kumbuka Mdo. 14:23; 6:1-6; 20:28; 1 Tim. 3:1-7; Tito 1:5-9. Wale wasio na tabia zinazolingana na neno la Mungu hawapaswi kuchaguliwa!

**Waalimu wa Uongo**

Waalimu Wa Uongo Wanatafuta Mambo Yao.

Wanatafuta njia yao ili wafanikiwe - Isa. 56:10-12.  
Walimu wa uongo wanajilisha wenyewe tu - Eze. 34:2-3.  
Wanatafuta mshahara tu - Yn. 10:12.  
Wanatafuta mambo bila faida - Yer. 2:8.  
Wanafundisha kwa pesa - Tit. 1:11.

Waalimu Wa Uongo Wanaharibu Kundi La Bwana.

Wanatawanya kondoo za Bwana - Yer. 23:2.  
Wanapoteza watu wa Mungu - Yer. 50:6.  
Wanafanya wafuasi wao wawe bure - Yer. 23:16.  
Watadanganya wengi - Mat. 24:11.

Tuwe Macho Waalimu Wa Uongo Watakuja.

Mwalimu wa uongo ni mkia - Isa. 9:15.  
Mwalimu wa Uongo ni mtu pumbavu - Hos. 9:7.  
Watavaa nguo ya kondoo - Mat. 7:15.  
Tujiandae watakuja na nguvu nyingi - Mk. 13:22-23.  
Roho wa Mungu anasema watafika - 1 Tim. 4:1.

Wanakiburi bila kuelewa kitu - 1 Tim. 6:3.  
Muda utafika wakati watu watafuata walimu wanaopendeza - 2 Tim. 4:3.

#### Tujaribu Mafundisho Ya Watu Wote.

Kama maneno yao siyo ya kweli tusiogope - Kumb. 18:22.  
Hawaelewi maneno yao - 1 Tim. 1:7.  
Tuwajaribu walimu wote - 1 Yoh. 4:1.  
Tuthibitis he mambo yote - 1 The. 5:21; Efe. 5:8-10; 2 Kor. 13:5.

#### Tuwache Waalimu Wa Uongo Walaniwa Peke Yao.

Mungu hataki mtu ambaye anaota ndoto - Kumb. 13:5.  
Wazazi hawatakiwa kusikia mtoto wao kuwa ni mwalimu wa uongo - Zek. 13:3.  
Wataangamiza haraka - 2 Pet. 2:1.  
Watalaniwa - Gal. 1:6-9.

### **Wajibu wa Wazazi**

#### Wajibu Maalum Wa Wazazi

Kufundisha sheria ya Mungu - Kumb. 6:7; Kumb. 4:9; Kumb. 31:13; Isa. 28:9; Yn. 21:5.  
Mlee mtoto katika njia ya Mungu - Mith. 22:16.  
Kutunza watoto - 2 Nya. 12:14.  
Msiwachokoze - Efe. 6:4.  
Kuthibiti - 1 Tim. 3:4.  
Kupenda - Tit. 2:4.  
Tia adhabu - Mith. 13:24; 19:18; 22:15; 23:13.

### **Kazi Za Wanawake**

Mt. 28:19, 20 - Anatakiwa kupeleka injili kila mahali.  
Mdo. 18:26 - Kusaidiana na mumewe ili apeleka injili.  
1 Tim. 2:10 - Kutenda matendo mema.  
2 Tim. 1:5 - Atunza watoto wake na kufundisha njia za Mungu.  
Tit. 2:3-5 - Wazee wa kike wanatakiwa kuwa na mwenendo matakatifu, na kufundisha vijana wanawake.  
Mit. 31:10-31 - Tunaona orodha na sifa nyingi ya mama mzuri.

### **Washiriki (Viungo)**

#### Viungo Vya Mwili:

Wakristo hawapaswi kuvitoa viungo vyao kwa dhambi - Rum. 6:13.  
Wanapaswa kuvitoa viungo vyao kwa Mungu viwe silaha za haki - Rum. 6:13, 19.

Vita katika viungo kwa sababu ya tamaa mbaya - Yak. 4:1; Rum. 7:23.  
Ulimi ni kiungo kidogo lakini hujivuna majivuno makuu - Yak. 3:5.  
Uasherati huvifanya viungo vya mkristo kuwa vya kahaba - 1 Kor. 6:15.  
Vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi - Kol. 3:5.  
Yafaa kiungo kimoja kipotee wala sio mwili mzima - Kol. 3:5.

#### Viungo Vya Kristo:

Wakristo ni viungo vya mwili wa Kristo - Efe. 5:30; 1 Kor. 6:15.  
Sisi tu viungo, kila mmoja kiungo cha mwenzake - Efe. 4:25; 1 Kor. 12:27.  
Katika mwili mmoja tuna viungo vingi - Rum. 12:4.  
Viungo vyote ni vya muhimu katika mwili wa Kristo - 1 Kor. 12:12-24.  
Viungo vya Kristo vihudumiane - 1 Kor. 12:25, 26.

#### **Watoto**

#### Biblia Inasema Juu Ya Watoto Kwamba:

Wao ni kipawa kitokacho kwa Mungu - Mwa. 33:5.  
Wao ni urithi wa Mungu - Zab. 127:3.  
Wana wa wana ndio taji ya wazee - Mit. 17:6.  
Wao hujijuli sha kwa matendo yao - Mit. 20:11.

#### Madaraka Ya Wazazi Kwa Watoto Wao:

Kuwafundisha neno la Mungu kila Mara - Kum. 6:6-7.  
Kuwafundisha kumcha Mungu - Kum. 31:12-13.  
Kuwafundisha maandiko matakatifu toka utotoni mwao - 2 Tim. 3:15.  
Kuwalea katika njia ipasayo nao hawataia cha hata wakiwa wazee - Mit. 22:6.  
Wanapaswa kuwaadhibu mara wafanyapo makosa - Mit. 13:24; 22:15; 23:13-14; 29:15-17; Ebr. 12:5-9.  
Hawapaswi kuwachokoza watoto wao - Efe. 6:4; Kol. 3:21.  
Wanapaswa kuonyesha mfano mzuri kwa watoto wao - 2 Tim. 1:5.  
Wanapaswa kuwatunza kwa kuwatimizia mahitaji yao - 1 Tim. 5:8.

#### Madaraka Ya Watoto:

Wamkumbuke Muumba wao - Mhubiri 12:1.  
Wamche Bwana - Mit. 24:21.  
Wamtii Mungu - Kum. 30:2.  
Wayasikilize mafundisho ya wazazi wao - Mit. 1:8, 9.  
Wawaheshimu wale waliowazaa - Efe. 6:2; Ebr. 12:9.  
Wawaheshimu wale waliowazaa - Efe. 6:2; Ebr. 12:9.  
Washike maagizo ya wazazi - Mit. 6:20; Efe. 6:1; 3:20.  
Wawatunze wale waliowazaa - 1 Tim. 5:4.

Wasifuata mfano mbaya wa wazazi wao - Ezeieli 20:18.

Watoto Waovu:

Huwadharau wazazi wao - Mit. 15:5, 20.

Humlaani baba yao - Mit. 30:11.

Huwaaibisha wazazi wao - Mit. 19:26.

Ni msiba kwa wazazi wao - Mit. 19:13.

Huwahuzunisha wazazi - Mit. 17:25.

Huwadharau wazee wao - Ayabu 19:18.

Kwa Njia Nyingine Watoto Ni Mfano Kwa Watu Wazima:

Watu wazima wanapaswa kuupokea ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo - Marko 10:15; Luka 18:17.

Ufalme wa Mungu ni wao - Marko 10:14; Mt. 19:13.

Wale wasiotubu na kuwa kama watoto wadogo hawatauingia ufalme wa Mungu hata kidogo - Mt. 18:3.

Wanapaswa kujinyenyekesha kama watoto wadogo - Mt. 18:4.

Katika uovu iweni watoto wachanga - 1 Kor. 14:20.

Wakristo Ni Watoto Wa Mungu:

Wamezaliwa mara ya pili kwa maji na kwa Roho - Yn. 3:3-5.

Wale wanaompokea Kristo ni watoto wa Mungu - Yn. 1:12.

Ni watoto wa Mungu kwa njia ya imani - Gal. 3:23, 27.

Watendao haki ni watoto wa Mungu - 1 Yoh. 3:10.

Wale wanaoongozwa na Roho ni watoto wa Mungu - Rum. 8:14.

Roho hushuhudia pamoja na roho zao kwamba wao ni watoto wa Mungu - Rum. 8:16.

Wanaitwa watoto wa Mungu na ndivyo walivyo - 1 Yoh. 3:1.

Wao ni watoto wa nuru - Yn. 12:36; Efe. 5:8; 1 The. 5:5.

Wao ni watoto wapendwao - Efe. 5:1.

Wao ni watoto watiifu - 1 Pet. 1:14.

Wao ni watoto wa ufufuo - Luka 20:36.

Lakini wengine huwa “watoto wa uasi” - Efe. 5:6; Kol. 3:6.

Watu wa aina hiyo watakuwa “wana wa laana” - 2 Pet. 2:14.

Watoto Huzaliwa Pasipo Dhambi (Hawana Dhambi). Angalia Dhambi.

**Watu Wema Wataokoka?**

Tunatakiwa Kuwa Watu Wema Ambao Tunamfuata Mungu.

Nyayo za mtu mzuri ziliamuru toka kwa Mungu - Zab. 37:23.

Mungu anampenda mtu mwema - Mith. 12:2.

Mtu mwema ataridhika - Mith. 14:4.  
Mtu mwema anazaa vitu vizuri - Mat. 12:35; Lk. 6:45.  
Watu watakufa kwa mtu mwema - Rum. 5:7.

#### Je, Watu Wote Wema Wataokoka?

Hatuokolewi kwa matendo - Efe. 2:8-9.  
Bila damu ya Yesu hakuna mwenye haki - Rum. 3:9-10.  
Kornelio alikuwa mtu mzuri lakini hakuokolewa mpaka alipobatizwa - Mdo. 10.

### **Wema (Upole)**

#### Mifano Dhahiri Ya Watu Wapole:

Musa alikuwa mpole sana zaidi ya wanadamu wote wa siku zake - Hesabu 12:3.  
Paulo - 1 The. 2:7; 2 Kor. 3:5.  
Yesu Kristo ni Mfano Mkuu wa upole - Mt. 11:29; 21:5; 2 Kor. 10:1.

#### Wakristo Wanapaswa:

Kuufuata upole - 1 Tim. 6:11.  
Kujivika utu wema na upole - Kol. 3:12.  
Kulipokea neno kwa upole - Yak. 1:21.  
Kuwajibu watu kwa upole - 1 Pet. 3:15.  
Kuonyesha upole wote kwa watu wote - Tito 3:2. Kuwaonya wale washindanao kwa upole - Gal. 6:1.  
Kuenenda katika upole wa hekima - Yak. 3:13.  
Kujivika upole ambao ni tunda la Roho - Gal. 5:23.  
Wanawake wanapaswa kujipamba kwa mapambo ya roho ya upole - 1 Pet. 3:1-4.

### **Wivu**

#### Wakati Mwingine Wivu Ni Kitu Kizuri:

Mungu ni mwenye wivu - hataki watu waiabudu miungu mingine - Kut. 20:5; 34:14; Kum. 4:24.  
Mungu aliona wivu kwa ajili ya nchi yake - Yoeli 2:18.  
Elia aliona wivu kwa ajili ya Mungu - 1 Fal. 19:10, 14.  
Mume anaweza akamwonea mkewe wivu - Hes. 5:14, 29; Mit. 6:34.  
Paulo aliwaonea Wakorintho wivu, wivbu wa Mungu ili kwamba wasidanganywe na Shetani - 2 Kor. 11:2-3.

#### Lakini Wivu Ni Kitu Kibaya Unapowatenganisha Wanadamu:

Raheli alimwonea Lea wivu - Mwa. 30:1.

Wafilisti walimwonea Isaka wivu (husuda) - Mwa. 26:14.  
Ndugu za Yusufu walikuwa na wivu - Mwa. 37:11; Mdo. 7:9.  
Hatupaswi kuwahusudu (kuwaonea wivu) wabaya - Mit. 24:19.  
Hatupaswi kuwaonea wivu wale wajivunao - Zab. 73:3.

#### Mungu Ni Mungu Mwenye Wivu, Anatafuta Upendo Wetu Wote:

Mungu ni mwenye wivu - Kumb. 5:9; Kut. 20:5.  
Mungu anataka upendo wetu - Kum. 6:5.  
Yesu alisema tunapaswa kumpenda Mungu kuliko mwingine awaye yote - Mt. 22:37.  
Tunapaswa kuatafuta ufalme wake kwanza - Mt. 6:33.  
Haiwezikani kwa mtu ye yote kuwatumikia mabwana wawili - Mt. 6:24.  
Kufuata miungu mingine au mapokeo ya wanadamu ni kuzini kiroho - Yer. 3:1, 6, 9.

#### **Je, Yesu Amesharudi?**

Je, Yesu atarudi? - Ebr. 9:28.  
Je, Yesu atarudi kwa siri? - Ufu. 1:7; Mat. 24:26.  
Je, Dunia bado ipo? - 2 Pet. 3:3-10.  
Je, Waliokufa wameshafufuka? - Mdo. 24:15.

#### **Yesu Kristo**

#### Kristo Kuhusiana Na Unabii Na Utimilifu:

Uzao wa mwanamke - Mwa. 3:15; Gal. 4:4; 1 Tim. 2:15.  
Uzao wa Ibrahimu - Mwa. 12:3; 22:18; Gal. 3:16; Mdo. 3:25-26.  
Amezaliwa na Bikira - Isa. 7:14; Mt. 1:18-25; Lk. 1:26-35.  
Kuzaliwa mjini Bethlehemu - Mika 5:2, 3; Mt. 2:1-6; Lk. 2:4; Yn. 7:42.  
Kabila ya Yuda - Mwa. 49:9; Mika 5:2-3; Mt. 1:2; Ebr. 7:14; Ufu. 5:5.  
Ukoo wa Daudi - 2 Sam. 7:12-16; Zab. 89:3-4; Isa. 9:6-7; Yer. 23:5; Mt. 1:1-6; Yn. 7:42; Ufu. 5:5; 22:16.  
Mateso yake - Zab. 22:1, 7, 18; Isa. 50:6; 53:1-12; Mt. 26:31; Lk. 24:25-26; Yn. 1:29; Mdo. 8:32-35.  
Kifo msalabani - Zab. 22:16; Mt. 20:18-19; Yn. 3:14; 12:32-33; Flp. 2:8.  
Maziko yake - Zab. 16:10; Yona 1:17; Mt. 12:40; 16:4; 27:63; Yn. 2:18-22; Mdo. 2:17-32.  
Kufufuka kwake - Zab. 2:1-9; 110:1-2; Mk. 16:19; Mdo. 2:33-36; Efe. 1:20-23; 1 Pet. 3:22.

#### Kristo Ameitwa:

Adamu wa Mwisho - 1 Kor. 15:45.  
Alfa na Omega, mwanzo na mwisho - Ufu. 22:13.  
Amina - Ufu. 3:14.  
Mtume - Ebr. 3:1; Yn. 3:17; 5:36; 6:29.



Mpatanishi - 1 Tim. 2:5.  
 Mjumbe - Ebr. 12:24; Mwombezi - 1 Yoh. 2:1.  
 Mfalme - Mt. 2:2; 21:15; Yn. 18:36; Ufu. 17:14; 19:16.  
 Bwana - Mdo. 2:36; Rum. 10:9; Flp. 2:11.  
 Mchungaji mwema - Yn. 10:1-14; Ebr. 13:20; 1 Pet. 2:25; 5:4.  
 Imanueli - Isa. 7:14; Mt. 1:23.  
 Ajabu - Isa. 9:6.  
 Mshauri - Isa. 9:6.  
 Mungu - Isa. 9:6; Yn. 1:1, 2; 20:28; 1 Yoh. 5:20; Mdo. 20:28.  
 Baba wa milele - Isa. 9:6.  
 Mfalme wa amani - Isa. 9:6.  
 Shahidi mwaminifu - Ufu. 1:5; 3:14.  
 Mtawala - Mt. 2:6; Mdo. 5:31; Ebr. 2:10.  
 Kuhani Mkuu - Ebr. 3:1; 4:14; 7:26; 8:1.  
 Kichwa cha kanisa - Kol. 1:18; Ebr. 1:22, 23; 5:23.  
 Mwana - Kondoo - Yn. 1:29; Mdo. 8:32-35; Ufu. 5:6; 7:14; 1 Pet. 1:18, 19.  
 Simba - Ufu. 5:5.  
 Mkuu wa uzima - Mdo. 3:15.  
 Ufufuo wa uzima - Yn. 11:25; 5:28, 29; 10:10; 20:31.  
 Mwokozi - 1 Yoh. 4:14; Flp. 3:20; Efe. 5:23; Mdo. 4:12.  
 Mtiwa mafuta (Masihi) - Dan. 9:25; Yn. 1:41; 4:25.  
 Neno - Yn. 1:1, 2; 1 Yoh. 1:1; Ufu. 19:13.  
 Yesu - Mt. 1:21, 25; Lk. 2:21; Mdo. 13:23; 10:38; Efe. 2:9.  
 Mtu. Yn. 19:5; Mdo. 2:22; 1 Tim. 2:5.  
 Mwana wa Daudi - Mt. 1:1; Lk. 1:32; 2 Tim.2:8; Ufu. 5:5; 22:16.  
 Mwana wa Mungu - Mk. 1:1; Mt. 16:16; Yn. 11:27; 1 Yoh. 5:11-13; 4:15.  
 Mwana wa Adamu - Dan. 7:13, 14; Mk. 2:27, 28; Mt. 12:31, 32; Lk. 19:10; Mdo. 7:56.  
 Mtumishi wa Mungu - Isa. 42:1-4; 53:11; Mt. 12:14-21; Mk. 10:45.  
 Tabibu - Mt. 9:11-13; Mk. 2:17; Lk. 5:30-32; 4:23.  
 Nabii - Kum. 18:18, 19; Yn. 1:21; Lk. 4:24; 13:33; Mdo. 3:22-26; 7:37; Mt. 17:5; Ebr. 1:1.  
 Jiwe - Mk. 12:1-11; Mdo. 4:11; Rum. 9:32, 33; 1 Pet. 2:6-8; Efe. 2:20.  
 Bwana - arusi - Mt. 9:14, 15; 2 Kor. 11:2; Efe. 5:22, 23; Ufu. 19:7; 21:9.  
 Mkate wa uzima - Yn. 6:35-68; Ufu. 2:17.  
 Nuru ya ulmwengu - Yn. 8:12; 9:5; 12:35, 36, 46; 3:19-21.  
 Njia - Yn. 14:6; Angalia Efe. 2:18; Ebr. 10:19, 20; Mdo. 9:2; 19:9.  
 Kweli - Yn. 14:6; 1:14; 8:32; 18:37; 1 Yoh. 5:20.  
 Uzima - Yn. 14:6; 1:4; 5:26; 11:25; 1 Yoh. 5:11-13, 20.  
 Hakimu - Yn. 5:22, 27; 12:47, 48; Mdo. 10:42; 17:31; 2 Tim. 4:1; 2 Kor. 5:10; Mt. 25:31-46.  
 Mwenye haki - Mdo. 3:14; 7:52; 22:14; 1 Pet. 3:18; 1 Yoh. 2:1.  
 Ni Mwamba - Mt. 16:18; 1 Kor. 10:1-3.  
 Ni Msingi - 1 Kor. 3:11.

### Tabia Za Kristo:

Mtakatifu - Lk. 1:35; Ufu. 3:7; Mdo. 3:14.  
Mwenye haki - Isa. 53:11; Mdo. 3:14; 22:14; 1 Yoh. 2:1.  
Hana hila - Isa. 53:9; 1 Pet. 2:22.  
Hana dhambi - Yn. 8:46; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Yoh. 3:5.  
Hana ila wala mawaa - 1 Pet. 1:19; Ebr. 9:14. Mwaminifu - Isa. 11:5; 2 The. 3:3; 2 Tim. 2:13.  
Amejaa neema na kweli - Yn. 1:14; 7:18; 1 Yoh. 5:20; Ufu. 3:7.  
Humtii Baba yake - Yn. 4:34; 6:38; 15:10; Ebr. 5:8.  
Mnyenyekevu wa moyo - Isa. 53:7; Mt. 11:29; Flp. 2:8.  
Mwenye huruma - Lk. 7:13; 19:41; Efe. 2:17; 4:15.  
Mvumilivu - 1 tim. 1:16.  
Mwenye upendo - Yn. 13:1; 15:13; 10:15.  
Hujitolea mwenyewe - Mt. 8:20; 2 Kor. 8:9.  
Husamehe - Lk. 23:34.

#### Kristo alikuwa Mwanadamu:

Alizaliwa na mwanamke - Lk. 1:20, 31; Mt. 1:24, 25; Gal. 4:4.  
Alikuwa na damu, na mwili - Yn. 1:14; Ebr. 2:14.  
Alikuwa na maisha ya kimwili - Mt. 26:38; Lk. 23:46.  
Alizidi kuendelea katika hekima na kimo - Lk. 2:52.  
Aliona njaa - Mt. 4:2; 21:18.  
Aliona kiu - Yn. 4:7; 19:28.  
Aliweza kuchoka - Yn. 4:6.  
Aliweza kulala - Mt. 8:24; Mk. 4:38.  
Aliweza kulia - Lk. 19:41; Yn. 11:35.  
Mtu wa huzuni nyingi na masikitiko - Isa. 53:3, 4; Lk. 22:44; Yn. 11:33; 12:37.  
Alitendwa jeuri - Mt. 26:67; Lk. 22:63-65; 23:11; 1 Pet. 2:23.  
Alipigwa mijeledi - Mt. 27:26; Yn. 19:1.  
Alisulubiwa msalabani - Lk. 23:33; Yn. 19:18.  
Aliwekwa kaburini - Mt. 27:59, 60; Mk. 15:46.  
Alijinyenyekeza - Flp. 2:6-8.  
Alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote - Ebr. 4:15.  
Alikuwa hana dhambi - Ebr. 4:15; 1 Yoh. 3:5.  
Yeyote akataaye kwamba Yesu Kristo hajaja katika mwili ni mpinga Kristo - 1 Yoh. 4:2, 3; 2 Yoh. 7.

#### Uungu Wake - Maneno Yaliyosemwa Kuhusiana Na Mungu Baba Pia Yalisemwa Kuhusiana Na Kristo:

Mungu (Bwana) - Isa 40:3; Mt. 3:3; Lk. 3:4; Yn. 1:23, 27, 29.  
Mwanzo na Mwisho - Isa. 44:6; 48:12; Ufu. 1:8, 17; 22:13.  
Bwana wa majeshi - Isa. 6:1-3; 8:13, 14; Yn. 12:41; 1 Pet. 3:15.  
Muumba wa milele - Zab. 102:24-27; Ebr. 1:8-12; Yn. 1:1-3.  
Mungu asiyebadilika - Zab. 102:27; Mhu. 3:6; Ebr. 13:8.

Mfalme wa Utukufu - Zab. 24:7, 10; 1 Kor. 2:8; Yak. 2:1.  
 Mungu mkuu - Isa. 1:24; 9:6; Tito 2:13.  
 Baba wa milele - Isa. 63:16; Mt. 5:16; Isa. 9:6.  
 Mungu wa kweli - Yer. 10:10; 1 Yoh. 5:20.  
 Bwana wa wote - Yer. 45:23; Mdo. 10:36; Rum. 10:12; Flp. 2:10, 11.  
 Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme - Kum. 10:17; Zab. 136:3; 1 Tim. 6:15; Ufu. 17:14; 19:16.  
 Hakimu - Mhu. 12:14; 1 Kor. 4:5; 2 Kor. 5:10.  
 Chanzo cha Baraka za kiroho - 2 The. 2:16, 17; 2 Kor. 13:11.  
 Haki yetu - Yer. 23:5, 6; 1 Kor. 1:30.  
 Mkombozi - Isa. 44:6; Mk. 10:45; 1 Tim. 2:6; Ebr. 9:15; 1 Pet. 1:18, 19.  
 Mchungaji - Zab. 23:1; Isa. 40:10, 11; Yn. 10:11, 14; 1 Pet. 2:25; Ebr. 13:20.  
 Anapaswa kuheshimiwa kama vile Baba - Yn. 5:23.  
 Aliabudiwa sawa na Mungu Baba - Mt. 28:17; Ufu. 5:12-14.  
 “Bwana wangu na Mungu wangu” - Yn. 20:28.

### Kazi Za Kristo - - Yesu Alikuwa Duniani:

#### Kumfunua Mungu Baba:

1. Yeye pekee ndiye alijua kumfunua Baba - Mt. 11:25-27.
2. Hapo mwanzoni alikuwa pamoja na Mungu lakini akafanyika mwili ili amdhihirishe Baba - Yn. 1:1, 2, 14, 18.
3. Aliyemwona Mwana amemwona Baba pia - Yn. 14:7-9.
4. Yeye ni mfano wa Mungu - Kol. 1:15.
5. Yeye ni chapa ya nafsi yake - Ebr. 1:13.
6. Alionyesha kwamba Mungu ni Baba wa Upendo - Mt. 6:25-34; 10:29-31.
7. Alionyesha kwamba Mungu mwenyewe humpenda kila mtu - Lk. 15; Mt. 18:10-14.

#### Kuondoa dhambi - 1 Yoh. 3:5.

1. Damu ya wanyama haiwezi kuondoa dhambi - Ebr. 10:4.
2. Lakini waaminifu wa Agano la Kale walisamehewa - Isa. 1:18; Zab. 103:12; Mika 7:19.
3. Mungu alikuwa na uwezo kufanya hivyo kwa kuwa alijua kwamba Yesu atakuja afe kwa ajili yao pia - 1 Pet. 1:18-21; Mdo. 2:23; 13:27-40; Ebr. 9:15.
3. Yesu alijitua mwenewe mara moja tu ili aziondoe dhambi - Yn. 1:29; 1 Kor. 15:1-4; Efe. 1:7; Ebr. 9:14, 28.

#### Kuziharibu kazi za Ibilisi - 1 Yoh. 3:8.

1. Kazi za Ibilisi:
  - a. Muuaji - kwa kuangamiza maisha - Yn. 8:44.
  - b. Mwongo - kwa kuharibu nuru na kweli - Yn. 8:44.
  - c. Muasi - kwa kuvunja sheria - 2 The. 2:8.
2. Yesu aliziharibu kazi zake:
  - a. Aliliharibu giza kwa kufanya nuru iangaze - Yn. 1:4; 8:12.
  - b. Aliharibu mauti kwa kutoa uhai - Yn. 1:4; 10:10; 17:3.
  - c. Aliharibu uongo kwa kufundisha kweli - Yn. 14:6; 8:32.
  - d. Aliharibu chuki kwa kuonyesha upendo - Yn. 13:34, 35.

Ili awe kuhani mkuu aliye na huruma na mwaminifu:

1. Alikuwa Mungu akafanyika mwili - Yn. 1:1,2, 14.
2. Kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanojaribiwa - Ebr. 2:17, 18.
3. Alijaribiwa katika mambo yote kama sisi - Ebr. 4:14-16.
4. Yeye ni Mwombezi wetu kwa Baba - 1 Yoh. 2:1, 2.
5. Yeye ndiye anayetuomba - Rum. 8:34; Ebr. 7:25.

Kazi tatu ambazo huendelea kuzifanya:

1. Huwatawala watu wake kama mfalme wa wafalme - Mdo. 2:32-36; Ufu. 1:5, 17:14; 19:16.
2. Husema katika maandiko mtakatifu kama Nabii wa Mungu - Mdo. 3:22, 23; Mt. 17:5; Ebr. 1:1, 2; 12:25.
3. Huwaomba watu wake kama Kuhani Mkuu - Rum. 8:34; Ebr. 7:25; 1 Yoh. 2:1.

### Ufufuo Wa Kristo:

Yesu alitabiri juu ya ufufuo wake - Yn. 2:19-22; Mt. 16:21; 17:9; Yn. 10:18.

Vitabu vinne vyote vya Injili hushuhudia kwamba alifufuka kutoka kwa wafu - Mt. 28; Mk. 16; Lk. 24; Yn. 20-21.

Mitume wake waliendelea kuhubiri juu ya ufufuo wake kila mara - Mdo. 2:22-36; 3:15; 4:10; 5:30, 31; 13:30, 31; 36:8, 23.

Maana ya ufufuo wa Kristo kwetu:

1. Alidhihirishwa kuwa Mwana wa Mungu - Rum. 1:4.
2. Twahebiwa haki kwa sababu ya ufufuo wake - Rum. 4:25; 10:9.
3. Tumezaliwa mara ya pili ili tupate tumaini la uzima - 1 Pet. 1:3-5.
4. Ufufuo wake huuthibitisha ufufu wetu wa uzima wa milele - 1 Kor. 15:50-58; 1 The. 4:14-18.
5. Bila ufufuo tungekuwa wenye dhambi wasio na tumaini kwa Mungu - 1 Kor. 15:12-19.

### Baraka Tuzipokeazo Tuwapo Ndani Ya Yesu:

Uzima wa milele - 1 Yoh. 5:11.

Hakuna hukumu kwa wale walio ndani ya Kristo - Rum. 8:1.

Tu viumbe vipya - 2 Kor. 5:17.

Tunapata ukombozi katika Yesu - Efe. 1:7.

Tunao msamahe - Efe. 1:7; Kol. 1:14.

Wokovu u katika Yesu - 2 Tim. 2:10; Mdo. 4:12.

Baraka zote za kirohoni zimo ndani ya Yesu Kristo - Efe. 1:3.

Njia ya kuingia ndani ya Kristo ili kuzipokea hizo baraka ni ubatizo - Gal. 3:26, 27.

(Angalia somo juu ya DHAMBI, “Njia ya Msamaha wa Dhambi.”)

### **Yesu ni Mwana wa Mungu.**

### Manabii Walifundisha Baba Atatumwa Mtoto Wake Kwa Ajili Ya Ulimwengu.

Isaya alitabiri Yesu atakuja kupitia bikira - Isa. 7:4.  
Atazaliwa Bethlehemu - Mik. 5:2.  
Atatoka kwenye uzao wa Daudi - 2 Sam. 7:12.  
Atakuwa mtu mwenye huzuni sana - Isa. 53:12.  
Atakataliwa na watu wake - Zab. 69:8.  
Atauzwa na rafiki yake - Zab. 41:9.  
Atasulubiwa kati ya wezi wawili - Isa. 53:12.  
Wakati atakufa roho yake itarudi kwa Baba - Zab. 31:5.  
Atafufuka toka kwa wafu - Zab. 16:10.  
Atachukua nafasi yake kwenye mikono ya kulia ya Mungu - Zab. 110:1.

Kwa Upendo Wa Mungu Alitumwa Mwana Wake Aliyetukomboa.

Kwa sababu aliupenda ulimwengu - Yn. 3:16.  
Bila kuamini Mwana wa Mungu hatuwezi kumwona Baba - Yn. 3:18.

Kama Kuhani Anayetuokoa Sisi na Anatuongeza Katika Ufalme Wake.

Mungu alimchagua Yeye iliaponye watu - Lk. 4:18-19.  
Kwa watu ambao watatubu na kubatizwa wataingia katika ufalme wake - Mdo. 2:36-47.  
Ufalme wake siyo wa ulimwengu huu - Yn. 18:36.  
Alitumikia kwa kutumwa watu - Mat. 20:25-28.  
Kama kuhani alitoa mwenyewe kwa sababu damu ya wanyama haifai - Yoh. 10:11-18; Ebr. 9:12.